# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

# KISWAHILI

*Mkusanyiko huu unatoa mkusanyiko uliopangwa kwa utaratibu wa tathmini zilizoigwa, iliyoundwa mahususi kwa ajili ya KCSE 2025. Kila tathmini imeundwa kwa uangalifu ili kuendana na mahitaji ya mtaala, na hivyo kuwapa wanafunzi uzoefu wa kina wa mazoezi.*

## *(INAJUMUISHA KARATASI 1, 2 & 3)*

## (JARIBIO LA KCSE 1-10)

*Kwa Miradi ya Kuashiria*

*Bw Isaboke 0746 222 000 / 0742 999 000*

# MAFANIKIO KWA WAGOMBEA WOTE!

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 1

**102/1**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 1 (INSHA)**

**MUDA: SAA 1¾**

**NAME**……………………………………………………………………………………

**SCHOOL**…………………………………………………… **SIGN**…………………………

**INDEX NO**………………………………………………… **ADM NO**……………………

***Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)***

**MAAGIZO**

**a)** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
**b)** *Andika insha **mbili**. Insha ya **kwanza** ni ya **lazima.***
**c)** *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya tatu zilizobakia.*
**d)** *Kila insha isipungue maneno **400***
**e)** *Kila insha ina alama **20***

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 40 | |

1. **LAZIMA.**

Umepata tangazo la nafasi ya kazi ya uhariri katika shirika la uchapishaji wa vitabu vya fasihi andishi kwenye gazeti la Taifa Leo. Andika barua ya kuomba nafasi hii na uambatanishe na wasifu kazi wako kwa maelezo zaidi. **(Alama 20)**

2. Utelekezaji wa mtoto wa kiume nchini ni janga kuu. Jadili. **(Alama 20)**

3. Andika insha inayoafikiana na methali Baniani mbaya kiatu chake dawa. **(Alama 20)**

4. Andika insha itakayomalizikia kwa; …walipofungua mlango huo hatimaye,wengi hawakuweza kuzuia hisia zao.Waliangua vilio kwa maafa waliyoyashuhudia. **(Alama 20)**

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**

***KILA LA HERI!***

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 1

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2 (LUGHA)**

**MUDA: SAA 2½**

**NAME……………………………………………………………………………………**

**SCHOOL……………………………………………… SIGN…………………………**

**INDEX NO……………………………………………… ADM NO……………………**

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**Maagizo**

***(a)Andika*** *jina na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

***(b)****Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani*

***(c)*** *Jibu maswali yote.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 4 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| | | |

**1.UFAHAMU (alama 15)**

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali</u>***

Suala la mahusiano ya wanadamu katika jamii, uainishaji wake na udhihirikaji wake limewashughulisha wataalamu wa elimu jamii kwa dahari ya miaka. Suala hili huwatafakarisha wataalamu hao kutokana na umuhimu wake katika maisha ya binadamu. Msingi mkuu wa uainishanji wa mahusiano hayo ni kukichuza kipindi cha mahusiano yenyewe. Yapo mahusiano bainaya waja ambayo yanachukua muda mfupi, kwa mfano saa au dakika chache na mengine ambayo huenda yakachukua miaka ayami.

Mahusiano ya muda mrefu kabisa ni yale yanayojulikana kama mahusiano ya kudumu. Inamkinika kudai kuwa miundo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi huweza kuyadhibiti mahusiano hayo kwa kiasi kikubwa. Watu wengi huitakidi kuwa uhusiano uliopo baina ya mtu na jamaa yake utachukua muda mrefu, na kwa hiyo ni uhusiano wa kudumu. Hali hii hutokana na uhalisi kuwa tunahusiana na jamaa zetu kwa kipindi kirefu labda tangu ukembe hadi utu uzima wetu. Uhusiano huuhautarajiwi kuvunjwa na umbali wa masafa baina yetu;tunaendelea kuwasiliana kwa barua au, katika enzi hii ya utandawazi,kwa kutumia nyenzo za teknohama kama mtandao na simu za mkononi na kudumisha uhusiano wetuwa kijamaa. Hata hivyo, inawezekana baadhi ya mahusiano ya kijamaa yasiwe ya kudumu. Mathalan, uhusiano uliopo baina ya mke na mume, na ambao unatarajiwa kuwa wa kudumu au wa kipindi kirefu,unaweza kuvunjwa kwa kutokea kwa talaka. Talaka hiyo inavunja ule uwezekano wa uhusiano wa kudumu unaofumbatwa na sitiari ya pingu za maisha.

Katika ngazi ya pili,mahusiano ya kipindi cha wastani,kuna mahusiano yanayohusisha marafiki zetu maishani, shuleni au kwenye taasisi zozote zile, majirani zetu, wenzetu katika mahali mwa kazi,washiriki kwenye sehemu za ibada au za burudani na wenzetu kwenye vyama tofauti na makundi ya kujitolea. Inawezekanakudahili kuwa baadhi ya mahusiano haya,hususan baina ya marafiki na majirani huweza kuwa ya miongo na daima. Hali hii huweza kutegemea muundo na mfumo wa jamii. Kwa mfano, kwa wanajamii waoishi kwenye janibu fulani mahsusi, na kwa miaka tawili bila ya kuhajiri,uhusiano wao na majirani huweza kuwa wa kudumu. Hali hii **inasigana** na hali iliyoko kwenye maisha ya mijini. Maisha ya mijini yana sifa ya kubadilikabadilika. Isitoshe,kutokana na mfumo wa maisha ya kibepari **yameghoshi** ubinafsi mwingi. Mawimbi ya mabadiliko na ubinafsi huweza kuumomonyoaukuta wauhusiano wa kudumu.

Mwelekeo wa maisha ya siku hizi ya uhamaji kutoka maeneo au viambo walikoishi watu unasababisha kupombojea kwa mahusiano ya kudumu baina yao na majirani zao. Uhusiano katiya wenza katika mazingira ya kazi unahusiana kwa kiasi fulani na ule wamajirani.

Vimbunga vya ufutwaji kazi, ubadilishaji wa kazi, hali zisizotegemewa na mifumo ya kimataifa pamoja na hata mifumo ya kisiasahuweza kuathiri mshikamano wa wanaohusika kazini.

Kiwango cha mwisho cha mahusiano ni uhusiano wa mpito au wa muda mfupi. Mahusiano ya aina hii hujirikatika muktadha ambapo pana huduma fulani. Huduma hizi zinaweza kuwa za dukani, kwenye sehemu za ibada,kwenye kituo cha mafuta,kwa kinyozi, kwa msusi na kadhalika. Kuna sababu kadha zinazotufanya kuyazungumzia mahusiano ya aina hii kama ya mpito. Kwanza,

uwezekanowa mabadiliko ya anayeitoa huduma hiyo ni mkubwa. Si ajabu kuwa unaporudi kwa kinyozi au msusi unatambua aliyekushughulikia hayupo. Hata hivyo, kuna **vighairi** hususa pale ambapo mtoa huduma anayehusika ni yule yule mmoja.

Mahusiano ya mpito yanatawaliwa na'uhusiano wa chembe chembe.' Uhusiano wa chembe chembe, bidhaa ya mfumo wa kibepari, unamaanisha kuwa kinachoshughulisha mtu ni chembe ndogo tu ya mwenzake. Chembe hiyo inaweza kuwa huduma, kwa mfano, gazeti analokuuzia mtu, viatu anavyokushonea,nguo anazokufulia,ususi anokufanyia na kadhalika. Mahussiano ya aina hii yametovukwa na hisia za utu na ni zao la mifumo ya kisasa ya kiuchumi na kijamii. Mtu anayehusiana na mwenzakekwa misingi ya chembe ndogo tu, huenda asijali kama mwenzake amekosa chakula,amefutwa kazi,amefiliwa,ameibiwa na kadhalika.

Suala kuu tunalopaswa kujiuliza ni: je, tunahusianavipi na jamaa zetu, marafiki zetuna majirani zetu? Je, uhusianowetu na raia wenzetu ni wa aina gani? Je, uhusiano wetu na nchi yetu ni wa mpito au ni wa kudumu?

<u>**MASWALI**</u>

***(a)*** Taja kigezo cha kuzungumzia mahusiano. **(alama 1)**

***(b)*** Eleza imani ya watu kuhusu mahusiano ya watu. **(alama 1)**

***(c)*** Fafanua athari ya teknolojia kwenye mahusiano ya watu. **(alama 2)**

***(d)*** Eleza sababu **nne** kuu za kuharibika kwa mahusiano katika maisha ya leo. **(alama 2)**

***(e)*** Taja sifa kuu za mahusiano ya muda mfupi. **(alama2)**

***(f)*** Je, kifungu hiki kina ujumbe gani mkuu? **(alama2)**

***(g)*** Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu. **(alama 3)**

**(a)** inasigana

**(b)** yameghoshi

**(c)** vighairi

**2 UFUPISHO (alama 15)**

Jamii ya leo inatawaliwa na kuendeshwa na kanuni ya maarifa. Inawezekana kusema kuwauchumi wa jamii za leo na zijazo utategemea maarifa zaidi kuliko utakavyotegemea uwezo wowote mwingine. Utambuzi wa uwezo mkubwa wa maarifa katika maisha ya binadamu ndio msingi wa watu kusema 'maarifa ni nguvu.'

Maarifa huelezwa kwa tamathali hii kutokana na uwezo wa: kuyadhibiti,kuyaendesha, kuyatawalana kuyaongoza maisha ya binadamu popote pale walipo. Mtu ameyakosa maarifa fulani huwa ameikosa nguvu hiyo muhimu na maisha yake huathirika pakubwa. Kwa msingi huu, maarifa yanawezakuangaliwa kama utajiri mkubwa ambao binadamu anaweza kuutumia kwa faida yake au kwa faida ya wanajamii wenzake. Ukweli huu ndio unaoelezwa na methali ya Kiswahili: 'Elimu ni mali.' Elimu ni chimbuko la maarifa muhimu maishani.

Msingi wa utajiri na maendeleo ya binadamu popote alipo basi ni maarifa. Je, maarifa kwa upande wake yana sifa gani? Maarifa yenyewe hayana upinzani. Maarifa uliyo nayo huweza kuwa

na watu wengine pasiwe na upinzani baina yenu kwa kuwa kila mmoja ana maarifa sawa. Kila mmoja ana uhuru wa kuyatumia maarifa hayo kama chanzo cha kuyazalisha mengine. Utumiaji wa maarifa yenyewe hauyamalizi maarifa hayo. Maarifa hayawezi kugusika ingawa mtu anaweza kuyanyumbua maarifa yenyewe kwa kuyatumia kwa namna tofauti.

Maarifa huingiliana na maarifa mengine. Maarifa aliyo nayo mtu huweza kuhusishwa na maarifa aliyo nayo mtu mwingine ili kuvyaza au kuzuka na maarifa tofauti. Maarifa yanaweza kuchukuliwa kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa namna ambavyo mtu huweza kufanya bidhaa nyingine ile. Kwa mfano, ni muhali mtu kulalamika kuwa hawezi kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa sababu ana mzigo wa maarifa kichwani.

Sifa nyingine muhimu ya maarifa ni kuwa yanaweza kuwasilishwa kwa njia au mitindo mingine ya kidhahania. Ikiwa unataka kukihamisha chombo fulani kutoka sehemu moja hadi nyingine, lazima uwazie ukubwa wake, uzito wake na labda hata umbali wa panapohusika. Maarifa huweza kubadilishwa au kugeuzwa na kuwa ishara ambazo huyafanya kuwasilishswa kwa njia nyepesi kuliko kwa mfano ikiwa mtu atayawasilisha katika muundo wa, kwa mfano,kitabu.

Maarifa yana sifa ya uhusianaji. Kipengele fulani cha maarifa huwa na maana kinapowekwa sambabmba au kugotanishwa na kipengele kingine cha maarifa. Huo huwa muktadha mzuri wa kueleweka au kuwa na maana kwa mfano, neno 'mwerevu' huweza kuwa na maana kwa kuwekwa katika muktadha wa 'mjinga', ' mjanja', 'hodari' na kadhalika.

Maarifa huweza kunifadhiwa katika nafasi ndogo sana. Suala hili linaeleweka kwa njia nyepesi tunapoangalia maarifa katika muktadha wa teknolojia. Data zinazowahusu mamilioni ya watu,ambazo zingehitaji maelfu ya maktaba na lukuki ya vitabu, huweza kuhifadhiwa kwenye kifaa kidogo kinachoweza kutiwa mfukoni.

Maarifa hayawezi kuthibitiwa au kuzuiliwa mahali fulani yasisambae. Maarifa huenea haraka sana. Maarifa ni kitu kinachoepuka pingu za watu wanaopenda kuwadhibiti binadamu wenzao. Hata pale ambapomfumo wa kijamii au wa kisiasa unafanya juu chini kuwadhibiti raia au watu wenyewe,ni muhali kuyadhibiti maarifa yenyewe. Inawezekana kuzidhibiti njia fulani za uenezaji wa maarifa lakini maarifa hayo yatapata upenyu wa kusambaa. Ni kweli kuwa maarifa ni nguvu inayozishinda nguvu zote.

**(a )** Fupisha aya ya pili na tatu **(maneno 55-60)(alama 5, 1 ya utiririko)**

**(b)** Eleza sifa kuu za maarifa kama zinavyojitokeza kuanzia aya ya nne hadi aya ya nane.
**(maneno 100-110) (alama 10, 2 za utiririko)**

**3 MATUMIZI YA LUGHA** **(alam 40)**

**(a)** Taja vipasuo sighuna **(alama**

Tunga sentensi yenye muundo ufuatao:
kirai nomino, kirai tenzi, kirai husishi **(alama 2)**

**(c )** Bainisha shamirisho na chagizo katika sentensi **(alama 2)**

Vibarua wamefanya kazi haraka ipasavyo .

**(d)** SahihishaMwalimu mwenye alikuja jusi anafudisha Kiswahili vizuli. **(alama 2 )**

**(e)** Yakinisha sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Hakuwapiga wala kuwalaghai.

**(f)** Eleza viambishi katika neno lifuatalo **(alama 3)**

Walichokilalia

**(g)** Bainisha vivumishi vilivyo katika sentensi ifuatayo: **(alama 2)**

Wanafunzi wote wenye nidhamu watapewa tuzo kubwa na mwalimu wao.

**(h)** Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mistari au mishale **(alama 4)**

Yohana na Otieno hucheza kandanda.

**(i)** Andika sifa tatu zinazobainisha sentensi changamano**.** **(alama 3)**

**(j)** Geuza sentensi ifuatayo iwe katika usemi halisi. **(alama2)**

Askari jela alimwuliza Kendi kama alidhani hapo ni kwao. Alimwamuru aende kwake mara moja.

**(k)** Toa mfano wa neno lenye muundo ufuatao wa silabi. **(alama1)**

IK+KI+KI+KI

**(l)** Onyesha matumizi ya viakifishi vifuatavyo. **(alama 2)**

(i) kibainishi

(ii) parandesi

**(m)** Tumia neno –baya kama: **(alama 2)**

(i) kiwakilishi

(ii) kielezi

**(n)** Tunga sentensi sahili ukitumia kitenzi ‘la’ katika kauli ya tendewa. **(alama 2)**

**(o)** Badilisha maneno yaliyopigiwa mstari yawe vitenzi**.** **(alama 2)**

Yunis amepata <u>faida</u> kutokana na <u>ukulima</u>.

**(p)** Kwa kuzingatia maagizo andika upya sentensi ifuatayo: **(alama2)**

Tinga amewafanya ng’ombe wake wanywe maji.

(Anza kwa : Mifugo wangu …………..usitumie ‘amewafanya’)

**(q)** Onyesha miundo miwili ya nomino za ngeli ya U-U. **(alama 2 )**

**(r)** Bainisha maana mbili zinazojitokeza kutokana na sentensi hii. **(alama2)**

Umu alimwandikisha mkewe.

**(s)** Tunga sentensi katika wakati uliopo hali isiyodhihirika. **(alama 1)**

**4. <u>ISIMUJAMII</u>** **(Alama 10)**

**(a)** Lahaja huainishwa katika makundi **mawili**. Yataje **(alama 2)**

**(b)** Eleza sifa zozote **nne** za lugha ya taifa. **(alama 4)**

**(c)** Tolea ushahidi namna **nne** kwamba Kiswahili ni lugha ya kimataifa. **(alama 4)**

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 1

**102/3**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 3 (fasihi)**

**MUDA: SAA 2½**

**NAME……………………………………………………………………………………**

**SCHOOL………………………………………………… SIGN…………………………**

**INDEX NO……………………………………………… ADM NO……………………**

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

- **a)** *Andika jina lako, nambari ya usajili, mkondo, sahihi na tarehe katika nafasi ulizoachiwa.*
- **b)** *Jibu maswali **manne** pekee.*
- **c)** *Swali la kwanza ni la **lazima**.*
- **d)** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Fasihi Simulizi.*
- **e)** *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
- **f)** ***Maswali yote ni sharti yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.***

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

## SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI

**1.** ***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali***.

(*Wazee wanne wa umri wa makamo wameketi kuunda mduara. Katikati ya mduara huo, kuna babu aliyempakata mtoto mdogo. Mtoto aliyepakatwa ni mdogo na ambaye hajafika umri wa kuzungumza*. *Babu ameshika ugoro mkononi*)

**Babu**: (Kwa mtoto) Unaitwa nani? (Mtoto ananyamaza tu. Anaonekana kutoelewa yanayofanyika katika mazingira yake) Unaitwa nani? Je, Wewe ni Kipkech?

**Wazee**: (Kwa pamoja) Huyu siye Kipkech. Amekataa kabisa.

**Babu**: (Akimpaka mtoto ugoro puani.) Unaitwa nani? Tuambie jina lako. Wazee wamechelewa kupeleka mifugo malishoni. Unaitwa Kipsimam? ... Maritim? Je, unaitwa Nusu?

**Mzee I:** Ni kama huyu mzee amejificha. Ama alikuwa mwoga alipokuwa hai? Ama amekasirika? Mwongezee ugoro. Huenda anataka zawadi ili ajitambulishe.

**Babu**: (Akimpaka mtoto ugoro puani.) Je, Unaitwa Chepkiyeng? (Mtoto anaenda chafya) Oyee! Karibu Chepkiyeng. Karibu nduguye Nusu. Karibu mzee wetu wa bidii.

**Wazee**: (Wakishangilia) Karibu Chepkiyeng. Mzee mwanzilishi wa maduka tunayotumia hadi sasa. Karibu babu yetu! (Wote wanaanza kunywa buzaa iliyo mtungini kwa mrija huku wakizungumza kwa furaha.)

### Maswali

**(a)** Ainisha kipera hiki cha fasihi simulizi. **(alama 2)**

**(b)** Bainisha sifa za utanzu ambapo kipera hiki kimetolewa. **(alama 4)**

(c) Umepewa nafasi ya kuwasilisha utanzu huu mbele ya hadhira. Eleza sifa **nne** unazofaa kuwa nazo. **(alama 4)**

(d) Bainisha shughuli **mbili** za kiuchumi katika jamii inayorejelewa katika kifungu hiki. **(alama 2)**

(e) Umeamua kutumia kalamu na karatasi (maandishi) kukusanya na kuhifadhi data ya fasihi simulizi. Eleza udhaifu wa mbinu hiyo. **(alama 4)**

(f) Fafanua changamoto **nne** zinazoweza kukukabili nyanjani, unapoenda kukusanya data kuhusu kipera hiki. **(alama 4)**

## SEHEMU YA B: TAMTHILIA

**T.M. Arege:** *Bembea ya Maisha*

*Jibu swali la 2 au 3*

**2.** "Japo nilipungukiwa na mengi niliyoyatamani, nilitaka nyinyi muote mbawa mpae juu angani na kuitazama dunia kutoka kule juu kwa niaba yangu."

**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

**b)** Bainisha aina **mbili** za taswira zinazojitokeza kwenye dondoo. **(alama 4)**

**c)** Onyesha toni inayopatikana kwenye dondoo hili. **(alama 2)**

**d)** Eleza umuhimu wa mandhari ya dondoo hili. **(alama 4)**

**e)** Fafanua sifa za msemewa katika dondoo hili. **(alama 6)**

**3.** a) Onyesha jinsi mwandishi alivyotumia mbinu ya kinaya kujenga hadithi ya **Bembea ya Maisha**. **(alama 10)**

b) **Bembea ya Maisha** ni tamthilia ya mabadiliko. Thibitisha. **(Alama 10)**

## SEHEMU YA C: RIWAYA

**C. Momanyi:** *Nguu za Jadi*

*Jibu swali la 4 au la 5*

**4. Kamwe** hangekubali kuwa mtu wa kuomba omba misaada na ufadhili kutoka kwa wale walio navyo. Aliumbwa mkamilifu, akili timamu na siha mwilini. Kwa nini basi aombe wale waliokirimiwa vitu kama yeye? Ni ada ya binadamu kufanya kazi ili aweze kulisukuma gurudumu la maisha.

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

b) Bainisha toni katika dondoo hili. **(alama 2)**

c) Fafanua maudhui katika dondoo hili. **(alama 3)**

d) Eleza sifa **tatu** za anayerejelewa kwa kurejelea riwaya ya **Nguu za Jadi**. **(alama 8)**

e) Fafanua jinsi wahusika mbalimbali kwenye riwaya ya **Nguu za Jadi** wanavyofanikisha kauli iliyopigiwa mstari. **(alama 8)**

**5. (a)** Changanua mtindo katika dondoo lifuatalo**.** **(alama 6)**

Kuna waliookota chupa za plastiki kwenda kuchuuza. Kuna waliobobea katika kuchakura taka ili kupata mikebe iliyotupwa. Kisha waliichuuza mjini. Ukifika majaani,kitu cha kwanza kinachokukaribisha ni harufu kali ya uvundo uliosambaa kila mahali. Kila dakika magari yaliyosaki taka kutoka katika mitaa ya mji yalifika hapa kutupa taka. Mafalahi waliochoka na maisha waliishi mahali hapa. Walisitiriwa na makombo ya vyakula kutoka katika jaa hili kuu. Walinyanganyana chakula na kunguru waliojaa mahali hapa.

b) Bainisha toni inayojitokeza katika dondoo hili. (**Alama** 2)

c) Jadili mbinu walizotumia raia wa Matuo kujikomboa kutokana na uongozi dhalimu wa Mtemi Lesulia. **(Alama12)**

## SEHEMU YA D: USHAIRI

*Jibu swali la 6 au 7*

**5. Soma shairi hili kisha ujibu maswali.**

Pindi ilipomjia, habari za binti kazaliwa
Uso ulimsawijika, kwa soni akachanganyikiwa
"Hii ni nakhusi?
Aka, na nakama!
La, ni neema!
Bali si beluwa?"

Wapi uso afiche?
Au mchangani auzike?
Izara hii asiipate!
Ya kuzaliwa mke.

Nitawatolea kisa…
Nawatangulizia sasa,

Kisa kilichoanza.,
Hakijawahi kukoma,
Kote kimeenea,
Namna wanavvomtesa,
Kiumbe dhalili wamemfanya,
Lini atathaminiwa?

Kisa chenyewe kitendawili,
Mwenyewe busara atoe tawili,
Ya haya mambo mawili,
Maisha bila mke ni awali,
Kisa kingeendelea?
Lulu iliyohifadhiwa ni ya pili,
Kisa kingeendelea?

**MASWALI**

**a)** Thibitisha kuwa shairi hili ni huru. **(alama 3)**
**b)** Eleza maudhui yanayojitokeza katika shairi hili. **(alama 2)**
**c)** Andika ubeti wa **tatu** katika lugha nathari. **(alama 4)**
**d)** Tambua matumizi ya mishata katika shairi hili. **(alama 2)**
**e)** Taja na ueleze mbinu za lugha zilizotumika. **(alama 2)**
**f)** Eleza umuhimu wa mke katika shairi. **(alama 2)**
**g)** Eleza jinsi mtunzi alivyotumia uhuru wake. **(alama 2)**
**h)** Eleza jinsi maneno haya yalivyotumika katika shairi. **(alama 3)**

- **i.** Nakama
- **ii.** Awali
- **iii.** izara

**6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Lau kama ingakuwa, madhali tuna uhuru,
Watu kodi kutotowa, na kuifanya kufuru,
Vije nchi ingakuwa, taifa bila kufuru,
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru.

Hivi taifa kumea, na kuendelea mbele,
Kwamba lajitegemea, haliwatege’i wale,
Yataka kujitolea, ushuru bila kelele,
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru.

Wafanyikazi wa umma, mfano mwema walimu,
Wauguzi mahashuma, daktari wahadimu,
Bila hizi darahima, vipi wangalihudumu?
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru.

Si vyema kuombaomba, kwa wageni kila mara,
Huwa twajifunga kamba, na kujitia izara,
Adha zinazotukumba, kujitegemea bora,
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru.

Miradi ya maendeleo, yahitaji darahima,
Ndo tufikie upeo, ulio dunia nzima,
Wadogo na wenye vyeo, bila kodi tutakwama,
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru.

Ushuru si kwa wanyonge, wasokuwa na uwezo,
Watozwe hata wabunge, na wengine wenye nazo,
Yeyote asijitenge, kodi akalipa bezo,
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru.

Kwetu kutoa ushuru, ndiko kujitegemea,
Pasiwepo na udhuru, usio wa kuelea,
Huwa ni kama kiguru, asenao kutembea,
Taifa halingakuwa, bilashi bila ushuru. **(Joseph Kiponda)**

**<u>Maswali:</u>**

**a)** Chambua maudhui katika shairi hili. **(alama 4)**
**b)** Eleza muundo wa shairi hili. **(alama 4)**
**c)** Bainisha aina **tatu** za urudiaji katika shairi hili. **(alama 3)**
**d)** Bainisha bahari zinazojitokeza katika shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo**:(alama 2)**
i. Mpangilio wa vina
ii. Idadi ya vipande katika kila mshororo
**e)** Fafanua aina **tatu** za uhuru wa kishairi katika shairi hili. **(alama 3)**
**f)** Andika ubeti wa **sita** kwa lugha nathari. **(alama 4)**

## SEHEMU YA E: HADITHI FUPI

**Clara Momanyi:** *Mapambazuko ya Machweo*

**8.** Utumwa mamboleo ndio huu. ***Ubedui uliogubikwa ndani ya ukawaida wa maisha*** ya kisasa ndio huu.

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**
b) Huku ukitoa mifano kutoka hadithi zifuatazo, thibitisha kuwa: **'Ubedui umegubikwa ndani ya ukawaida wa maisha.'**
(i) Mapambazuko ya Machweo **(alama 5)**
(ii) Msiba wa Kujitakia **(alama 5)**

**W. N. Ogenche:** ***Sabina***

(c) "*Samahani mwalimu, nina majukumu mengi ya kutekeleza nyumbani kabla ya kuja shuleni kila asubuhi*." Eleza jinsi msemaji alivyotumika kuwakuza wahusika wengine hadithini. (alama 6)

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 2

**102/1**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 1 (INSHA)**

**MUDA: SAA 1¾**

**NAME…………………………………………………………………………………**

**SCHOOL………………………………………………… SIGN…………………………**

**INDEX NO……………………………………………… ADM NO……………………**

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

- ***a)*** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
- ***b)*** *Andika insha **mbili**. Insha ya **kwanza** ni ya **lazima.***
- ***c)*** *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya tatu zilizobakia.*
- ***d)*** *Kila insha isipungue maneno **400***
- ***e)*** *Kila insha ina alama **20***

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
| --- | --- | --- |
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 40 | |

1. **LAZIMA**

   Wewe ni mhariri wa gazeti la Mzalendo. Andika tahariri kuhusu athari za mitandao ya kijamii kwa wanafunzi wa shule nchini Kenya.

2. Unywaji wa pombe haramu una madhara mengi.
   Fafanua.

3. Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo:

   Nazi mbovu harabu ya nzima.

4. Tunga kisa kinachoanza kwa kauli ifuatayo:
   Nilipigwa na butwaa nilipomwona, sikujua nifurahi au nihuzunike….

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 2

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2 (LUGHA)**

**MUDA: SAA 2½**

**NAME**…………………………………………………………………………………

**SCHOOL**………………………………………………… **SIGN**…………………………

**INDEX NO**……………………………………………… **ADM NO**……………………

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**Maagizo**

***(a)Andika*** *jina na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

***(b)****Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani*

***(c)*** *Jibu maswali yote.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 4 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| | | |

1. **SEHEMU A: UFAHAMU (Alama. 15)**
   ***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.</u>***

"Asubuhi moja alinipata ndani ya afisi ya mwalimu mkuu wa Shule ya Msingi ya Kilimo. Mwalimu Mkuu, Bi. Tamasha, alisikiliza kadhia yangu kwa makini. Hakuonyesha kushtuka kwa yaliyonipata katika umri wangu mdogo hivi.

'Unaweza kuanza masomo katika darasa la pili. Nitamwomba mzazi mmoja akupe hifadhi,' alisema Bi. Tamasha. Huo ndio uliokuwa mwanzo wa maisha yangu katika makao ya wafanyakazi wa mashamba ya chai. Bwana Tenge na mkewe, Kimai, walinichukua kunilea pamoja na watoto wao watano. Wenzangu, nyinyi hamjui adha zinazowapata wafanyakazi wa kima kidogo. Mtajuaje na hamjawahi kukilalia kitanda hiki mkafahamiana na kunguni wake? Ninayowaambia ni asilimia ndogo mno ya niliyoyaona. Chumba cha wafadhili wangu kilikuwa hicho hicho kimoja; ndicho cha malazi, ndicho cha mapokezi, ndicho jikoni. Sebule na chumba cha malazi viligawanywa na shuka moja nyepesi. Usiku sisi watoto tulilala juu ya vigodoro ambavyo ni kama viliwekwa mvunguni mwa kitanda cha wazazi.

"Usiniulize niliyaona na kuyasikia mangapi katika chumba hiki ambacho kiligeuka *danguro* wakati Bi. Kimai alipokuwa ameenda mashambani. Wakati huu Bwana Tenge angeamua kumleta mwanamke mmoja baada ya mwingine, hapo hapo, mbele ya macho ya wanawe, hadi usiku wa kuamkia siku ya kurudi kwa Bi. Kimai. Mara mojamoja Bi. Kimai angerudi bila kutarajiwa na kumshika ugoni mke mwenzake! Mwaka mmoja, miwili, mitatu …. hata nikaona kwamba, mbali na dhiki za *kisaikolojia* nilizozipata kwa kushuhudia vituko vya kila aina, nilikuwa mzigo mkubwa kwa wahisani wangu. Si kwamba waja hawa walinibagua, la! Kusema hivyo kutakuwa kuwapaka mashizi bure. Hata hivyo nilihisi kwamba nimepata mbavu za kufanya angaa kibarua kidogo, na kuwatua wawili hawa mzigo wa kuninunulia sare na madaftari.

"Nilianza kuchuna majanichai kwa malipo kidogo nikiwa katika darasa la tano. Wakati mwingine ningerauka alfajiri na mapema kufanya kazi kabla ya kwenda shuleni saa kumi na mbili asubuhi. Jioni nilipitia huko huko. Nyakati nyingi nililala humo humo katikati ya michai, wakati mwingine kwa marafiki wanfu, kwa Bwana Tenge, na juu ya uchaga mkubwa wa saruji uliotumiwa kama karo na wauza chakula sokoni. Hakuna mmoja kati ya walimu wangu aliyejua mabadiliko haya hadi pale nilipoufanya mtihani wangu wa darasa la nane na kufuzu vyema.

"Wakati huo Bwana Tenge alikuwa ameisha kupewa uhamisho, akaenda kufanya kazi katika shamba lingine. Ndivyo wafanywavyo wafanyakazi hawa; kuhamishwa kila uchao bila mtu kuwazia kwamba wana watoto wanaoenda shule, na kwamba kuhamahama huku kunawavurugia masomo wana hawa."

## <u>MASWALI</u>

***(i)*** Eleza namna wazazi wanavyoweza kuchangia katika kuzorotesha maadili ya watoto katika jamii. **(alama 2)**

***(ii)*** Onyesha namna haki za watoto zilivyokiukwa katika kifungu. **(alama 3)**

***(iii)*** Wafanyakazi wa kima kidogo hupitia dhiki zipi kulingana na kifungu? **(alama 3)**

***(iv)*** Eleza sifa **tatu** za mkewe Tenge – Kimai. **(alama 3)**

***(v)*** Eleza namna ndoa inavyosawiriwa katika kifungu. **(alama 2)**

***(vi)*** Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika kifungu. **(alama 2)**

**(a)** Danguro

**(b)** Kisaikolojia

**2. SEHEMU B: UFUPISHO (Alama 15)** ***<u>Soma kifungu kisha ujibu maswali.</u>***

Ripoti za kila mara kuhusu uharibifu wa pesa za umma katika serikali za kaunti ni za kusikitisha. Kuna mabilioni ya pesa za mlipa ushuru ambazo hufujwa katika serikali kuu, na hivyo basi wananchi wanakosewa sana wanapoona mtindo huu ukiendelea pia katika serikali za kaunti. Wakati katiba ilipopitishwa mwaka wa 2010, Wakenya wengi walikuwa na matumaini mno kwamba ugatuzi ungewatatulia matatizo ambayo walikuwa wakipitia katika tawala zilizotangulia, hasa katika maeneo yaliyotengwa kimaendeleo.

Miaka tisa baadaye, kuna mafanikio ambayo yamepatikana ila hatua kubwa zaidi inaweza kupigwa katika kuboresha maisha ya aina raia kama mianya inayotumiwa kufuja pesa za umma itazibwa. Wizi huu unaojumuisha pia jinsi magavana wanavyobuni nafasi za kazi zisizo na maana ambazo wakati mwingi hupeanwa kwa jamaa na marafiki wao, ni sharti ukomeshwe mara moja.

Kuna wananchi wengi ambao tayari wameanza kufa moyo kuhusu umuhimu wa ugatuzi ilhali ukweli ni kwamba hatungependa kurejelea utawala ulio chini ya serikali kuu pekee. Changamoto za ugatuzi zinazosababishwa na ulafi wa viongozi wachache zinatoa nafasi kwa wakosoaji wa mfumo huu wa uongozi kushawishi wananchi na hata wahisani wasishughulike kuchangia katika maendeleo ya kaunti zao.

Juhudi zozote zile za maendeleo haziwezi kufanikishwa bila ushirikiano kutoka kwa wananchi na wahisani na hivyo basi ni jukumu la viongozi kuonyesha nia ya kutumia mamlaka walizopewa kwa manufaa ya raia. Tume ya maadili ya kupamban ana ufisadi

(EACC) kufikia sasa imeonekana kufanya kazi nzuri kwa kuwasaka na kuwashtaki magavana walio mamlakani na wengine walioondoka, kwa kushukiwa kufuja mali za umma. Tungependa asasi zote zinazohusika na masuala ya kupambana na uhalifu, pamoja na wadau wengine katika jamii wenye nia njema kwa wananchi wasifumbie macho maovu yanayotendwa katika kaunti zetu.

Nchi hii inatawalwa kwa misingi ya kisheria na hivyo basi hakuna sababu kumhurumia kiongozi yeyote anayekiuka sheria anapokuwa mamlakani kwa msingi wa mamlaka aliyoshikilia. Ni kupitia adhabu kali za kisheria pekeee ambapo tutafanikiwa kukomesha uongozi mbaya kwani kama wananchi watakuwa wakisubiri kuwaadhibu wahusika kwa kuwaondoa mamlakani pekee, watakuwa wametoa nafasi ya ufujaji kwa viongozi wapya kila miaka mitano. ***(Kutoka gazeti la Taifa Leo)***

**(a)** Fupisha ujumbe wa aya **tatu** za kwanza kwa maneno 80. *(alama 8, 1 ya mtiririko)*

**(b)** Fupisha aya **mbili** za mwisho kwa maneno 70. *(alama 7, 1 ya mtiririko)*

3. **SEHEMU C: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA** (Alama 40)

(a) Andika sifa **mbili mbili** za sauti zifuatazo. i) /e/ ii) /ch/ **ala. 2)**

(b) Unda maneno yenye muundo ufuatao wa sauti. **ala. 2)**

) KIKIKI ii) IKKI

c) Onyesha shadda inapowekwa katika maneno yafuatayo: **ala. 1)**

) mwanafunzi

ii) Alhamisi

d) Tunga sentensi **moja moja** kuonyesha matumizi ya viakifishi vifuatavyo: **ala. 2)**

i) Vifungo

ii) Kibainishi

(e) Maneno yafuatayo yako katika ngeli gani? **ala. 2)**

i) Changu

ii) Manowari

(f) Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa. **ala. 2)**

*Ndege hao wana manyoya mengi*

(g) Ainisha viambishi katika neno lifuatalo: **ala. 3)**

*Mliyempikia*

(h) Tumia kielezi cha kiasi badala ya kile kilichopigiwa mstari. **ala. 1)**

*Msichana yule alizungumza <u>kitausi</u>.*

(i) Bainisha vishazi katika sentensi ifuatayo. **ala. 2)**

*Ingawa alitia bidii masomoni, alifeli mtihani.*

(j) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya jedwali/vijisanduku. **ala. 3)**

*Mvua kubwa inayonyesha itasababisha mafuriko.*

(k) Andika upya sentensi ifuatayo ukianzia na yambwa tendewa. **ala. 2)**

*Kirwa alimjengea mama huyo nyumba kwa matofali.*

**ala. 2)**

**(l) Kanusha sentensi ifuatayo kwa wakati ujao hali ya kuendelea.**

*Walimu wanafunza.*

(m) Geuza sentensi ifuatayo katika usemi halisi. **(ala. 2)**

*Muliwa alimwambia Farida kuwa angewatembelea wazazi wao siku hiyo jioni.*

(n) Tunga sentensi **moja** kubainisha maana **mbili** za neno 'hema' **(ala. 2)**

(o) Amrisha katika nafsi ya <u>tatu wingi</u>**.** **(ala. 1)**

*Lala*

(p) Andika sentensi ifuatayo upya ukitumia vinyume vya maneno

yaliyopigiwa mstari. **(ala. 2)**

*Mama <u>alijitwika</u> kikapu mgongoni baada ya <u>kuinjika</u> chungu mekoni.*

q) Bainisha aina za virai vilivyopigiwa mstari. **ala. 2)**

*Mhadhara <u>huo tata</u> ulitolewa <u>jana jioni</u>.*

r) Tunga sentensi **moja** itakayodhihirisha matumizi matatu ya 'na' **ala. 3)**

s) Tunga sentensi ukitumia vitenzi vifuatavyo katika kauli ulizopewa mabanoni. **ala. 2)**

i) Paka (*tendata*) ii) Choma (*tendua*)

t) Andika sentensi zifuatazo kwa lugha ya tafsida. *i) Mama huyo alizaa mtoto msichana.* **ala. 2)**

*ii) Mtoto ameenda kukojoa.*

4. **SEHEMU D: ISIMUJAMII** (Alama 10)

***Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.***

Kibiko: Hujambo dada Cheupe?

Cheupe: (*Akikohoa*) Sijambo ndugu Kibiko.

Kibiko: Unaendelea namna gani?

Cheupe: *Niko poa* isipokuwa maumivu kidogo ya *chest*.

Kibiko: Usijali nitakupa *pain relievers* utakuwa sawa.

Cheupe: Asante sana, nashukuru.

**<u>Maswali</u>**

a) Eleza muktadha wa mazungumzo haya. **ala. 2)**

b) Taja na ueleze sifa za lugha inayotumika katika mazungumzo haya. **ala. 8)**

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 2

**102/3**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 3 (fasihi)**

**MUDA: SAA 2½**

**NAME……………………………………………………………………………………**

**SCHOOL…………………………………………………… SIGN…………………………**

**INDEX NO………………………………………………… ADM NO……………………**

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

***a)*** *Andika jina lako, nambari ya usajili, mkondo, sahihi na tarehe katika nafasi ulizoachiwa.*
***b)*** *Jibu maswali* **manne** *pekee.*
***c)*** *Swali la kwanza ni la* ***lazima****.*
***d)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Fasihi Simulizi.*
***e)*** *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
**f)** ***Maswali yote ni sharti yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.***

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

**SEHEMU YA A – SHAIRI**

**1.Swali la lazima**

**Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali**

Kila niamkapo husikia tama
Nami kila wakati
Na kuwazia hali inayonizunguka
Kwa vile
Imekuwa kawaida

Huyawazia kwa kipindi
Ndiyo
Huyawazia madhila na zaidi
Huyawazia madhila
Huziwazia shida
Hujiwazia dhiki

Dhiki ya ulezi
Dhiki ya kudhalilishwa kazini kwangu
Madhila ya kufanyiwa dharau na kukebehiwa
Kwa sababu ya jinsia ya kike
Kwa vile mimi ni jinsiia tofauti
Hukaa na kujiuliza
Hujidadisi kujua ni kwa nini
Jamii haikisikii kilio changu
Kilio na simanzi za kila siku
Wezangu hawanishiki mikono
Bali wananidharau kwa kuikosea utamaduni

Na sasa
Hukaa na kujiuliza
Iwapi raha yangu ulimwengu huu?
Iwapi jamaa nzima ya wa'wake?
Iwapi !Iwapi !Iwapi !

Maswali

**a)** Bila kutaja mistari mishata taja na ueleze sifa tatu zingine za shairi huru zinazojitokeza katika shairi **hili** **(alama 3)**

**b)** Eleza dhamira ya mshairi **(alama 1)**

**c)** Kwa kutoa mifano miwili, eleza maana ya mistari mishata **(alama 3)**

**d)** Eleza umuhimu wa mbinu zifuatazo katika **shairi** **(alama 4)**
i) Swali balagha
ii) Nahau
**e)** Eleza nafsineni katika shairi hili **(alama 1)**
**f)** Tambua toni ya shairi hili **(alama 1)**
**g)** Taja maudhui matatu katika shairi hili **(alama 3)**
**h)** Fafanua idhini ya mshairi jinsi inavyojitokeza **(alama 2)**
**i)** Eleza dhima ya aina mbili za urudiaji katika shairi (alama 2)

**SEHEMU YA B – TAMTHILIA YA BEMBEA YA MAISHA – Timonthy Arege**

***JIBU SWALI 2 AU 3***

**2.** 'Maradhi!......... Dawa zikiingilia huku, maradhi hutokezea pale hali pesa zinakwenda, shughuli sinasimama. Mifuko hufukarika lakini zaidi huleta wasiwasi usioisha. Ningekuwa na uwezo ningefanya chochote madhali ugonjwa uondoke. Dunia ina mitihani tosha lakini panapo maradhi sugu, uzito wake hauamithiliki. Inabaki kumwomba Mola afanye wepesi huku ukijipigapiga kutafuta jawabu.'

a) Changanua mtindo katika nukuu **(alama 6)**
b) Eleza umuhimu wa mandhari katika nukuu. **(alama 4)**
c) Taasubi za kiume katika jamii ya Bembea ya Maisha zina changamoto si haba. Fafanua. **(alama10)**

**AU**

**3.** Hata akifanya sana haitasaidia.Watu watapata sababu ya kumcheka.
(a) (i)Weka dondoo hili katika muktadha wake. **(alama 4)**
(ii) Eleza sifa sita za anayezungumziwa kwa kurejelea tamthilia ya Bembea ya maisha. **(alama 6)**
(b) Suala la ndoa lina changamoto katika jamii ya Bembea.Thibitisha**.** **(alama 10):**

**SEHEMU C: HADITHI FUPI – Mapambazuko ya Machweo na Hadithi nyingine**

***Nipe nafasi-MzamaneNhlapo***

**4.** "Matusi yaliyoje! Mwanamke anamwambia mumewe kuwa ni mzembe!"
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama 4)**
(i) Fafanua dhima ya vipengele viwili vya kimtindo vilivyotumika katika dondoo hili. **(alama 4)**
(ii) Fafanua toni iliyotumika katika dondoo. **(alama 2)**

**(b)** Kutamani ni huhitaji ambao umetawaliwa na tamaa katika hadithi ya **'Nilitamani.'** kulingana na '**Phibbian Muthama'** Pambanua haya kulingana na hadithi husika. **(alama 10)**

**AU**

**5.** a) Mabadaliko ni hali ya maisha. Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hadithi ya ***Sabina***. **(alama 10)**
b) Fafanua changamoto za watoto mayatima kulingana na hadhithi ya ***Toba ya Kalia.*****(ala10)**

**SEHEMU D: RIWAYA YA - Nguu za Jadi-Clara Momanyi**

**Jibu swali la 6 au 7**

**6.** a) Baada ya Lonare kushinda uchaguzi na kuwa Mtemi wa Matuo alinuia kuzingatia hatua kadhaa ili kujenga upya nchi ya Matuo. **Eleza** **(alama 10)**

b) "Ujinga wa kutotambua kwamba kile walichoiba ndicho kitakachowatia kitanzi."
Onyesha ufaafu wa usemi huu kwa kurejelea Riwaya nzima. **(alama 10)**

**AU**

**7. (a)**"Lazima amejiunga na kundi la marafiki wenye pesa wanaojaribu kumpotosha."

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

(ii) Fafanua umuhimu wa msemaji wa maneno haya. **(alama 6)**

(b)Matatizo yanayowakumba wanamatuo ni mwiba wa kujidunga. Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea Nguu za Jadi. **(alama 10)**

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**

**8.** Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali

*Ukiwa ni wewe mwanangu*
*Niliyekulea , ukilia usiku kuchaBaada y*
*Ukanikonjelea na kamasi kuimenga puani mwako*
*Kwa mdomo wangu angalau niokoe maisha yako nikuone*
*Chanjo nikakupeleka, ukambi , polio zote ukapewa*
*Maziwa nikakupea yote nikuokoe uzimezwe na gonjwa la kwashiako*
*Kisomo ni kauza ndengu na mbaazi zangu ni kalala njaa mkanda huku nimejifunga*
*Sasa wa unanitusi upendavyo na kunitivulia kivumbi na gari lako*
*Wewe muasi eti umeoa mzungu na mimi waniona mama kizee , mchafu*
*Mizimu waone uchungu na kilio changu, nalala njaa na mararu ndio vasi*
*Laana wakumimine mpaka kizazi chako cha kumi na mbili*
*Usiwahi furahia pato lako hata chembe*
*Hicho unanitendea mie kikuandame katika nyayo zako hadi mauko yako*

**a)** a)Weka kifungu hiki katika Utanzu kisha kipera chake**.** **(alama 2)**

**b)** Toa sifa tano za kipera hiki**.** **(alama 5)**

**c)** Ni mbinu zipi za kiuchumi zinazoendelezwa na jamii husika. **(alama 2)**

**d)** Tambua na uthibitishwe nafsi neni na nenewa utunguni. **(alama 2)**

**e)** Umeamua kutafiti kipera hiki kwa mbinu ya video, eleza manufaa ya mbinu hii **(alama 5)**

**f)** Kipera hiki kinaendelea kufifia katika jamii yako, eleza mbinu za kisasa ambazo jamii yako inaweza kutumia kuhifadhi kipera hiki**.** **(alama 4)**

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 3

**102/1**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 1 (INSHA)**

**MUDA: SAA 1¾**

**NAME**…………………………………………………………………………………

**SCHOOL**……………………………………………… **SIGN**…………………………

**INDEX NO**…………………………………………… **ADM NO**……………………

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

***a)*** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

***b)*** *Andika insha **mbili**. Insha ya **kwanza** ni ya **lazima.***

***c)*** *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya tatu zilizobakia.*

***d)*** *Kila insha isipungue maneno **400***

***e)*** *Kila insha ina alama **20***

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 40 | |

## MASWALI

1. Wewe ni mwanahabari katika shirika la Tangaza. Andika mahojiano kati yako na waziri wa Kilimo nchini kuhusu athari za baa la njaa na hatua zinazochukuliwa na serikali katika kukabili tatizo hili. **(alama 20)**

2. Ufisadi umekita mizizi nchini Kenya. Jadili madhara yake huku ukipendekeza suluhu. **(alama 20)**

3. Andika insha itakayothibitisha ukweli wa methali : **Mchelea mwana kulia, hulia yeye.** **(alama 20)**

4. Andika insha itakayomalizia kwa :
   **....** walipofungua mlango huo hatimaye wengi hawakuweza kuzuia hisia zao.
Waliangua vilio kwa maafa waliyoyashuhudia. **(alama 20)**

*Published by Mwalimu Consultancy Limited. Tel; 0746 222 000*

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 3

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2 (LUGHA)**

**MUDA: SAA 2½**

**NAME……………………………………………………………………………….**

**SCHOOL……………………………………………….    SIGN………………………….**

**INDEX NO……………………………………………..    ADM NO…………………….**

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**Maagizo**

*(a)**Andika** jina na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

***(b)**Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani*

***(c)** Jibu maswali yote.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 4 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| | | |

*Ukihitaji majibu, Pigia - 0746 222 000 / 0742 999 000*

**1. UFAHAMU**

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali*.**

Ufisadi ni uhalifu unaohusu kuzitumia njia za ulaghai kujipatia pesa, mali au vitu hasa vya umma.

Nchini Kenya ufisadi hujitokeza kwa njia mbalimbali na kila mojawapo ina athari zake. Kwa mfano, kuna maafisa wa serikali wajipatiao pesa kwa kuuza stakabadhi za serikali kama vile pasi, vyeti vya kuzaliwa, vyeti vya kumiliki mashamba, vitambulisho na nyinginezo kwa raia, kuna hatari kubwa kwa sababu watu wasio raia wa Kenya wameweza kusajiliwa kama wakenya na kuendeleza uhalifu kamaugaidi, wizi na ulanguzi wa dawa za kulevya.

Wengine hujipatia vibali vya kufanya kazi na kuajiriwa kazi ambazo zingefanywa na wakenya.Hii imechangia ongezeko la uhaba wa kazi nchini. Watumizi wengine wa umma huuza mali ya serikali kama vile magari, nyumba na ardhi na kufutika pesa za mauzo mifukoni mwao. Wengine wao hujinyakulia na kufanya vitu hivyo kuwa mali yao. Ufisadi wa aina hii umegharimu serikali kiasi kikubwa cha fedha. Serikali imelazimika kununulia maafisa wake magari baada ya muda mfupi, kulipia wafanyikazi wake kodi za nyumba na kukosa viwanja vya upanuzi na ujenzi wa shule hospitali, vituo vya polisi na taasisi zingine maalumu. Baadhi ya wataalamu kama madaktari huiba dawa kutoka hospitali za umma kupeleka vituo vyao vya afya. Pia hutumia wakati wao mwingi katika kazi zao za kibinafsi na kuwaacha wagonjwa katika hospitali za umma wakihangaika. Sio madaktari tu, kuna masoroveya, wahandisi, mawakili, walimu na mahasibu ambao hukwepa **majukumu** yao serikalini na kufanya kazi za kibinafsi. Wengine wasio wataalamu huendesha biashara za aina tofauti, na huku wanaendelea kupokea mishahara.

Wanafunzi wanaotaka kujiunga na vyuo na shule bora za umma na hawakuhitimu wakati mwingine hulazimika kusalimu amri na kutoa hongo hili wapate nafasi za kusoma. Kiasi cha pesa kinachohitajika huwa kikubwa hivi kwamba ni wachache humudu hizo rushwa. Wale **wasiojimudu** kifedha hubaki **wakilia ngoa**. Kuna wazazi ambao hutumia vyeo vyao na 'undugu' kupata nafasi zilizotajwa, jambo ambalo huwanyima wanafunzi werevu kutoka jamii maskini nafasi ya kupata elimu. Matokeo huwa ni kuelimisha watu wasiostahili na ambao mwishowe hawaziwezi kazi wanazosomea wakihitimu na kuanza kuhudumia jamii. Ufisadi **umekita** mizizi na **kushamiri** katika sekta za umma za kibinafsi kwa upande wa kuajiri wafanyakazi. Ni vigumu kupata kazi ikiwa hujui mtu mkubwa katika shirika linalohusika au uzunguke mbuyu. Matokeo ni kuajiri wafanyakazi wasiohitimu na wasiowajibika kazini.

Vyeo na madaraka katika baadhi ya mashirika hutolewa kwa njia ya mapendeleo na ufisadi. Kwa hivyo, wafanyakazi wenye bidii hufa moyo kwa sababu hawasaidiwi ipasavyo. Badala yake wale wasioleta bidii hupandishwa vyeo na kuwaacha palepale.

Hata hivyo, mbio za sakafuni huishia ukingoni. Serikali imetangaza vita dhidi ya ufisadi. Tayari tume kadhaa zimebuniwa kuchunguza visa vya ufisadi uliotekelezwa hapo mbeleni. Mojawapo ya tume hizo ni Tume ya kuchunguza **Kashfa** ya "Goldenberg" ambapo pesa za umma (mabilioni) ziliporwa na mashirika na watu binafsi kwa njia siziso halali. Watakaopatikana na hatia ya kushiriki ufisadi huo watahitajika kurudisha pesa hizo.

Serikali pia imeunda kamati ya kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi **waliohasiriwa** na mawakili walaghai ambao hupokea ridhaa kwa niaba ya wateja wao na kukosa kuwalipa au kuwatetea mahakamani ilhali wamekwishalipwa. Ni matumaini yetu kuwa ulaghai huu utaangamizwa kabisa kwani hakuna refu lisilokuwa na ncha.

**Maswali**

**a)** Eleza aina nne za ufisadi zilizotajwa katika kifungu ulichosoma**.** **(alama 4)**

**b)** Kulingana na kifungu ulichosoma,ufisadi umeathiri nchi yetu kwa njia gani ? **(alama 2)**

**c)** Serikali inafanya jitihada gani ili kukomesha ufisadi ? **(alama 3)**

**d)** Kwa maoni yako, unafikiri ufisadi husababishwa na nini ? **(alama 2)**

**e)** Toa msamiati mwingine wenye maana sawa na rushwa. **(alama 1)**

**f)** Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa kifunguni: **(alama 3)**

**i)** shamiri

**ii)** waliohasiriwa

**iii)** wakilia ngoa

**2. MUHTASARI (ALAMA 15)**

***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali uliyopewa.***

Taifa la Kenya limekuwa na tatizo la njaa kwa muda mrefu na hili ni tatizo ambalo hutokea mwaka baada ya mwaka. Kuna sababu kadhaa ambazo zimelifanya tatizo hili likithiri. Wananchi wengi hutegema ukulima kujipatia pato pamoja na chakula. Jambo hili limekuwa shida kubwa kwa vile kilimo hutegemea mvua isiyotabirika. Watabiri wa hali ya hewa huwashauri wakulima wapande mbegu zitakazohimili jua lakini mvua nayo inakuwa nyingi na kuharibu mimea.

Bidhaa za ukulima kama mbegu za kupanda, mbolea, dawa za kunyunyizia n.k, zimekuwa ghali. Kuna sehemu kubwa ya ardhi ambayo ni kame na haiwezi kutumika kwa kilimo. Mazao yanayotolewa shambani hayahifadhiwi vizuri. Mengine yanaharibikia shambani na mengine yanavamiwa na wadudu kiasi kwamba hayawezi kutumika.

Tatizo lingine ni vita vya kikabila. Kabila tofauti zinapopigana, watu huhama na kuacha mashamba ilhali wengine huchoma maghala ya chakula. Wafanyabiashara pamoja na serikali huwanunulia wakulima mazao yao kwa bei ya chini sana mpaka wanakosa shauku ya kuyashughulikia mashamba,yao. Siku hizi wakulima hawashughuliki tena kuzuia mmomonyoko wa udongo. Hivvo mvua inaponyesha rotuba yote inachukuliwa. Serikali haina sera mwafaka za kukabiliana na njaa. Hii ndiyo sababu sehemu zingine kama Turkana zimekabiliwa na njaa kwa muda mrefu.

Tatizo hili linaweza kutatuliwa ikiwa wakulima wataelimishwa juu ya mbinu bora za ukulima. Pia wakulima waishio katika sehemu ambazo hazina mvua ya kutosha wapewe mbegu ambazo zitahimili kiangazi. Ukulima wa kunyunyuzia mimea maji unafaa kuzingatiwa.Mazao yanayotolewa shambani yahifadhiwe vizuri kwa kuwekwa dawa za kuwaua wadudu.

Sehemu kubwa za ardhi ambazo hazitumiwi zitolewe kwa kilimo. Ni muhimu wakulima waelimishwe kuhusu jinsi ya kuzuia mmomonyoko wa udongo na umuhimu wake. Wakulima wanunuliwe mazao yao kwa bei nafuu ili wajibidiishe katika kazi yao. Serikali inafaa iwe na sera mwafaka ili iweze kutatua tatizo hilo ambalo limekuwa ni janga kuu.

**a)** Fupisha aya tatu za mwanzo (maneno 70) **(alama 8)**

**b)** Fupisha aya mbili za mwisho. (Maneno 60 **(alama 7)**

**3. MATUMIZI YA LUGHA** **(Alama 40)**

**a)** Eleza tofauti kati ya sauti **(alama 2)**

**i)** | d |

**ii)** | t |

**b)** Andika maneno yenye miundo ifuatayo: **(alama 2)**
i) KKKl
ii) ll

**c)** Andika katika umoja. **(alama 2)**
Machaka haya hayazai maua meusi

**d)** Andika kinyume cha sentensi ifuatayo: **(alama 2)**
Dada aliinama na akasimama ndani ya nyumba.

**e)** Tambua aina ya vishazi katika sentensi hii: **(alama 2)**

**f)** Ijapokuwa ni mgonjwa tutamwandalia karamu leo.

**g)** Bainisha matumizi ya 'ki' katika sentensi ifuatayo. **(alama 2)**

**h)** <u>Ki</u>toto hiki kilinichezea <u>ki</u>jinga.

**i)** Tumia neno 'mle' kwenye sentensi kama : **(alama 3)**
i) kivumishi ii) kiwakilishi iii) kielezi

**j)** Andika katika ukubwa. **(alama 2)**
Kiti kilichokuwa kimebebwa na mvulana kilivunjika.

**k)** Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo: **(alama 3)**

**l)** Atieno alijengewa nyumba na mamake kwa matofali.

**m)** Changanua sentensi hii kwa kutumia mtindo wa jedwali. **(alama 4)**
Wanafunzi wageni waliofika shuleni mapema walibeba vitabu vingi ajabu.

**n)** Eleza maana ya dhana ya <u>chagizo</u> kisha uonyeshe kwa kupigia mstari chagizo katika sentensi ifuatayo. **alama 2)**
Mkuliwa hodari zaidi atatuzwa kwa bidii yake.

**o)** Kwa kutoa mifano katika sentensi, onyesha matumizi mawili ya kistari kifupi.**(alama 2)**

**p)** Andika katika usemi halisi. **(alama 3)**
Mwalimu aliwasisitizia wanafunzi kuwa kulikuwa na umuhimu kuwatii wazazi wao kwani hilo lingeongeza siku zao duniani.

**q)** Tunga sentensi sahihi ukitumia hali ya 'a' isiyodhihirika. **(alama 2)**

**r)** Ainisha vitenzi katika sentensi ifuatayo: Wazazi walikuwa wangali harusini. **(alama 2)**

**s)** Tumia o-rejeshi badala ya amba-
Wachezaji ambao hucheza kwa bidii ndio ambao hufaulu maishani. **(alama 2)**

**t)** Nyambua kitenzi 'ja' katika kauli ya kutendewa. **(alama 1)**

**u)** Nimenunua dawa ili iwamalize wadudu wanaotusumbua hapa kwetu nyumbani. **(alama 2)** Aanza: Wadudu ............

**4. <u>ISIMUJAMII</u>**

"Anachukua mpira, kisigino anatuliza, kengeuka, kulia, kushoto, hesabu wa kwanza tesa wa pili,baki peke yake na goalkeeper.

**a)** Taja sajili inayorejelewa na maneno haya. **(alama 2)**

**b)** Fafanua sifa za sajili hii. **(alama 8)**

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 3

**102/3**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 3 (fasihi)**

**MUDA: SAA 2½**

**NAME……………………………………………………………………………………**

**SCHOOL……………………………………………… SIGN…………………………**

**INDEX NO…………………………………………… ADM NO……………………**

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

- ***a)*** *Andika jina lako, nambari ya usajili, mkondo, sahihi na tarehe katika nafasi ulizoachiwa.*
- ***b)*** *Jibu maswali **manne** pekee.*
- ***c)*** *Swali la kwanza ni la **lazima**.*
- ***d)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Fasihi Simulizi.*
- ***e)*** *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
- **f)** ***Maswali yote ni sharti yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.***

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

**SEHEMU A:**

**FASIHI SIMULIZI**

**1. LAZIMA**

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali**

Lala mtoto lala*2
Mama atakuja lala
Alienda sokoni lala
Aje na ndizi lala
Na maziwa ya mtoto lala
Kukupa kwangu wewe kinofu
Kipenzi mwana lala*2

Lala mtoto lala*2
Basi kipenzi lala
Baba atakuja lala
Aje na mkate lala
Mkate wa mtoto lala
Tanona ja ndovu lala

**Maswali**

**a)** Huku ukithibitisha jibu lako eleza huu ni wimbo wa aina gani? **(alama 2)**

**b)** Eleza sifa za wimbo wa aina hii. **(alama 5)**

**c)** Onyesha umuhimu wa wimbo huu. **(alama 4)**

**d)** Eleza ni shughuli gani za kiuchumi ambazo jamii hii inajihusisha nayo katika wimbo huu. **(alama2)**

**e)** Tambua mbinu zozote mbili za lugha zilizotumika katika wimbo huu. **(alama 2)**

**f)** Fafanua changamoto **tano** ambazo mtafiti anaweza kumbana nazo akiwa nyanjani. **(alama 5)**

**SEHEMU YA B: RIWAYA- NGUU ZA JADI**

**Jibu swali la 2 au 3**

**2. Hivyo**, alitaka kubadili hali hata kama ilimaanisha kukitia kichwa chake kinywani mwa simba. Alitaka kuliokoa jahazi lililokuwa likielekea mwambani kwa kasi. Lakini angeliweza vipi kupambana na utandu wa mahasidi hao?.

**(a)** Eleza mbinu nne za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili **(alama 4)**

**(b)** Eleza sababu za msemaji kutaka kufaulisha kauli iloyopigiwa mstari **(alama 10)**

**(c)** Eleza umuhimu wa mrejelewa katika kuijenga riwaya hii **(alama 6)**

**au**

**3.** Dunia yote inajua aliyemsaliti Yesu Kristo. Unajua mtu huyo aliishia wapi

**a)** Fafanua muktadha wa dondoo hili **(alama 4)**

**b)** Tambua mbinu mbili za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili. **(alama 4)**

**c)** Fafanua namna wahusika walivyowaendea kinyume wenzao katika riwaya ya Nguu za Jadi. **(alama 12)**

**SEHEMU C: TAMTHILIA; -BEMBEA YA MAISHA – TIMOTHY M. AREGE**

**Jibu Swali la 4 au 5.**

**4. "Huku ndiko kuvumilia hasa. Tazama faraja ilivyoalika sasa"**

a) Weka dondoo hili katika muktadha. **(alama 4)**

b) Eleza sifa za msemaji katika dondoo. **(alama 6)**

c) Onyesha jinsi faraja ilivyoalika katika maisha ya msemewa kwa kurejelea tamthilia ya: Bembea ya Maisha. **(alama 10)**

**AU**

**5.(a) Changanua mtindo katika kifungu kifuatacho. (alama 10)**

Maskini mke wangu! Kumbe ugonjwa haukumsaza mwaka baada ya mwaka. Umemla bila huruma. Awali niliona kama mchezo. Kumbe ilikuwa kweli! Kauli yake ninaona imesimama. Ni mwele hakika. Laiti ningejua, jana ningeishi tofauti. Silesi zetu za maisha tungezila zilivyokuja kwa furaha. (*Kimya*). Siku hazigandi wala jana hairudi. Sasa jana imebaki kuwa kumbukizi baada ya kusombwa na wakati mfano wa mafuriko msimu wa masika. (*Kimya*). Kwa bahati nzuri bado tupo. Ninaweza kuiachia dunia tabasamu iwe silesi kwa vizazi vijavyo na kila mwenye nia njema. (*Kimya*). Siwezi kuendelea kuishi hivi. Sasa nimekata shauri. Lazima niache njia ya zamani na kuifuata mpya. Maisha mapya. Pombe! *(kama anayeisemea pombe)*. Umenichezesha kama mwanasesere kwa muda mrefu. Umeninyima fursa ya kuielewa familia yangu. Hapana! Siku zangu za uzeeni lazima nizitumie kumwangalia mke wangu mgonjwa. Lazima nimshukuru kwa vitendo kwa jinsi alivyojitolea kuijenga familia yetu. *(anapunga mkono.)* Kwaheri pombe. Buriani.

b) Bainisha toni ya dondoo hili. **(alama 2)**

c) Fafanua umuhimu wa msemaji wa maneno haya katika kuijenga tamthilia nzima. **(alama 8)**

**SEHEMU YA D-USHAIRI**

**Jibu swali la 6 au la 7.**

6. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali:**

Binadamu hatosheki, ni kiumbe chenye zani, kweli mja hapendeki,
Kwa kweli haaminiki, hila ameficha ndani, la wazi ni unafiki
Ukweliwe haafiki, njama zake zi moyoni, usimwone ni rafiki
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Wengine watakuua, wakiona una pesa, hata zikiwa kidogo,
Hizo kwao ni maua, hupupiwa zikatesa, wakazifuata nyago,
Hadi kwenye wao ua, pasipo hata kupesa, wala kukupa kisogo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka

Pindi kinunua kitu, hafurai Shaitani, bali tajawa chukizo,
Mtu kiwa mtukutu, tanunua mtimani, kwalo lako tekelezo,
Tamko lake 'Subutu', kuondoa tumaini, na kukuulia wazo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Aliye na taraghani, taabu kuishi naye, kazi yake kujidai,
Takusema faraghani, asosema kiwa naye, kupendeza maadui,
Hana faida nyumbani, ni mtu akuchimbaye, mradi usitumai,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Kwa hakika ni balaa, kumkirimu mchawi, aliejaa uchoyo,
Bahati ina hadaa, kukupa alo sadawi, aibatili rohoyo
Mipangoyo kwake jaa, na nia ya ustawi, huwiza vunja kaniyo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka

Ninacho change killo, ninalia sanasana, kinyesi nimetupiwa,
Ningetoa azimio, lakini uwezo sina, kwa matatizo kuambiwa,
Ama nitumie mbio, fuadi ninanena, akilini nazuiwa,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

**MASWALI:**

**a)** Lipe shairi hili anwani mwafaka. **(alama 1)**

b) Fafanua mambo **matatu** ambayo nafsineni analalamikia. **(alama 3)**

c) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. **(alama 3)**
(i) Idadi ya vipande katika kila mshororo
(ii) Mpangilio wa vina katika kila ubeti
(iii) Idadi ya mishororo katika kila ubeti

d) Andika ubeti **wa nne** katika lugha nathari. **(alama 4)**

e) Bainisha tamathali mbili za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. **(alama 2)**

f) Huku ukitoa mifano, onyesha mbinu mbili alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. **(alama 2)**

g) Andika aina mbili za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. **(alama 2)**

h) Fafanua muundo wa ubeti **wa tano**. **(alama 3)**

**AU**

**7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Na ujenge nyumba yako, jingi jasho likuoshe,
Ufyeke, upime na uweke nguzo,
Kisha paa uweke na ukandike,
Siku nyingi bila kuingiliwa na mgeni hutakaa.

Wataanza kutalii mpaka mende usiku,
Nje na ndani ya nyumba watazunguka,
Bila woga, bila ruhusa ulichonacho watakula,
Masalia yatakuwa yako, ijara ya kaziyo.

Na nyingi dawa uweke, nyumba nzima uihame,
Ukae nje nzima siku usubiri,
Wazima wamelala ukirudi usiku,
Vichwa vigumu hawafi mende rahisi.

Kifo cha mende sharti miguu juu
Kichwa ukikanyage kipasuke usikie,
Na kisha wengine usiku mchana uwasake.
Mpaka watakapokwisha. Usiseme nao.

**Maswali**

(i) Hili ni shairi la aina gani? **(alama 1)**
(ii) Eleza **muundo** wa shairi hili **(alama 3)**
iii) Eleza jinsi mshairi alivyoutumia **uhuru** wake katika utunzi wa shairi hili. **(alama 4)**
iv)Taja mbinu **mbili za lugha** alizotumia mshairi na uzitolee mifano**.** **(alama 4)**
v)Andika **ubeti wa tatu** kwa lugha nathari. **(alama 4)**
vi)Eleza **ujumbe** wa mshairi. **(alama 2)**
vii)Toa mfano mmoja wa mshororo **mshata**. **(alama 1)**
viii)Kichwa gani kinaliafiki shairi hili? **(alama 1)**

**SEHEMU E:**
**HADITHI FUPI**
**Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine.**

**8. Harubu ya maisha *Paul Nganga Mutua***

"Naja. Nakamilisha shughuli ndogo hapa kisha nianze safari…"

**(a)** Weka dondoo hili katika muktadha wake **(alama 4)**
**(b)** Eleza sifa sita za msemaji wa kauli hii **(alama 6)**
**(c)** Jadili changamoto wanazokumbana nazo waajiriwa kwa kurejelea hadithi hii**.** **(alama10)**

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 4

**102/1**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 1 (INSHA)**

**MUDA: SAA 1¾**

**NAME……………………………………………………………………………………**

**SCHOOL……………………………………………… SIGN…………………………**

**INDEX NO…………………………………………… ADM NO……………………**

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

***a)*** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

***b)*** *Andika insha* ***mbili****. Insha ya* ***kwanza*** *ni ya* ***lazima.***

***c)*** *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya tatu zilizobakia.*

***d)*** *Kila insha isipungue maneno* ***400***

***e)*** *Kila insha ina alama* ***20***

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 40 | |

## MASWALI

**1.** Hivi karibuni kumekuwa na visa vya wawaniaji wa nyadhifa mbalimbali kulalamika kuhusu matokeo ya uchaguzi. Wewe ni mwanahabari katika shirika la utangazaji la Tabasamu. Andika mahojiano kati yako na mwenyekiti wa Tume Huru yauchaguzi na mipaka kuhusu vyanzo vya malalamishi haya na namna yakusuluhisha tatizo hili. **(Al. 20)**

**2.** Kutoka na na ongezeko la visa vya ukosefu wa usalama, eleza namna usalama unavyoweza kuimarishwa nchini **(Al. 20)**

**3.** Andika kisa kitakachodhihirisha ukweli wa methali 'Mkokoto wa jembe si bure yao' **(Al. 20)**

**4.** Kamilisha kwa maneno haya …wote waliokuwepo waliinama na kuvitikisa vichwa vyao, kisha wakaviinua na kukubaliana kwakauli moja kuwa vijana wanastahili kushirikishwa katika ujenzi wa taifa **(Al. 20)**

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 4

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2 (LUGHA)**

**MUDA: SAA 2½**

**NAME……………………………………………………………………………………**

**SCHOOL……………………………………………… SIGN…………………………**

**INDEX NO……………………………………………… ADM NO……………………**

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**Maagizo**

*(a)**Andika** jina na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

*(b)Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani*

*(c) Jibu maswali yote.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 4 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| | | |

## 1. UFAHAMU (ALAMA 5)

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***

Ilikuwa siku ya Jumapili moja yalipotokezea mambo hayo. Kwa kawaida, Jumapili ni siku yangu ya kupumzika. Siku ya kuachana na vitabu na shughuli nyingine za masomo baada ya kazi ngumu za juma zima. Nilihisi **nastahiki** kupumzika, anagalau siku moja kwa wiki. Nipumzike kwa kufanya nililopenda.

Kwangu mimi kupumzika kulikuwa na maaana tofauti na maaana ya kupumzika kwa watu wengine. Kupumzika kwangu mimi ni kuwasaidia wazazi wangu kuchunga ng'ombe na mbuzi ili nipate fursa ya kuweko vichakani peke yangu. Nipate kuwa karibu na maumbile. Niwe karibu nayo huku nimetulia kimya huku natazama mandhari na maumbile ya kijiji chetu. Mara nyingine hali hii ya utulivu wa maumbile hunifanya niimbe kwa sauti ya juu au kimyakimya. Pengine husinzia hapo na kuota ndoto za hamu yangu. Kuota baadaye yangu na mema ninayojitakia. Naam, haya yote ndiyo yaliyokuwa na maana ya kupumzika kwangu. Yote haya na zaidi ya haya ambayo nitayataja baadaye.

Leo lakini, kinyume na unavyodhani wewe, nilikuwa nimejaa mchanganyiko wa huzuni na furaha wakati mmoja. Kule mwituni nilikokuwa nikichunga ng'ombe, kumbe sikufuatwa **kuposwa** kama nilivyofikiri. Nilifutwa ili kumwonyesha yule mteja mifugo aliyotaka kununua. Baba na mama waliamua kuwauza wanyama wetu wote hatimaye. Baba alisema kuwa mjomba Kasimu, aliyefariki miezi sita iliyopita, ameacha kibanda huko jijini. Na yeye baba na mama wameamua kuenda kuishi huko jijini ili wanipe fursa ya kusoma na kuelimika zaidi, Sasa nadhani utaweza kufahamu maana ya mchanganyiko wangu wa huzuni na furaha. Furaha, kwa sababu ndoto yangu imeitikiwa hatimaye. Yale maombi yangu niliyoyaomba karibu na mbingu yamekubaliwa. Sasa niko tayari kwenda jijini kutimiza wajibu wangu.Kwenda kuikabili kazi ngumu. Kuitumia fursa hiy ya kusoma na kujielimisha zaidi kuliko huku kijijini. Niko tayari kusoma na kujituma kwa bidii zangu zote ili nifike **ukomo** wa masomo yote ni nayoweza kufikia.

Kwa upande mwingine lakini, nilikuwa mzito kuondoka kwa sababu nyingi. Kwanza, kwa jinsi nilivyokipenda kijiji chetu. Pili, sikuwa tayari kutengana na wale mifugo wetu ambao kwa muda mrefunimefanya urafiki nao. Leo ghafla wamenunuliwa na kuchukuliwa na mtu mwingine. Nilihitaji muda mrefu kuweza kuwasahau.Kama ningeweza kamwe. Tatu, niliona aibu, na aibu zikanitia huzuni kwa kuwafikiria vibaya wazazi wangu. Kwa nini niliweka mbele hamu yangu tu?Kwa nini nilionyesha ubinafsi wangu tu? Kwa nini nilisahau mapenzi na ahadi ya watu hawa wanaonipenda kuliko kitu chochote? Kwa nini niligeuka haini mara moja bila ya kufikiri. Kwa nini sikutaka hata kusadikisha ukweli au uongo wa ile fikira ya posa?

**(*Kutoka kwaVipawa vya Hazina, na Said A Mohamed, OUPEA.*)** **Maswali**

***a)*** Ipe taarifa hii kichwa mwafaka **(al. 1)**

***b)*** Taja msimulizi wa habari hii **(al. 1)**

***c)*** Msimulizi anasema ya kwamba kupumzika kwake na kwa watu wengine kulikuwa tofauti, dhihirisha. **(al. 2)**

***d)*** Kulingana na kifungu, utulivu anaoudai mwandishi ulikuwa na faida gani kwake **(al. 2)**

***e)*** Fafanua hasara mbili za msimulizi kuhamia mjini **(al. 4)**

***f)*** '…sasa niko tayari kwenda jijini kuitimiza wajibu wangu. Kwenda kuikabili kazi ngumu…' Msimulizi alimaanisha nini aliposema haya. **(al. 2)**

g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu **(al. 3)**

i) nastahiki ii)kuposwa

iii)ukomo

**2. UFUPISHO** **(ALAMA 15)**

***Soma makala yafuatayo kasha ujibu maswali***

Maradhi ya kipindupindu yameendelea kuripotiwa katika sehemu mbalimbali nchini. Kufikia sasa watu zaidi ya sita wameripotiwa kufariki na wengine zaidi ya mia tatu kulazwa hospitalini.

Maradhi haya yamebainika kuchangiwa na maji ama chakula chenye vidudu vya kolera. Hujitokeza kwa mtu kuharisha majimaji na pia kutapika.

Hii si mara ya kwanza kwa Kenya kushuhudia maradhi haya na yameonekana kujitokeza zaidi katika miaka ya hivi punde. Kati ya Desemba 2014 hadi Januari 2016, visa zaidi ya elfu kumi na moja vya kipindupindu viliripotiwa huku kukiwa na vifo mia moja sabini na nane kote nchini.

Kufikia Aprili 2016, visa 1,629 vilikuwa vimeripotiwa na vifo 18 kutokea Mandera. Chama cha madktari humu nchini. Kimeripotiwa kusema kuwa kunapoanza kutokea mikurupuko ya maradhi kama hayo ni ishara ya mfumo wa matibabu kuwa na kasoro.

Maradhi haya yameonekana pia kuwa changamoto kuu na watafiti kuhofia kuwa baadhi ya viini vyake hasa Nairobi ni sugu, havitibiki na dawa zilizopo na vimewahi kuchangia vifo vingi katika mikurupuko iliyotokea Haiti, Rwanda na Jamhuri ya Demokrasia ya Congo. Wahusika wakuu katika masuala ya afya ya umma walionekana kusita mwanzoni kujitokeza wazi na kuanza kukabiliana na tatizo hilopamoja na kurushiana lawama.

Hata hivyo ni muhimu kwa wanaohusikana afya ya uma pamoja na matibabu kuchukua hatua zinazostahili mapema na sio wakati wote kusubiri mukurupuko kuanza kutaka kuonekana kuwa wako kazini.

Wanapaswa kujua kama wanaopika kando ya barabara na kwenye vibanda wamechunguzwa kiafya kupikia watu.

Tunatoa wito kwa wananchi wasisubiri serikali bali na wao wachukue hatua ya kukabiliana na ugonjwa huu. Lazima wajali kuhusu maisha yao pamoja na kuwajali wengine,

Kuna watu ambao wamekuwa wakiuza mboga kwa kutumia maji ya maji taka na kuna wanaoendesha biashara za maji, ambayo huyachota kutoka sehemu zisizo salama na kisha kuyauzia wengine wasiokuwa na habari bila kujali madhara wanayoeneza kwa wengine.

Juhudi za kila mmoja zinahitajika kukabiliana na kipindupindu na watakaogundua ishara watafute tiba mara moja badala ya kujitibu kama ilivyo desturi kwa wengi hadi wanapozidiwa. *(Taifa Leo Jumatano Julai 26, 2017)*

***Maswali***

**a)** Bila kupoteza maana, fupisha aya tatu za mwanzo (maneno 60-69) (al. 7, utiririko 3)

**b)** Kulingana na aya tatu za mwisho, ni hatua zipi ambazo zinaweza kuchukuliwa kuzuia ugonjwa huu hatari wa kipindupindu (maneno 50) **(al. 5)**

**3. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA** **(ALAMA 40)**

**a i)** Andika vigezo viwili vya kuianisha konsonanti **(al. 2)**

ii) Tofautisha /sh/ na /ch/ **(al. 1)**

**b)** Tumia kiimbo katika sentensi mbili tofauti sahihi kudhihirisha uamilifu wake **(al. 2)**

**c)** Eleza maana za maneno yafuatayo kwa kuzingatia mahali ambapo shadda imewekwa **(al. 2)**
'ala a'la

**d)** Fafanua dhana ya sauti mwambatano kwa kutolea mfano sahihi **(al. 2)**

**e)** Bainisha majukumu ya viambishi katika fungutenzi hili:
nimsubiriaye **(al. 2)**

**f)** Weka nomino hizi katika ngeli mwafaka

i) debe …………………………………………………………… **(al. 1)**

ii) mtaimbo ……………………………………………………… **(al. 1)**

**g)** Yakinisha
Mgonjwa yule hasikii wala kusema lolote **(al. 2)**

**h)** Andika kwa ukubwa wingi
Panya huyo alinaswa mtegoni na nyama kubwa mdomoni **(al. 2)**

**i)** Geuza katika kauli iliyo kwenye mabano

i) Wanyama wa pori huwavutia watalii (tendwa) **(al. 1)**

ii) Viota hivyo vya ndege vilivamiwa na wadudu (tenda) **(al. 1)**

**j)** Andika katika usemi halisi **(al. 3)**
Daktari alitaka kujua kama kulikuwa na jamaa wake yeyote ambaye alikuwa ameugua ugonjwa huo

**k)** Tumia kiwakilishi cha pekee chenye kuleta dhana ya msisitizo katika sentensi sahihi **(al. 2)**

**l)** Changanua kwa njia ya jedwali
Waswahili husema chema chajiuza, kibaya chajitembeza **(al. 4)**

**m)** Andika sentensi upya kulingana na maagizo **(al. 2)**
Ongezeko la visa vya uhalifu linatishia kuangamiza amani katika miaka ya hivi karibuni.( anza Amani…)

**n)** Tunga sentensi moja kwa kutumia kirai kihusishi kisha upigie mstari **(al. 2)**

**o)** Bainisha vishazi
Tangu awasili kutoka Marekani amewasaidia mayatima wengi **(al. 2)**

**p)** Eleza matumizi mawili ya alama ya mkato **(al. 2)**

**q)** Onyesha shamirisho na chagizo katika sentensi ifuatayo **(al. 3)**
Mwanamwali alirembeshwa nyusi kwa wanja taratibu

**r)** Kamilisha methali ifuatayo **(al. 1)**
Mfamaji haachi

**4. ISIMU JAMII** **(ALAMA 10)**

**a)** Taja mambo **matatu** yanayopelekea kufifia na kufa kwa lugha **(al. 3)**

**b)** Isimujamii ina umuhimu gani kwa mwanafunzi wa shule ya upili **(al. 4)**

**c)** Andika sifa **tatu** za lugha utakayotumia kuwatangazia watu kuhusu kinyang'anyiro cha soka **(al. 3)**

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 4

**102/3**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 3 (fasihi)**

**MUDA: SAA 2½**

**NAME……………………………………………………………………………………**

**SCHOOL………………………………………………… SIGN…………………………**

**INDEX NO……………………………………………… ADM NO……………………**

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

- **a)** *Andika jina lako, nambari ya usajili, mkondo, sahihi na tarehe katika nafasi ulizoachiwa.*
- **b)** *Jibu maswali **manne** pekee.*
- **c)** *Swali la kwanza ni la **lazima**.*
- **d)** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Fasihi Simulizi.*
- **e)** *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
- **f)** ***Maswali yote ni sharti yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.***

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

**1. SWALI LA LAZIMA (AL. 20)**

Aidha, ngome inapoteketezwa na waovu wachache walio ngomeni, hawatasalia wale wasio na hatia. Msiba huwaendea wote.

a. (i) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(al. 4)**

(ii) Jadili namna mrejelewa anavyoendeleza na kukuza vipengele vifuatavyo.

Ploti **(al 3)**

Wahusika **(al 3)**

b. "Pengine maneno yako yana ukweli kidogo"

"Si kidogo. Huu ndio ukweli mtupu. Huu ndio uhalisi wa mambo. Ukweli daima hupendeza kila wakati, ingawa huweza kuwa mchungu pia. My brother, wewe ukitaka kuona penzi usitafte mjini. Nenda kijijini. Huko utabahatika kupata huba. Lakini ujitayarishe kumfundisha ustaarabu wa mji. Umfunze hata kutumia vitu kama microwave, hee hee hee!"

Aliendelea kucheka. Meno yake yalijaa papachi. Inashangaza kwa nini mtemi na mapesa yote yale hakumpeleka kwa daktari wa meno. Angalau aondoe hizo papachi kinywani. ***(al 10)***

**<u>BEMBEA YA MAISHA. (ALAMA 20)</u>**

Jibu swali la pili ama la tatu.

**2.** Tayari unakuwa umeonja seli. Hata wahudumu wenyewe hawana mlahaka mwema. Amri na vitisho kama askari. Unashindwa kama uuguze moyo ama ugonjwa. Katika wodi, hewa iliyojaa harufu ya dawa imezagaa, vitanda vimesalimu amri mpaka shiti zikagura. Yaani hali nzima haikupi matumaini ya kutoka ukiwa bora. Matumaini yanadidimia. Tumaini lako unaliweka katika sala.

a. Tambua toni mbili katika kifungu hiki. **(al 2)**

b. Tambua aina mbili za taswira katika dondoo hili. **(al 2)**

c. Kando ya taswira chambua vipengele sita vya kimtindo. **(al 6)**

d. Fafanua namna mandhari ya dondoo hili yalivyochangia kujenga tamthilia ya Bembea ya Maisha. **(al 10)**

**3. ……**haikuwa mara moja mnavyofikiria, ilianza pale chuoni. Wenzangu walinipa mvinyo kunirai kuonja ulevi.

**a.** (i) Tambua mbinu ya kimtindo inayotawala katika dondoo **(al 2)**

(ii) Eleza namna mbinu uliyoitambua (i) ilivyotumiwa kuendeleza maudhui katika tamthilia nzima ya Bembea ya Maisha. **(al 8)**

**b.** Kwa kurejelea mifano mitano katika tamthilia ya Bembea ya Maisha, eleza tofauti iliopo katika maisha ya ndoa ya zamani na ya sasa. **(al 10)**

**<u>MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI ZINGINE. (ALAMA 20)</u>**

***Jibu swali la 4 au la 5***

**4.** Jamii na serikali zinatunyima sisi wanawake haki na uhuru. Wanawake wanalazimika kuomba ruhusa kwa kila jambo wanalohitaji kufanya. Kabla sijafa, nataka niwe nimepata nafasi ya

kuboresha maisha yangu na yale ya wanangu.

**a.** Eleza muktadha wa dondoo hili. **(al 4)**

**b.** Tambua toni inayojitokeza katika dondoo hili. **(al 2)**

**c.** Eleza jinsi jamii na serikali inanyima wanawake haki na uhuru kwa kurejelea hadithi **Nipe Nafasi.** **(al 7)**

**d.** Tambua mikakati anayochukua msemaji wa maneno haya ili kuboresha maisha yake na wanawe. **(al 7)**

**5.** Umdhaniye ndiye kumbe siye.

**a.** Fafanua ukweli wa kauli hii ukurejelea hadithi ya Mzimu wa Kipwerere**.** **(al 10)**

**b.** Eleza nafasi ya vijana na wazee katika hadithi ya mapambazuko ya machweo.

Wazee **(al 5)**

Vijana **(al 5)**

**<u>USHAIRI (ALAMA 20)</u>**

***Jibu swali la 6 au la 7***

**6.** *<u>Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.</u>*

Nina Habari kamili, naozwa hali nasoma, Nalia sili silali, nakerwa na hino njama, Elimu kwangu halali, ndoa sitamani mama, Ninasoma siolewi!

Naihitaji elimu, japo mie msichana,
Elimu nguzo muhimu, na yenye kubwa dhamana, Kwani kosa gani humu, kuzaliwa msichana?
Ninasoma siolewi!

Dhana kwamba mvulana, akisoma afadhali, Mashiko kamwe haina, ni bure ukatatili, Kuoa na kuoana, kwangu sasa kubwa feli, Ninasoma siolewi!

Wapo wake mahashumu, wasomi mama pulika, Wahimili kuzikimu, aila zao hakika,
Mahari hayatokimu, elimu ghala la nyaka, Ninasoma siolewi!

Nina Mawazo fahamu, japo ubwabwa shingoni, Wazazi nitalaumu, endapo sendi shuleni, Kisomo kunidhulumu, sema kwa sababu gani? Ninasoma siolewi!

Wa nikaha utatimu, muda niozwe mzima, Ela sasa ni haramu, elimu yangu kuzima, Kuoza mwenye elimu, huwa kuu taadhima, Ninasoma siolewi!

**<u>Maswali.</u>**

**a.** Fafanua maudhui makuu manne yanayojitokeza katika shairi hili. **(al 4)**

**b.** Bainisha bahari za shairi hili ukizingatia: **(al 4)**

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 5

**102/1**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 1 (INSHA)**

**MUDA: SAA 1¾**

**NAME**……………………………………………………………………………………

**SCHOOL**……………………………………………… **SIGN**…………………………

**INDEX NO**…………………………………………… **ADM NO**……………………

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

**a)** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
**b)** *Andika insha **mbili**. Insha ya **kwanza** ni ya **lazima.***
**c)** *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya tatu zilizobakia.*
**d)** *Kila insha isipungue maneno **400***
**e)** *Kila insha ina alama **20***

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 40 | |

## MASWALI

1. Wewe ni balozi mteule wa nchi yako katika nchi ya kigeni. Andika tawasifu utakayotoa katika siku ya kutoa stakabadhi zako kwa rais wa nchi uliyoteuliwa kuwa balozi.

2. Utumizi wa afyuni [mihadarati} katika taasisi za masomo nchini ni suala ambalo ni muhali kutatuliwa. Jadili.

3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Mwenye kovu usidhani kapoa.

4. Andika kisa kitakachomalizikia kwa: ... hivyo ndivyo ukurasa mpya katika kitabu cha maisha yangu ulivyofunguka.

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 5

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2 (LUGHA)**

**MUDA: SAA 2½**

**NAME**……………………………………………………………………………………

**SCHOOL**……………………………………………… **SIGN**…………………………

**INDEX NO**…………………………………………… **ADM NO**……………………

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**Maagizo**

*(a)**Andika** jina na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

*(b)Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani*

*(c) Jibu maswali yote.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 4 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| | | |

**Sehemu A: Ufahamu**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo**

Halmashauri ya mpwito nchini imetoa mwongozo kuhusu majukumu yanayofaa kutekelezwa na serikali za kaunti kote nchini kuanzia Julai mosi mwaka huu.

Mwongozo huo utasaidia kuondoa wasiwasi ambao baadhi ya mashirika yasiyo ya serikali yalielezea kuwa huenda baadhi ya sekta zizipate ufadhili kutokana na utata kuhusu ni serikali ipi inafaa kuzishughulikia.

Shughuli hizi zinajumuisha kilimo ambapo zitahakikisha maendeleo ya mimea, mifugo na uvuvi. Serikali za kaunti pia zitashughulikia huduma za afya kuhakikisha kuna sawa na vifaa vya kutosha katika zahanati na hospitali.

Uhifadhi wa mazingira na tamaduni za kijamii kama vile makavazi, maktaba na majumba ya burudani vilevile zitakuwa chini ya usimamizi wa kaunti.

Serikali hizo pia zitasimamia masuala ya uchukuzi kwa kushughulikia ukarabati wa barabara, taa za kudhibiti msongamano wa magari na bandari.

Kulingana na taarifa iliyochapishwa kwenye vyombo vya habari, serikali hizo pia zitashughulikia maendeleo ya biashara na vyama vya ushirika.

Serikali za kaunti zitajihusisha na kudhibiti mipaka na matumizi ya kawi, elimu ya chekechea na vyuo vya ufundi katika ngazi za vijijini, taarifa hiyo ilisema.

Halmashauri hiyo ilisema kuwa serikali hizo zitasimamia uhifadhi wa masitu, ardhi, huduma za maji kupambana na mikasa ya moto, sawa za kulevya na picha za ngono.

Taarifa hiyo iliyotiwa sahihi na mwenyekiti wa halmashauri ya Mpwito ilisema pia serikali za kaunti zinapaswa kuhakikisha kuwa umma umeshirikishwa katika usimamizi wa rasilimali za vijiji.

Kulingana na kipengee cha 15 cha katiba ya Kenya, binge la kitaifa katika muda usiopita miaka mitatu kutoka Siku ya uchaguzi linahitajika kuunda sheria za kuhakikisha kuwa serikali za kaunti zimepata uwezo wa kuendeleza shughuli zake.

Aidha kipengee cha 23 kuhusu ugatuzi kinahitaji halmashauri ya mpwito kutambua shughuli zitakazo tengewa serikali za kaunti kutoka serikali kuu punde to baada ya uchaguzi mkuu. Shughuli hizo zilitayarishwa kupitia hati ya sheria nambari 16 ya 2013.

Katiba katika kipengee cha 24 inatoa masharti ya kufuatwa kabla serikali za kaunti kuanza rasmi shughuli zake za kutoka huduma kwa wananchi.

**Maswali.**

1. Yape makala haya kichwa mwafaka. **(Alama 1)**
2. Je, kaunti inawajibikaje katika kuwahudumia wananchi? **(Alama 2)**
3. Utawala wa kaunti unaweza kupunguza vipi maafa yanayotokea kutokana na mapuuza ya mwanadamu? **(Alama 3)**
4. Bunge la kitaifa lina wajibu gani katika serikali ya kaunti? **(Alama 2)**
5. Ni changamoto zipi zinazoweza kukabili suala la ugatuzi nchini? **( alama 3)**

*6.* Ni kwa njia gani serikali ya kaunti inaweza kufufua uchumi wa nchi na kuinua kiwango cha maisha ili kufikia ruwaza ya 2030. **( alama 2)**

Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika ufahamu. **(alama 2)**

a.) uchukuzi

b.) ugatuzi

**SEHEMU B : UFUPISHO**

Miezi mitano iliyopita,serikali ya kitaifa na zile za kaunti ziliwasilisha makadirio yao ya bajeti,miezi miwili kabla ya mwaka wa kifedha kuisha kama zinavyohitajika na katiba.

Serikali hizo zilieleza jinsi zinavyonuia kutumia mabilioni ya pesa kufadhili shughuli zao mwaka ujao was kifedha was 2017 / 2018.

Serikali ya Raid Uhuru Kenyatta ilisema itatumia shilingi 1.6 trilioni kufadhili maendeleo na shughuli za sekta na idara zake tofauti. Makadirio haya ambayo yaliwasilishwa na kiongozi was kitita hicho kitakavyopatikana. Nasema hivi kwa sababu kuna habari ambazo zimenipa tumbojoto na wasiwasi mkubwa. Imebainika kuwa kufikia mwishoni mwa Machi mwaka huu, Kenya ilikuwa inadaiwa shilingi 1.8 trilioni na wafadhili was humu nchini na wa kigeni.

Kama habari hizi hazijakushtua sitakulaumu kwa sababu huenda ukawa hujui ukubwa wa kiasi hiki cha fedha. Ili uweze kuelewa, nitazigawanya fedha hizi miongoni mwa wakenya milioni 40 ili tujue kila mkenya anadaiwa kiasi gani. Kila mkenya nchini, wakiwemo watoto na wazee wakongwe, anadaiwa shilingi 45,000! Hivyo basi ili deni hili liweze kulipwa, kila mkenya atalazimika kutoa kiasi hicho cha fedha.

Ni deni ambalo Rais Uhuru Kenyatta alirithi kutoka kwa mtangulizi wake,Rais Mwai Kibaki ambayo utawala wake ulivunja rekodi ya kukopa. Wahenga hawakukosea waliposema dawa ya deni no kulipa. Deni hili linapaswa kumkosesha usingizi Rais Kenyatta ambaye anapaswa kutafuta njia za kulilipa bila kuathiri uchumi, maendeleo na utekelezaji was ahadi nyingi alizowapatia wakenya wakati wa kampeni.

Hili halitafanyika kama serikali itatenga fedha nyingi kuwalipa maafisa wake mishahara na marupurupu minono pamoja na kuwapa mabilioni ya pesa kununulia magari ya kifahari. Pengine rais hajafahamishwa kuwa mwaka ujao was kifedha serikali itajipata pabaya kwani Halmashauri ya Ukusanyaji ushuru nchini (KRA), haitaweza kukusanya kiwango kilichowekewa na serikali baada ya shughuli ya ukusanyaji ushuru kutatizwa na hofu iliyotanda wakati was uchaguzi mkuu.

KRA ilikuwa imekusanya shilingi 560 bilioni kufikia mwishoni mwa mwaka ilhali ilikuwa imeagizwa kukusanya shilingi 881 bilioni.

Serikali za kaunti, ambazo zingali changa, zimependekeza kutumia mabilioni ya fedha ambazo hazitaweza kukusanya. Badala yake zimeiomba serikali kuu ijaze pengo hilo au zipewe idhini ya kukopa.

Rais Kenyatta hana budi kuchukua hatua za dharura kuhakikisha kuwa wakenya hawataendelea kuandamwa na madeni maishani mwao.

***(Imenukuliwa kutoka Taifa Leo- Mei 9,2017)***

**<u>MASWALI</u>**

**a)** Kwa maneno yasiyozidi 70, fupisha aya za kwanza nne. **(alama 10)**

**b)** Kwa nini serikali haitaweza kulipa madeni yake.(maneno 40-50**)** **(alama 5)**

**C. MATUMIZI YA LUGHA**

***a)*** Linganisha sauti /o/ na /w/. **(alama 2)**

***b)*** Eleza maana ya silabi funge na utoe mfano mmoja wa neno na uiibainishe. **( alama 2)**

***c)*** Eleza miundo miwili ya nomino katika ngeli ya U-ZI na utoe mfano mmoja wa kila muundo. **(alama 2)**

***d)*** i) Eleza maana ya kiambishi. **( alama 1)**

ii) Ainisha viambishi katika neno hili: **(alama 3)**

humfisha

***e)*** Tunga sentensi iliyo na muundo ufuatao: **( alama 3)**

KN(W+V+E)+KT(T+KE)

***f)*** Andika katika usemi wa taarifa. **( alama 2)**

"Sitakuja shuleni kesho." Asha alisema.

***g)*** Tunga sentensi moja ukitumia kiwakilish kiashiria cha karibu katika ngeli ya KU-KU.**(alama 2)**

***h)*** Tunga sentensi moja moja kwa kila jozi kubainisha maana ya maneno yake. **( alama 2)**

sima /zima

dada /tata

***i)*** Eleza maana mbili za sentensi hii. **( alama 2)**

Mwanafunzi alimwendea mwalimu ofisini.

***j)*** Unda aina za nomino zilizo mabanoni kutokana na maneno uliyopewa. **(alama 2)**

i. refu (kitenzi jina)

ii. erevu (dhahania)

***k)*** Tunga sentensi **<u>moja</u>** katika wakati uliopita hali ya kuendelea. **(alama 2)**

***l)*** Yakinisha sentensi ifuatayo katika wingi. **(alama 2)**

Nisipomlipa pesa zake, hataniamini tena wakati ujao.

***m)*** Akifisha sentensi hii. **( alama 3)**

labeka maria alimjibu mamake nisubiri hadi alhamisi

***n)*** Bainisha aina za vitenzi katika sentensi ifuatayo. **(alama 3)**

Wewe ulikuwa ukifunga mabao mengi kwa sababu u mchezaji bora.

o) Andika sentensi ifuatayo upya katika hali ya mazoea. **alama 2)**

Nguo zinazochafuka ndizo zinazofuliwa.

p) Eleza matumizi ya "po" katika sentensi ifuatayo. **( alama 2)**
Ali**po**ona ali**po**keti palikuwa na vumbi, alisimama.

q) Tambua na ueleze aina za virai katika sentensi hii. **(alama 2)**
Mama mzee alikuwa anatabasamu.

r) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendeshwa. **(alama 1)**
i) la

ii) nywa

**D. ISIMU-JAMII (ALAMA 10)**

**(a)** Eleza **maana** ya lugha **(alama 1)**

**(b)** Andika sifa **nne** za lugha. **(alama 4)**

**(c)** Eleza sifa **tano** za sajiri ya maabadini. **(alama 5)**

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 5

**102/3**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 3 (fasihi)**

**MUDA: SAA 2½**

**NAME……………………………………………………………………………………**

**SCHOOL……………………………………………… SIGN…………………………**

**INDEX NO……………………………………………… ADM NO……………………**

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

- **a)** *Andika jina lako, nambari ya usajili, mkondo, sahihi na tarehe katika nafasi ulizoachiwa.*
- **b)** *Jibu maswali **manne** pekee.*
- **c)** *Swali la kwanza ni la **lazima**.*
- **d)** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Fasihi Simulizi.*
- **e)** *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
- **f)** ***Maswali yote ni sharti yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.***

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

**SEHEMU A: LAZIMA**

**FASIHI SIMULIZI**

**SOMA UTUNGO FUATAO KISHA UJIBU MASWALI**

Apingaye akidi yangu na Kanini wa Miteni
Nyota kutoka angani,uteuzi wa mtimani
Na ashushe shamsi aligeuze kigoda
Ama amchukue bafe,asugulie meno kwaye!
Mwingine kamawe sioni,daharini na hata ahera,
Ila kunali lanikama roho,kama masuo anitema
Nikimlunga anikwepa,kunitia fundo moyoni,
Anisonya na kuniasi,mabezo kunionyesha
Kisa ndinyi mahasifi, mlonitilia utambi
Kanini anichukie,sili sisemi silali
Moyongu kunitetema,narai mjibari naye
Barafu ya moyo wangu
Sijui nitumie nini,lulu yangu nirudie,
Hirizi nitumie gani,impagaze tunu angu
Anikalia shonde,mmhibu kunivuruga mtimani
Tamu yake ya zamani,imekuwa tamu chungu
Yu wapi huyo tabibu,hirizi dawa anipe?
Nimpe huyu kigoli,anipe yake mahaba
Waganga na waganguzi nipeni hino na tembe
Punguze haya madhila,ya hili penzi kunila.

**MASWALI**

- **a)** Huu ni wimbo wa mapenzi. Thibitisha kwa kutoa hoja sita. **(alama 6)**
- **b)** Tambua nafsineni katika utungo huu. **(alama 1)**
- **c)** Tambua toni mbili zinazojitokeza kwenye utungo huu. **(alama 2)**
- **d)** Jadili mifano sita ya matumizi ya lugha/kimtindo katika utungo huu**.** **(alama 6)**
- **e)** Fafanua umuhimu wa fasihi simulizi. **(alama 5)**

**SEHEMU B: TAMTHILIYA**

**TIMOTHY AREGE: BEMBEA YA MAISH**A

**Jibu swali la 2 au 3**

2``Hekima si hekima itokapo kwa mwanamke''

a) Eleza muktadha wa maneno haya **(alama 4)**
b) Fafanua toni inayojitokeza katika dondoo. **(alama 2)**
c) Fafanua umuhimu wa mandhari katika nukuu. **(alama 4)**
d) Eleza jinsi kauli hii ni kinaya ukirejelea tamthilia nzima. **(alama 10)**

**AU**

**3**

**i.** Jadili suala la elimu kama linavyojitokeza katika tamthilia ya bembea ya maisha.**(alama 10)**

**ii.** Kazi hizi nazo ni kama safari ya ahera; mwisho wake hakuna mwenye habari nayo. Basi imekuwa mfano wa magurudumu kwenye gari la masafa marefu,lenyewe hilo linasukumwa tu. Linaviringiswha bila kupenda; halina hiari wala muhitari. Kazi yake kumenyana na ardhi; si pa mvua si pa jua. Haijalishi kkama kuna miba au mawe. Kwake mwendo ni wajibu. Yaani hata likachomeka haliwezi likafumua moto. Ndivyo maisha yetu yalivyo. Tunaendeshwa kama tiara. Upepo unatupigia tukiwa hewani huku mshika kamba pale chini anaona raha kwa sisi kuyumbishwayumbishwa.

a) Eleza muktadha wa dondoo. **(alama 4)**

b) Tambua mbinu mbalimbali zinajitokeza katika kifungu ulichopewa. **(alama 4)**

c) Bainisha sifa zozote mbili za msemewa wa maneno haya. **(alama 2)**

**SEHEMU C: HADITHI FUPI**

**DW LUTOMIA NA P.MUTHAMA(WAH) MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE;Jibu swali la 4 au 5**

**4. FADHILA ZA PUNDA: RACHEL WANGARI**

``Uliacha mbachao kwa msala upitao''

**a.** Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

**b.** Jadili istilahi ya lugha iliyotumika. **(alama 2)**

**c.** Fafanua sifa tano za msemewa. **(alama 5)**

**d.** Jadili maudhui ya dhuluma katika hadithi za fadhila za punda. **(alama 9)**

**AU**

**5. NIPE NAFASI/NILITAMANI**

a. Jadili namna maudhui ya ubabedume yalivyodhihirika katika hadithi ya ``*Nipe Nafasi*''
**(alama 10)**

b. ``Hali ya uhitaji husababisha athari hasi''. Thibitisha kauli hii kwa kurejea hadithi.``*nilitamani*''.
**(alama 10)**

**SEHEMU D: USHAIRI**

**Jibu swali la 6 au 7**

**6. SOMA SHAIRI LIFUATALO KISHA UJIBU MASWALI**

Kidete ninasimama,ninene yalo moyoni,
Na nyinyi muweni wima,masikiyo yategeni,
Nalikashifu mapema,la ulevi hadharani,
Dawa hizi za kulevya,mbona mwazikimbilia?

Mihadarati mwapenda,kaburi mwajichimbia,
Siha zenu mwaziponda,vifi vingi kuibua,
Mbegu mbovu mwazipanda,maskini mwajifia,
Dawa hizi za kulevya,mbona mwazikimbilia?

Meleta wingi wazimu,akili kuvurugika,
Kwa mambo mwazipada,maskini mwajifia,
Dawa hizi za kulevya,mboa mwazikimbilia?

Dawa hizi kitumiwa,jamii huathirika,
Ugomvi yake mabawa,yanapaa kwa haraka,
Wake wanadhulumiwa,mawazo yapapatika,
Dawa hizi za kulevya, mbona mwazikimbilia?

Na magonjwa ya zinaa,kila siku mwaeneza,
Mejazana kwa mabaa,ukahaba kuiguiza,
Mwakosa kujitambua,ukimwi mwajipangaza,
Dawa hizi za kulevya,mbona mwazikimbilia?

**MASWALI**

1. Ainisha shairi hili kutegemea; **(alama 3)**
   i. Idadi ya mshororo katika kila ubeti wa shairi hili.
   ii. Idadi ya vipande katika kila mshororo wa shairi hili.
   iii. Mpangilio wa vina wa shairi hili.
2. Taja madhara manne yanayosababishwa na dawa za kulevya. **(alama 4)**
3. Eleza muundo wa shairi hili. **(alama 4)**
4. Andika ubeti wa tano kwa lugha ya nathari/tutmbi/kawaida. **(alama 4)**
5. Andika mifano mitatu ya uhuru wa kishairi kutoka kwenye shairi hili**.** **(alama 3)**
6. Eleza toni ya mshairi. **(alama 1)**
7. Tambua nafsi-neni na nafsi-nenewa katika shairi hili. **(alama 1)**

**Au**

**7. SOMA SHAIRI LIFUATALO KISHA UJIBU MASWALI**

**1)** Tunda la elimu zote,wanansema wanazuoni
Ni kwamba mtu apate,kumtambua manani
Ndipo hadhi apate,akumbukwe duniani.

**2)** Elimu bila ukweli,haizidi asilani
Giza na nuru muhali,katu havitangamani
Uwongo ufe kweli,itue nuru moyoni

**3)** Elimu ni kama mali,haichoshi kutamani
Ni bora yashinda mali, taji la wanazuoni
Elimu njema miali,langazayo gizani

**4)** Mtu hachomwi na mwiba,na viatu miguuni
Ulimwengu una miiba,tele tele majiani
Elimu ukiishiba,u salama duniani.

**5)** Wafu ni wasiosoma,watazikwa ardhini
Hai ndio maulana,wapaao maangani
Elimu jamboadhima,aso nayo maskini.

**6)** Toa wakfu ujana,elimu ukitamani
Na uwe mzee sana,kuju usijihini
Elimu ni jambo adhima,aso nayo maskini.

**7)** Elimu ina alipo,utoyalipwa mwishoni
Pale uitafutapo,ujira usitamani
Mwanachuoni afapo,mbingu uwa na huzuni.

**8)** Haki ya kuheshimiwa, ni yao wanachuoni
Wao wameongelewa,na ni taa duniani
Kweli wanapoijua,watoe bila kuhuni.

**9)** Elimu bila amali,mti usio majani
Haumtii kivuli,aukaliaye chini
Inakuwa mashkeli,wa kughuri insane

**Maswali**

**a)** Fafanua ujumbe mkuu/dhamira katika shairi hili **(alama 2)**

**b)** Taja aina na bahari ya shairi hili kutegemea;idadi ya mishororo katika kila ubeti,idadi ya vipande katika kila mshororo na mpangilio wa vina. **(alama 3)**

**c)** Jadili jins mshairi ametumia idhini yake. **(alama 3)**

**d)** Fafanua maudhui katika ubeti wa tatu na wa saba **(alama 4)**

**e)** Andika ubeti wa mwisho kwa lugha ya tutumbi/nathari. **(alama 3)**

**f)** Eleza toni,nafsi-neni na nafsi nenewa katika shairi hili. **(alama 3)**

**g)** Eleza maana ya maneno yafuatayokama yalivyotumika kayika shairi **(alama 2)**

i. Adhima

ii. Wameonolewa

**SEHEMU E. RIWAYA**

**CLARA MOMANYI: NGUU ZA JADI**

``kiongozi si mwanasiasa pekee. Kila mmoja wetu ni kiongozi kwa namna yake ya kipekee.’’

**a)** Andika muktadha wa maneno haya. **(alama 4)**

**b)** Eleza umuhimu wa mnenaji. **(alama 4)**

**c)** Fafanua umuhimu wa mandhari katika nukuu. **(alama 4)**

***d)*** Tathmini

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 6

**102/1**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 1 (INSHA)**

**MUDA: SAA 1¾**

NAME…………………………………………………………………………………

SCHOOL……………………………………………… SIGN…………………………

INDEX NO…………………………………………… ADM NO………………………

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

***a)*** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

***b)*** *Andika insha* ***mbili****. Insha ya* ***kwanza*** *ni ya* ***lazima.***

***c)*** *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya tatu zilizobakia.*

***d)*** *Kila insha isipungue maneno* ***400***

***e)*** *Kila insha ina alama* ***20***

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 40 | |

**SWALI LA KWANZA (LAZIMA)**

**1.** Wewe ni mwenyekiti wa kamati ya kupigana na ufisadi nchini Kenya na umealikwa, kuhutubia kongamano la kitaifa kuhusu athari za ufisadi huku ukipendekeza hatua za kukabiliana na janga hili. Andika hotuba utakayoitoa. **(Alama 20)**

**2.** Nyimbo za kitamanduni zilikuwa na nafasi kubwa katika ufanisi wa jamii kwa jumla. Eleza. **(Alama 20)**

**3.** Andika kisa kitakachodhihirisha ukweli wa methali isemayo;.

Bahati ni chudi **(Alama 20)**

**4.** Andika insha itakayomalizia kwa maneno yafuatayo;

**….**Hapo ndipo iliponibainikia kuwa nilikuwa nikiogelea baharini pekee kinyume na wenzangu wote.

**(Alama 20)**

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 6

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2 (LUGHA)**

**MUDA: SAA 2½**

**NAME**……………………………………………………………………………………

**SCHOOL**……………………………………………… **SIGN**…………………………

**INDEX NO**…………………………………………… **ADM NO**……………………

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**Maagizo**

***(a)Andika*** *jina na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

***(b)****Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani*

***(c)*** *Jibu maswali yote.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 4 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| | | |

**UFAHAMU (ALAMA 15)**

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali***

Hakuna dakika inayopita bila kisa cha kuchelewa. Mikutano karibu yote huchelewa kuanza kwa sababu wahusika hawafiki wakati ufaao. Ibada nazo hucheleweshwa kwa uzembe wa waumini. Na mazishi je? Taratibu hucheleweshwa vilevile. Ingawa hapa yaweza kufikiriwa kuwa pengine wampendao marehemu hawataki kuharakisha safari yake ya kwenda kuzimuni. Lakini hata arusi ambazo huwa na misururu ya mikutano ya maandalizi, siku itimiapo shughuli huchelewa. Si ajabu sherehe kuendelea mpaka usiku ambapo ratiba ilionyesha zingekomea masaa ya alasiri.

Uchunguzi unabainisha kuwa watu huchelewa kwa sababu mbalimbali. Sababu mojawapo ni kutowajibika; yaani, watu wengi hawaoni umuhimu wa kuzingatia saa. Wengine hufanya hivi kwa kisingizio kuwa ni kawaida ya mwafrika kutozingatia muda. Huu ni upuuzi mtupu. Wazee wetu walizingatia muda ipasavyo tangu jadi ingawa hawakuwa na saa wala kalenda. Hii ndiyo sababu walipanda mimea walipohitajika, wakavuna na hatimaye wakapika na kuandaa ipasavyo. Wahenga hawa walituachia methali nyingi kama funzo, kwa mfano; ‘Chelewachelewa utakuta mwana si wako’, na hata wakasindikiza kuwa, ‘Ngoja ngoja huumiza matumbo’.

Watu wengine huchelewa kwa sababu ya kutojiandaa kwa yale yatakayojiri. Watu wasiopanga shughuli zao na badala yake kuzifanya kwa kushtukia aghalabu hushindwa kuhudhuria hata mahojiano ya kuajiriwa kazi kwa wakati ufaao. Hawa huwa neema kwa washindani wao. Kujitayarisha si jambo gumu. Anachopasa kujua mhusika ni saa ya miadi na hali ya usafiri.

Hivi viwili vitamwezesha kujua muda wa safari na hivyo kukadiria wakati wa kuondoka. Ni wangapi wameiona milolongo ya watu nje ya milango ya benki wakiwasihi mabawabu na pengine kuwahonga wawaruhusu kuingia? Hawa huwa si wageni. Ni wateja wanaojua ratiba ya kazi lakini hushindwa kupanga mwenendo wao barabara.

Mikutano, sherehe na shughuli nyingi huchelewa kuanza kwa masaa mengi kwa sababu eti mgeni mashuhuri amechelewa kufika. Muda wa kungoja huwa mrefu zaidi kutegemea ukubwa wa cheo cha mhusika. Watu hawa huchelewa makusudi kwa sababu pengine ya kiburi. Majivuno haya huwafanya wafurahi wanaposubiriwa na watu wadogo. Wakubwa hawa wanapofika badala ya kuomba msamaha, hujigamba kuhusu majukumu yao mengi na makubwa.

Aidha kuna watu ambao hupenda kutekeleza mambo mengi kwa wakati mmoja. Tujuavyo ni kuwa mambo mawili yalimshinda fisi. Pia watu wanaposhika mengi, mahudhurio yao katika baadhi ya mambo hutatizwa na hivyo huchelewa. Isitoshe, kuna watu wa aina hii hata wanapopewa ratiba mapema, hujikokota na hivyo kupitwa na wakati.

Ingawa sababu tulizozitaja hutokana na watu wenyewe, kuna zile zinazosababishwa na dharura nyingine. Hizi ni pamoja na misongamano ya magari, kuchelewa kwa vyombo vya usafiri na hata kuharibika kwa vyombo. Hii ndiyo sababu inashauriwa kuwa mtu anapoamua kutekeleza jambo, atenge muda takribani wa dakika 30 kwa ajili ya dharura fulani. Kwa hivyo hata anapopata tuseme pancha njiani bado atafika kwa wakati ufaao.

Kuchelewa hakuudhi tu watu wanaocheleweshwa bali huwa na matokeo mengine mengi. Mara nyingi watu waliochelewa huharakisha mambo ili kufidia muda walioupoteza. Kama wanaendesha gari, kwa mfano, basi huzidisha kasi matokeo huweza kuwa ajali ambayo mara nyingine huleta ulemavu au vifo.

Ratiba ya mambo ichelewapo watu waliofika mapema hupoteza muda kusubiri. Muda huu wangeutumia kwa harakati muhimu. Mfumo wa uchumi wa kisasi unahitaji mamilioni ya watu kukurubiana, kutagusana na kuendesha shughuli zao kwa ujima. Aidha, watu hawana budi kubadilishana bidhaa na huduma. Mambo haya yanapocheleweshwa basi gharama huwa kubwa.

Tatizo hili hubainika sana katika ofisi za umma.

Ni kwaida watu kufika kazini dakika nyingi baada ya wakati wa kufungua milango ya kazini. Ajabu ni kuwa wafanyakazi wawa huwa wa kwanza kufunga kazi kabla ya kipindi rasmi. Inakisiwa Kenya hupoteza shilingi bilioni 80 kila mwaka kupitia uzembe wa kutozingatia wakati.

Jambo la kwanza ni kuweka sera ya kitaifa inayolenga kuwaelimisha wananchi umuhimu wakuzingatia saa. Halikadhalika kanuni iwekwe ya kuwafungia nje watu wanaochelewa kuhudhuriashughuli za mikutano au hafla. Wananchi nao wazinduliwe kuwa ni haki yao kufumkana muda washughuli unapowadia kabla mgeni wa heshima kufika. Nchi ya Ekwado (Ecuador) imefanikiwakutekeleza haya. Kenya pia haina budi kuandama mwelekeo huo. Hii ndiyo njia mojawapo ya kufufua uchumi na kuhakikisha taifa linapiga hatua kimaendeleo.

***<u>Maswali:</u>***

**1.** Kipe kifungu hiki anwani mwafaka **(ala. 1)**

**2.** Taja watu **<u>watatu</u>** walio na mazoea ya kuchelewa katika shughuli walizoalikwa **ala. 3)**

**3.** Taja sababu zinazofanya watu kushindwa kutimiza miadi **ala. 4)**

**4**. Taja na ueleze njia **<u>nne</u>** zinazoweza kuondoa tatizo la kuchelewa **ala. 4)**

**5.** Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika taarifa **ala. 3)**

***a)*** ujima

***b)*** miadi

***c)*** pancha

## F. <u>UFUPISHO (ALAMA 15)</u>

***<u>Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yote</u>***

Takriban kila siku vyombo vya habari hueleza kuhusu mateso ya watoto; cha kusikitisha zaidi ni kwamba mbali na visa vinavyoripotiwa, kuna vingine chungu nzima ambavyo havijaripotiwa. Mateso kwa watoto hawa ni ya aina mbalimbali. Mwezi wa Julai, 2005 wavamizi walipowaua watu zaidi ya sabini Kaskazini mwa Kenya, walianza

kwa kuwauwa watoto katika shule ya msingi ya Mabweni. Waliwauwa watoto ishirini na wawili huku mamia wakijehuriwa.

Kuna wazazi ambao huwapiga watoto wao mithili ya kumpiga nyoka. Utaona watoto wakiwa na majeraha yanayofanya malaika kusimama mwilini. Visa vingi vimeripotiwa ambapo wazazi au walevi huwakata au kuwadhuru watoto sehemu fulani za mwili kama vile masikio, miguu au mikono. Vilevile, kumetokea visa vya kuwachoma watoto na wengine kuwachwa bila chakula.

Kenya ni mojawapo ya nchi zilizotia sahihi mkataba wa kulinda haki za watoto. Serikali yetu ina idara katika ofisi ya makamu wa rais inayoshughulikia maslahi ya watoto. Mwezi wa Julai 2005, Serikali ilianzisha kampeni kabambe za kukomesha mateso dhidi ya watoto. Ajabu ni kwamba watu wengi na hata watoto wenyewe hawajui haki zao. Sheria ya watoto ilipitishwa ili kutetea haki za watoto katika nchi ya Kenya.

Baadhi ya haki za watoto ni kama vile kulindwa kutokana na ubaguzi wowote, kutunzwa na wazazi na kupewa elimu. Watoto wana haki ya elimu ya kiakademia na dini. Vilevile wana haki ya kulindwa kiafya. Watoto hawatakikani kunyanyaswa kiuchumi au kwa njia nyinginezo kama vile kusajiliwa kupigana katika vita. Kila mtoto akiwemo mlemavu, ana haki ya kuheshimiwa katika jamii.

Hata hivyo, sharti pia watoto wawajibike ipasavyo kwa wazazi, walezi na jamii kwa jumla. Mtoto anapaswa kuheshimu wakuu wake na kuwasaidia panapo haja. Watoto wana jukumu la kudumisha na kuimarisha umoja wa jamii na raia kuendeleza maadili mema katika jamii.

***<u>Maswali:</u>***

**(a)** Fupisha aya ya kwanza na ya pili kwa maneno 60-80 **(ala. 6, mtiririko 1 )**

**(b)** Bainisha mambo muhimu aliyoyajadili mwandishi katika aya tatu za mwisho. (Maneno 100 – 120 ) **(ala. 20, mtiririko 1)**

**G. <u>SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA</u>** **(ALAMA 40)**

***(a)*** Taja vipasuo <u>viwili</u> vya ufizi **(alama 2)**

***(b)*** Onyesha maumbo <u>mawili</u> ya silabi funge kwa kutolea mifano katika maneno **(alama 2)**

***(c)*** Bainisha mofimu za neno 'kilichonywewa' **(alama 3)**

***(d)*** Unda nomino moja moja kutokana na nomino zifuatazo **(alama 2)**

(i) Madhara

(ii) Kitenzi

***(e)*** Tambua virai vihusishi katika sentensi ifuatayo **(alama2)**

Wengine wao waliegesha kando ya barabara iliyokarabatiwa na kampuni ya Kichina

***(f)*** Andika sentensi zifuatazo upya kwa kutumia 'po' **(alama 2)**

(i) Raia wakipatana maendeleo yataimarika

(ii) Mkiwatesa watoto wenu mtashtakiwa

***(g)*** Andika kwa ukubwa hali timilifu **(alama 3)**

Mtego ulimnasa ndovu huyo

***(h)*** Andika sentensi ifuatayo upya ukibadilisha neno lililopigiwa mstari kuwa kivumishi **(ala. 2)**

Msichana amepigwa <u>vibaya</u>

***(i)*** Ainisha yambwa na chagizo katika sentensi ifuatayo **(alama 4)**

Wanafunzi walimwatikia mwalimu mkuu miche ya matunda nje ya nyumba yake kwa ustadi wakitumia vijiti.

***(j)*** Andika visawe viwili vya neno 'vurumai' **(alama 2)**

***(k)*** Taja na utolee mifano matumizi mawili ya mshazari **(alama 2)**

***(l)*** Tunga sentensi yenye muundo ufuatao kisha uichanganue kwa matawi **(alama 4)**

S – KN (N + V) + KT (T + E)

***(m)*** Andika kwa usemi halisi **(alama 2)**

Kyalo alikiri kuwa kama wangefika mapema wangekamilisha shughuli zote

***(n)*** Tofautisha maana ya sentensi zifuatazo **(alama 2)**

(i) Alipokelewa mgeni

(ii) Alipokezwa mgeni

***(o)*** Andika kinyume **(alama 3)**

Vijana walivunja kambi baada ya macheo

***(p)*** Kanusha **(alama 3)**

Asha aliwapelekea wageni chakula na akawanavya mikono

**H. <u>ISIMU JAMII</u>** **<u>(ALAMA 10)</u>**

**(a)** Eleza sifa zozote tano za lugha ya itifaki **(alama 5)**

**(b)** Hakiki sifa zozote tano za sajili ya kituo cha polisi **(alama 5)**

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 6

**102/3**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 3 (fasihi)**

**MUDA: SAA 2½**

**NAME……………………………………………………………………………………**

**SCHOOL……………………………………………… SIGN…………………………**

**INDEX NO……………………………………………… ADM NO……………………**

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

**a)** *Andika jina lako, nambari ya usajili, mkondo, sahihi na tarehe katika nafasi ulizoachiwa.*
**b)** *Jibu maswali* ***manne*** *pekee.*
**c)** *Swali la kwanza ni la* ***lazima****.*
**d)** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Fasihi Simulizi.*
**e)** *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
**f)** ***Maswali yote ni sharti yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.***

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

## SEHEMU A: USHAIRI

**1. LAZIMA**

Awaza akiwazua,kwa nini yeye hiniwa?
Kasi yeye ajibikia,yote masaa 'takiwa
Sawa punda amekuwa,masaibu andaliwa
Bahati inamwandama,apaa fika paani

Ngumu kasi kwa hakika,wake moyo tamaata
Yake maisha umika,nyingi hatari 'apata
Sugu wechi awashika,kiua tabu zipata
Bahati inamwandama,apaa fika paani

Butu silaha zishika,marafiki wa daima
Adui anamyeka,kali silaha jihama
Mengi mateso 'teseka,lini haya yatakoma?
Bahati inamwandama,apaa fika paani

Mifuko dola 'kimbia,mamilioni ye'lindia
Peso peso mchukia,zimwonapo kakimbia
Omba omba kakua,mahitaji mlemea
Bahati inamwandama,apaa fika paani

Ulinzi atolea,usingizi twaupata
Giza macho tumbulia,nyinyi hatari huleta
Baridi mtekenyea,mbu mlo waupata
Bahati inamwandama,apaa fika paani

Mfano kuku 'jifia ,machozi mamba liliwa
Mhesh' akizimia,upesi ambolezewa
Familia zaumia,misada kosa tumiwa
Bahati inamwandama,apaa fika paani

Machache tu kayanena,mengi 'tatizo kalia
Serukali kaazana,yake hali badilia
Asikaru atapona,mema malipo raia
Bahati inamwandama,apaa fika paani.

**Maswali.**

**a)** Nafsi nenewa katika shairi hili ana masaibu si haba. Thibitisha. **(alama 5)**
**b)** Fafanua njia zozote tatu alizotumia mshairi ili kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. **(alama 3)**
**c)** Eleza muundo wa shairi hili. **(alama 3)**
**d)** Changanua mitindo yoyote miwili iliyotumika katika shairi hili. **(alama 2)**
**e)** Eleza toni ya shairi hili. **(alama 2)**
**f)** Bainisha bahari **tatu** zilizotumika katika shairi hili **(alama 3)**
**g)** Andika ubeti wa **nne** kwa lugha nathari. (**alama 2)**

**SEHEMU B: RIWAYA**

**C. Momanyi: Nguu za Jadi.**

***Jibu swali la 2 au la 3.***

**2** ‘Suluhisho ni kwamba hayo mahema yapelekwe Matango… Hatuhami hata kwa makombora.’

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

b) Eleza sifa **nne** za msemaji. **(alama 4)**

c) Fafanua umuhimu wa mandhari ya dondoo hili. **(alama 4)**

d) Fafanua mikakati ambayo msemaji na wenzake walitumia kukabiliana na hali zao katika nchi ya Matuo. **(alama 8)**

**3.a)** Changanua mtindo katika dondoo hili. **(alama 6)**

‘…hakuwa na hamu ya kuzikimbilia zile noti wala kuchota zile sarafu.Alipozitazama,zilimtafishi na kumtia kichefuchefu.Hapo alipata nafasi ya kulikimbia na kujisalimisha.Jinamizi hilo lilimshtua sana hadi akaamka.Mwili wote ulilo jasho.Alijaribu kulala tena lakini akashindwa kabisa.Hapo ndipo aliposikia mayowe mfululizo.Kuna nini?Alifungua dirisha la chumba chake akatazama nje.Mama yangu!

b) ‘Lazima tuokoe kizazi hiki kinachopotea nyikani bila matumaini.’

i) Msemaji wa kauli hii amedhihirisha uwajibikaji mkubwa katika jamii. Thibitisha. **(alama 7)**

ii) Jadili changamoto zinazowakumba wananchi kwa kurejelea hotuba ya Lonare katika Uga wa Taifa. **(alama 7)**

**SEHEMU C: TAMTHILIA**

**T.M.Arege: Bembea ya Maisha**

***Jibu swali la 4 au la 5***

**4.** ’’Yenyewe yamekuja wakati wake bora.Yangetokea jana ile ,leo hii tusingekuwa na la kusema’’

**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

**b)** Bainisha toni inayojitokeza katika dondoo hili. **(alama 2)**

**c)** Eleza umuhimu wa msemewa wa maneno haya katika kujenga:

i. Sifa za wahusika **(alama 6)**

ii. Maudhui **(alama 8)**

**5** i. “Mara ile nilipokuja kilijitia kunifundisha hata kikanipa na homework!”

**a)** Eleza sifa sita za msemaji wa maneno haya. **(alama 6)**

**b)** Fafanua umuhimu wa mandhari ya dondoo hili katika kuendeleza tamthilia ya Bembea ya maisha. **(alama 6)**

ii. Bembea inapolika na kukatika haiwi mwisho wa mchezo.

Jadili ukweli wa kauli hii ukirejelea tamthlia ya *Bembea ya Maisha*. (alama 8)

**SEHEMU D: HADITHI FUPI**

**D.W.Lutomia na P. Muthama(wah.): Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine.**

***Jibu swali la 6 au la 7***

**6 .P. Muthama.''Nilitamani''**

''Wajua siku hizi huwezi kuamini yeyote apitaye na hasa akiomba msaada au umekuja kututapeli?

**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

**b)** Fafanua umuhimu wa msemewa wa maneno haya katika kukuza maudhui katika hadithi hii. **(alama 5)**

**c)** Fafanua jinsi mbinu ya majazi imetumika kujenga wahusika katika hadithi ya ''Msiba wa Kujitakia.'' **(alama 5)**

**d)** Eleza changamoto **sita** zilizokumba wafanyikazi katika hadithi ya ''Harubu ya Maisha.'' **(alama 6)**

**7.** ***D.M.Oigo :Kifo cha Suluhu***

''Kwa muda wote nilioishi nawe, sikukuendea kinyume wala hayakunijia kichwani mawazo yenyewe.''

**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama 4)**

**b)** Mrejerewa wa kauli hii anastahili kuomba msamaha.Thibitisha **(alama 8)**

**c)** Eleza namna maudhui ya uwajibikaji yalishughulikiwa katika hadithi ya Mapambazuko ya Machweo. **(alama 8)**

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**

**8. <u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata</u>.**

Katika enzi za zamani kabla ya majilio ya wakoloni,vita vilitokea kati ya jamii ya Sangura na jamii ya Kitivo.Vita hivi vilipiganwa na wanaume pekee kwa sababu jamii ya Sangura ilitaka kulipiza kisasi dhidi ya jamii ya Kitivo iliyokuwa imewaibia ngombe,mbuzi na kondoo wao.Kila jamii iliamini kuwa ingeshinda vita hivyo kutokana na kila jamii kuwa na zana zake za kivita kama mishale iliyopakwa sumu ya nyoka.

Kitali hiki kilizuka na kupiganwa kwa majuma mawili bila maji na chakula.Jamii ya Sangura iliwazidi nguvu wapiganaji kutoka jamii ya Kitivo na kuwaua kama mende.Walionusurika walikumbatiwa na wahaka uliowasababisha kutorokea kwingine ili kuopoa nafsi zao.

Jamii nzima ya Kitivo ilibaki na wanawake pekee bila wanaume.Wanawake wa Kitivo waliishi kwa majonzi kutokana na yale yaliyowajia ghafla hadi wanaume wa jamii ya Sangura wakawahurumia na kuamua kuwarithi.Watoto waliozaliwa walianza kuzungumza Kisangura.Hivi ndivyo jamii ya Kitivo ilivyomezwa na jamii ya Sangura na eneo zima la Kitivo likawa eneo la Sangura.

**<u>Maswali.</u>**

**a)** Tambua na ufafanue kipera cha hadithi ulichokisoma hapo juu **(alama 2)**

**b)** Eleza sifa **sita** za kipera ulichokitaja hapo juu **(alama 6)**

**c)** Fafanua vizingiti **vinn**e vinavyokumba ngomezi katika jamii **(alama 4)**

**d)** Eleza namna fanani anaweza kuihusisha hadhira katika usimulizi wake **(alama 4)**

**e)** Fafanua umuhimu wa kutumia maandishi kama njia ya kuhifadhi data **(alama 4)**

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 7

**102/1**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 1 (INSHA)**

**MUDA: SAA 1¾**

**NAME……………………………………………………………………………………**

**SCHOOL…………………………………………………  SIGN…………………………**

**INDEX NO……………………………………………… ADM NO………………………**

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

a) *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
b) *Andika insha* ***mbili****. Insha ya* ***kwanza*** *ni ya* ***lazima.***
c) *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya tatu zilizobakia.*
d) *Kila insha isipungue maneno* ***400***
e) *Kila insha ina alama* ***20***

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 40 | |

**SWALI LA KWANZA (LAZIMA)**

1. Umeteuliwa kuwa katibu wa kikao kikao kitakachowaelimisha wananchi kuhusu njia mbalimbali za kupambana na umaskini nchini. Andika hotuba utakayoitoa.

2. Vijana wamekumbwa na changamoto si haba.Thibitisha.

3. Andika insha itakayodhihirisha maana ya methali:

Samaki mkunje angali mbichi.

4. Andika insha inayoanza kwa:Nilipopata fahamu/nilikuwa hospitalini…

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 7

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2 (LUGHA)**

**MUDA: SAA 2½**

**NAME…………………………………………………………………………………**

**SCHOOL…………………………………………………… SIGN…………………………..**

**INDEX NO………………………………………………… ADM NO……………………..**

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**Maagizo**

***(a)Andika*** *jina na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

***(b)****Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani*

***(c)*** *Jibu maswali yote.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 4 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| | | |

A. **UFAHAMU** **(alama 15)**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***

Ulikuwa usiku wa manane.Maria hatawahi kuyasahau yaliyotokea usiku huo na madhara yaliyoikumba aila yake;ambayo hadi wa leo huwasumbua na kuwafuata lika waendako na hata kuishi. Matokeo ya kitendo kilichotekelezwa na nduguye mnuna yamesalia kama dondandugu moyoni mwake.Yeye hujaribu kuyafutilia mbali lakini yanakataa katakata Kuondoka fuvuni mwake hasa anapomtazama nduguye mdogo.Tom,akitaabika bila miguu Maria alikuwa akidurusu somo la fizikia Abdallah,kakake mkubwa akimpa Tom Wosia"Tom, itakuwa bora ikiwa mtanena kwa amani na baba kuhusu tofauti zenu.

Hamna haja ya kumrushia chehche za matusi.Kumbuka kuwa heshima kwa mzazi ni taadhima kwa mterehemezi. Matokeo yake ni Baraka na **sudi** tele"Tom alikinai kuyatilia maanani mawaidha ya kaka yake.Akajitia hamnazo na kudai kuwa baba yake amemdunisha kwa mwia mrefu na angemfunza adabu.Watu wote katika familia walijaribu kumsihi lakini ikawa kazi bure.

"Upyaro haufai ndugu yangu .Hata kama una kimo kikubwa kuliko baba kumbuka kuwa ndiye mzazi aliyuekulea wewe', Alidokeza Maria

Baba yake Maria,Mugambi,alikuwa amechoshwa na vitendo vya mwanawe vya kutumia dawa za kulevya.Aghalabu Tom alikuwa akizua rabsha kila jioni baada ya kutoka shule. Mugambi alikuwa amemwadhibu mwanawe na hata kumshtaki katika kituo cha polisi lakini hakubalika.Watu walisema kuwa alikuwa na fedha nyingi kutokana la ulanguzi wa mihadarati. Jambo hili lilimwezesha kuhepa mitego ya askari kwa **kuzunguka mbuyu**. Tom akawa asiyesikia la mwadhini wala mteka maji msikitini.

"Mzee ninataka unipe urithi wangu, la sivyo, leo utaiona dunia hii paa!"Tom akamtisha baba yake. Mugambi akaja juu na kumwambia mwanawe kuwa umri wake haukutosha kupewa urithi. Ingembidi akamilishe masomo kwanza,ajijengee msingi bora wa maisha yake ya kesho na hata kupata mali yake mwenyewe." Mimi si mtoto. Ninataka uelewe kuwa leo ilikuwa siku yangu ya mwisho kuhudhuria shule. Hiyo elimu ya wakoloni imenichosha! Katu sisomi tena," Akasema Tom. Punde si punde Mugambi alipandwa na za mkizi na kumwandama mwanawe kwa makonde. Ikawa vurugu si vurugu **kuwamamanua** bila mafanikio. Licha ya kuumizwa na kujeruhiwa sehemu kadha za mwili wake,Tom alishikilia kikiki na kuendelea kupambana na baba yake. Mama yake alipoona maji yamezidi unga, aliamua kuingilia kati na liwe liwalo. Kwa bahati mbaya,Tom alimrushia teke la ubavuni na kumwangusha chini pu!

"Aghrr! haya yote unayotufanyia sisi wazazi wako yatakufuata daima''Magambi alilaani huku akigaragara sakafuni kwa maumivu tele"Ninataka uniue leo, siwezi kukulea kwa dhiki na taabu tele halafu unikosee mimi na mamako heshima namna hii utaona kilichomtoa kanga manyoya", Mugambi alimwambia mwanawe akiwa na uchungu mwingi moyoni majirani mimi nikiwemo walikuja kujionea sinema ya bure."Teresia ,unaona namna Tom alivyowakosea wazazi wangu heshima?'' Maria aliniuliza.''Kwa muda mrefu, familia yetu imekosa amani kwa sababu ya Tom kuzua fujo mara kwa mara. Amewajeruhi wazazi wangu mara nyingi huku akivivunjavunja

kenyekenye vyombo vya mama.Tandabelua anaozua Tom hunifanya mimi na ndugu zangu kutohudhuria shule wakati mwingine. Huwa tunahofia kuangamizwa kwa wazazi wetu, hivyo kubaki nyumbani kama walinzi wao. Tom amegeuka hayawani. Hajali habali,’’alinieleza Maria huku machozi yakimtiririka tiriri; njia mbilimbili. Nyumba yetu ilikuwa mita chache kutoka nyumbani kwa akina Maria. Nilikuwa wa kwanza kushuhudia Tom akiwatendea wazazi wake unyama pamoja na ndugu yake Abdallah. Alikuwa amewajeruhi vibaya. Abdallah alipojaribu kuwasaidia wavyele wake alirushiwa upanga uliompata barabara kwenye kisigino.Ninakumbuka namna Abdallah alivyochechemea kwa uchungu mwingi huku akiwa ameyauma meno.Ninakumbuka namna Abdallah alivyochechemea kwa uchungu mwingi huku akiwa ameyauma meno. ninakumbuka vyema

Kamsa alivyotawala nyumbani kwa mzee Mugambi.Watu wote walioshuhudia unyama wa Tom walilengwalengwa na machozi huku wakiulaani.Wanakijiji cha Umoja, waliamua kumpiga kitutu na kumfukuza. Alipotambua wamemzidi nguvu,alikimbia kiswara kuelekea upande wa chini. Kwa bahati mbaya, alianguka shimoni na kuvunjika miguu yote miwili. Aketipo na kudhukuru vitendo alivyokuwa akiifanyia familia yake, Tom hupatwa na mjuto makubwa. Leo ameamini kuwa majuto ni mjukuu.

**<u>Maswali</u>**

**(a)** Eleza msimamo wa Mugambi kuhusu kumpa mwanawe urithi **(alama 2)**

**(b)** Taja sababu kuu iliyomfanya Tom kutekeleza vitendo vya kinyama **( alama 1)**

**(c)** Eleza athari tano za watoto kutowatii wazazi wao kwa mujibu wa Taarifa hii **(alama 5)**

**(d)** Kwa nini Tom aliepuka mkono mrefu wa serikali? **(alama 1)**

**(e)** Fafanua wasifu wa Tom kulingana na taarifa hii **( alama 3)**

**(f)** Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa **(alama 3)**

***i.*** Sudi

***ii.*** kuzunguka mbuyu

***iii.*** kuwamamanua

**<u>SEHEMU B: UFUPISHO</u>** **(alama 15)**

Dhuluma kwa wanawake sio matokeo ya siasa baada ya uhuru,bali ni matokeo ya hali iliyokuwepo tangu enzi za mababu zetu;kabla ya ukoloni. Kubaguliwa na kudhulumiwa kwa wanawake kisiasa kunaoana na kunyonywa kwake kijamii kunakoshuhudiwa miaka nenda miaka rudi.

Elimu ya jadi alimwandaa mwanamke kuwa chombo kitiifu cha mwanamume. Mwanamke aliandaliwa katika unyago na katika mfumo mzima na malezi kuwa chombo cha kumtumikia mwanamume ,kumstarehesha, kumfariji,kumlisha na kumzalia watoto.

Mwanamke tangu jadi hakuruhusiwa kushiriki katika shughuli za kisiasa na utawala wala hakuna mtu aliyeamini kwamba mwanamke angeweza kushikilia wadhifa wowote wa uongozi.

Demokrasia ya jadi naihusudu sana; ambapo wazee walikaa chini ya mbuyu na kuamua mambo ya jumuiya. Mahakama ya kijiji ilikuwa aghalabu ni ya wazee na wanaume peke yao. Hakukuwa na mwanamke na mwanamke aliyeshirikishwa, hata kama alikuwa ajuza. Sifa waliyokuwa nayo wanawake ni ile ya usihiri na uganga.

Mwanamke yeyote aliyezeeka alidhaniwa kuwa bingwa na uchawi ,ulozi na ushirikina. Kwa hivyo,wanawake ndio waliokuwa washirika wakubwa, maana fursa ya kupata elimu pana zaidi hawakuwa nayo. Si ajabu kuwa mwanamke alipojitokeza na kusema jambo la busara, alipuuzwa na pengine kutukanwa hadharani

Kwa bahati nzuri, kumezuka mwamko uliotuingiza katika enzi mpya.Vita vya wanawake kujihami na kujiendeleza katika ulimwengu unaotawaliwa na wanaume vimetapakaa kote katika kila sehemu ya dunia.Wanawake wengi wamekiuka misingi na mizizi ya utamaduni na kung'oa asasi za kijamii na itikadi ambazo daima zimeendelea kupitishwa na umoja na mataifa mwaka hadi mwaka huku masuala ya wanawake ya kijamii,utu na utamaduni yakishangiliwa kupitishwa watetezi wameeleza wasiwasi wao ikiwa kupitishwa kwa maazimio kutasaidia kuleta maendeleo ya haraka kwa wanawake kimataifa au katika nch moja.Fauka ya hayo, baadhi ya wachunguzi wanaonelea kuwa maazimio mengi hayadokezi hatua za kufikiwa haki za wanawake.

Maazimio mengine yanazungumzia juu ya kuondolewa kwa ubaguzi dhidi ya wanawake kushiriki kwao katika uendelezaji wa amani ya kimataifa na ushirikiano wa kimataifa,majukumu yao katika jamii,mfuko wa umoja wa mataifa wa wanawake (unifem) na kuimarisha hadhi ya wanawake katika sekretariati ya umoja wa mataifa miongoni mwa shughuli nyingine katika mkabala huu.

Wanawake wameonyesha vipaji vyao katika nyanja mbalimbali za maisha; siasa,uchumi, utawala na kadhalika.Wanawake wamejikakamua na kudhihirisha kuwa wao pia wana jukumu muhimu la kutekeleza ili kuyaongoza maisha yao na ya watu wengine.

Wadumishaji wa dhuluma za kijinsia hawana budi kusalimu amri na kukubali ukweli huu wapende wasipende. Mtazamo juu ya haki sawa unatokana na kukubaliwa na kuondolewa kwa aina zote za ubaya dhidi ya wanawake. Kwa bahati mbaya,itikadi na mila za kiasili bado hazitupi nafasi ya kuwashangilia wanawake. Kwa bahati mbaya,itikadi na mila za kiasili bado hazitupi nafasi ya kuwashangilia wanawake wanaojitolea mhanga kutetea hadhi yao pamoja na ya wanyonge wengine. Wao huonekana kama waasi wapinga mila na matovu wa utii.

**Maswali**

**(a)** Bila kubadilisha maana asilia ,fupisha aya tatu za kwanza.(Maneno 50-50) (alama 5,1 utiririko)

**(b)** Kwa kurejelea aya tatu za mwisho ,pambanua hoja muhimu zinazogusiwa na mwandishi (maneno 70-80) (alama 8,1 utiririko)

**MATUMIZI YA LUGHA** **(Alama 40)**

**(a) Andika sauti zenye sifa zifuatazo:** **(alama 2)**

*i.* Kikwamizo sighuna cha kaakaa gumu……

*ii.* Kipasuo kwamizo cha kaakaa gumu……

*iii.* Irabu ya nyuma ,wastani………………

*iv.* Nazali ya kaakaa laini………….

**(b) Weka shadda katika neno lifuatalo ili itoe maana mbili tofauti** **(alama 2)**

walakini-

**(c)** Tunga sentensi **moja** ukitumia nomino katika ngeli ya U-YA pamoja na kivumishi kiashiria kisisitizi cha karibu **(alama 2)**

**(d)** Onyesha mofimu katika neno: aliyemcha **(alama 3)**

**(e) Kanusha sentensi ifuatayo** **(alama 1)**

Ukimpiga utashtakiwa na kuchukuliwa hatua kali

**(f) Andika sentensi ifuatayo kulingana na maagizo.** **(alama 1)**

Mwanafunzi huyo alipita kwa vile alisoma kwa bidii

Anza kwa nomino ya kitenzi jina

**(g) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha mishale** **(alama 3)**

**(h)** Mama na nyanya walinunuliwa jozi za viatu na baba

**(i) Andika sentensi ifuatayo kwa wingi**

Nikimuuliza ua hili ataweza kuifanya harusi yake iwe ya kupendeza **(alama 2)**

**(j) Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa:** **(alama 3)**

"Mito yetu imechafuka mno;itabiditushirikiane wakubwa kwa wadogo ,wamaume kwa wanawakeili tuisafishe''.Waziri wa Mazingira alituhimiza

**(k) Eleza matumizi ya 'ku' katika sentensi ifuatayo** **(alama 2)**

Hukumwelewa alivyoeleza namna ya kuwalisha mifugo

**(l) Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa** **(alama 2)**

Mtoto aliwaua nyoka kwa kuwapiga vichwa

(o) Tunga sentensi sahihi ukitumia kitenzi ‘la’ katika kauli ya kutendwa **(alama 2)**

(p) Andika kinyume cha sentensi **(alama 1)**

Watoto wameombwa waanike nguo

(q) Bainisha aina za virai vilivyopigiwa mistari **(alama 2)**

Ubaguzi wa kijinsia umekashifiwa na

Viongozi wenye msimamo thabiti

(r) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Angalilima kwa bidii angalivuna mavuno tele

(s) Tunga sentensi zenye vivumishi vya pekee vya kuonyesha dhana zifuatazo (i) umiliki **(alama 2)**

(ii) kutobagua

(t) Bumba ni kwa nyuki ni kwa samaki _____ **(alama1)**

**(m) Bainisha aina za shamirisho katika sentensi ifuatayo** (alama 3)

Baba yake alivamiwa na wezi waliomvunjia mlango kwa chuma

**(n)** Kwa kutunga sentensi eleza matumizi mawili ya mkato **(alama 2)**

**(o)** Eleza maana mbili za sentensi hii: **(alama 2)**

Mamake Juma na Maria walitutembelea

ni kwa siafu

## <u>ISIMUJAMII</u> <u>(ALAMA 10)</u>

**(a)** Eleza sifa **tano** za lugha rasmi **(alama 5)**

**(b)** Eleza mambo **matano** yaliyochangia katika maenezi ya Kiswahili katika **(alama 5)**

**(c)** Afrika Mashariki kabla ya uhuru

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 7

**102/3**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 3 (fasihi)**

**MUDA: SAA 2½**

**NAME……………………………………………………………………………………**

**SCHOOL…………………………………………… SIGN…………………………**

**INDEX NO………………………………………… ADM NO……………………**

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

**a)** *Andika jina lako, nambari ya usajili, mkondo, sahihi na tarehe katika nafasi ulizoachiwa.*
**b)** *Jibu maswali* ***manne*** *pekee.*
**c)** *Swali la kwanza ni la* ***lazima****.*
**d)** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Fasihi Simulizi.*
**e)** *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
**f)** ***Maswali yote ni sharti yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.***

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

**SEHEMU YA A: USHAIRI : LAZIMA**

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali:**

Binadamu hatosheki, ni kiumbe chenye zani, kweli mja hapendeki, Kwa kweli haaminiki, hila ameficha ndani, la wazi ni unafiki Ukweliwe haafiki, njama zake zi moyoni, usimwone ni rafiki
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Wengine watakuua, wakiona una pesa, hata zikiwa kidogo, Hizo kwao ni maua, hupupiwa zikatesa, wakazifuata nyago, Hadi kwenye wako ua, pasipo hata kupesa, wala kukupa kisogo, Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka

Pindi kinunua kitu, hafurahi Shaitani, bali tajawa chukizo, Mtu kiwa mtukutu, tanuna mtimani, kwalo lako tekelezo, Tamko lake 'Subutu' Kuondoa tumaini, na kukuulia wazo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Aliye na taraghani, taabu kuishi naye, kazi yake kujidai, Takusema faraghani, asosema kiwa naye, kupendeza maadui, Hana faida nyumbani,ni mtu akuchimbaye, mradi usitumai, Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Kwa hakika ni balaa, kumkirimu mchawi, aliyejaa uchoyo, Bahati ina hadaa, kukupa alo sadawi, aibatili rohoyo,
Mipangoyo kwake jaa, na nia ya ustawi, huwiza kuvunja kaninyo, Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Ninacho changu kilio, ninalia sanasana, kinyesi nimetupiwa, Ningetoa azimio, lakini uwezo sina, kwa matatizo kuambiwa, Ama nitumie mbio, fuadini ninanena, akilini nazuiwa,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

**MASWALI:**

**a)** Lipe shairi hili anwani mwafaka **(alama1)**

**b)** Fafanua mambo **manne** ambayo nafsineni analalamikia **(alama4)**

**c)** Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo: **(alama3)**

(i) Idadi ya vipande katika kila mshororo

(ii) Mpangilio wa vina katika kila ubeti

(iii) Idadi ya mishororo katika kila ubeti

**d)** Andika ubeti wa **nne** katika lugha nathari **(alama3)**

**e)** Bainisha tamathali **mbili** za usemi zilizotumiwa katika shairi hili **(alama2)**

**f)** Huku ukitoa mifano, onyesha mbinu **mbili** alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi **(alama2)**

**g)** Andika aina **mbili** za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili **(alama2)**

**h)** Fafanua muundo wa ubeti wa **tano** **(alama3)**

**SEHEMU YA B:**

**TAMTHILIA T.M Arege: Bembea ya Maisha Jibu swali la 2 au la 3.**

**2.** "Hayo ni ya kale ... na ya kale hayanuki. Wengi hawafuati tena mila hizo. Walimwengu sasa wanavaa sare moja."

**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama4)**

**b)** Fafanua tamathali mbili za usemi zilizotumika katika dondoo hili. (**alama2)**

**c)** Eleza sifa za mzungumzaji wa kauli hii. **(alama5)**

**d)** Jadili maudhui ya utamaduni kama yanavyojitokeza katika Tamthilia nzima. (**alama9)**

**3.** "...Hebu fikiri! umepata ajali mbaya. Inakuacha mahututi. Anapita mtu katika gari lake. Kwa Imani anaguswa. Anakufanyia mpango wa Flying Doctors, ndege inafika inakupeleka hospitali. Mwenyewe huyo anakulipia kila kitu! Mtu huyo atakosaje kuwa zawadi kwako?"

**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. **(al.4)**

**b)** Tambua umuhimu wa mbinu zozote mbili za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili. **(al.4)**

**c)** Eleza umuhimu wa anayerejelewa katika dondoo hili**.** **(al.4)**

**d)** Kwa kutoa hoja zozote nane kutoka kwa tamthilia nzima. Eleza ukweli wa kauli, 'mtu huyo atakosaje kuwa zawadi kwako?' **(al.8)**

**<u>SEHEMU C: Hadithi Fupi – Mapambazuko ya Machweo</u> Jibu swali la 4 au 5**

**4.** ***(a) Mzimu wa kipwerere-Yussuf Shoka***

"Siku iliyofuata, majira ya magharibi pevu, nilifika pale mzimuni. Kama ilivyo ada yangu, nilivaa guo jeupe lililonifunika gubigubi kama maiti. nikaangalia huku na huko, sikuona mtu. Hapo nikasogea karibu zaidi na ule mzimu. Nilipofika nikauimba ule wimbo wote.

Nilipomaliza tu nikajitoma kichakani mle bila hofu wala kimeme…nilichokiona humo, sikuamini macho yangu! <u>Mle ndani ya mzimu mlikuwa na makanda na makasha ya</u> <u>tumbaku, unga wa kilevi na bangi</u> <u>kwenye marobota. Kulikuwa na mapipa ya chang'aa na</u> <u>tembo ya mnazi</u>. Humo pia, mlikuwa na kitanda cha besera kilichotandikwa vizuri. Juu ya kitanda hicho, palitupiwatupiwa asumini na maua ya mlangilangi.."

**a)** Eleza aina za taswira katika kifungu hiki **(alama 4)**

**b)** Ukirejelea hadithi ya ***" Mzimu wa Kipwerere***," Fafanua jinsi imani katika mambo ya kichawi yamejikita katika jamii**.** **(al 6)**

**c)** Katika hadithi ya **Msiba wa kujitakia na D.W.Lutomia** athari za uteuzi mbaya wa viongozi zinaoenkana wazi. Zitambue**.** **(alama 10)**

***SABINA-Winnie Nyaruri***

**5.** "Mike! Mike! Mike! Njoo! Nilijua utafanya vyema mwanangu…"

**(a)** Tambua na ueleze **toni** ya dondoo hili. **(alama 2)**

**(b)** Changanua mtindo katika dondoo hili. **(alama 2)**

**(c)** Eleza sifa **nne** za msemaji wa dondoo hili. **(alama 4)**

**(d)** Eleza mbinu **mbili** ulizozitumia kutambua sifa za msemaji wa dondoo hili. **(alama 4)**

**(e)** Tambua na ufafanue madhila yanayomsakama mhusika mkuu katika hadithi hii ya *"Sabina"*.

**(alama 8)**

**<u>SEHEMU YA D: NGUU ZA JADI-CLARA MOMANYI</u>**

**<u>Jibu swali la 6 au 7</u>**

**6. Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali;**

**'au amekuja hapa kwa sababu za kibiashara. Kifo cha panzi furaha ya kunguru ati. Mnajua anakiwanda cha sharubati? Kesho mtamuona ameagiza vinywaji mbalimbali viletwe hapa muuziwe. Huenda hata akafungua kijiduka uchwara hapa.'**

**a)** Weka maneno haya kwenye muktadha wake. (**alama 4)**

**b)** Kwa kutumia mifano minne, jadili mtindo wa dondoo hili. (**Alama 8)**

**c)** Tathmini umuhimu wa mandhari ya dondoo hili. (**Alama 8)**

**7. '**Mwanamke ni mhusika mkuu katika kuibomoa jamii yake.' **Jadili.** **(Al20)**

**SEHEMU E : FASIHI SIMULIZI**

**8.** Niaje wazungu wanaweza kutunza vitu vikajaa kwenye friji. Yani nimeweka soda mbili tu kweye friji lakini akili haitulii hadi nizinywe. Niko sebuleni nazunguka tu. Najaribu kuwaza vitu vingine lakini wapi akili inaniambia 'My friend, kunywa soda.'

**a)** Bainisha kipera cha utungo huu **(alama2)**

**b)** Utanzu wa kipera hiki huweza kuchukua nafasi muhimu katika fasihi simulizi. Thibitisha kwa kurejelea hoja zozote sita **(alama6)**

**c)** Ufanisi wa uwasilishaji wa utanzu huu unategemea fanani. Tetea kauli hii. **(alama6)**

**d)** Ni changamoto zipi zinaweza kumkabili mwanafasihi mtafiti nyanjani? **(alama6)**

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 8

**102/1**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 1 (INSHA)**

**MUDA: SAA 1¾**

**NAME**………………………………………………………………………………………

**SCHOOL**……………………………………………… **SIGN**…………………………

**INDEX NO**…………………………………………… **ADM NO**……………………

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

## MAAGIZO

- ***a)*** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
- ***b)*** *Andika insha **mbili**. Insha ya **kwanza** ni ya **lazima.***
- ***c)*** *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya tatu zilizobakia.*
- ***d)*** *Kila insha isipungue maneno **400***
- ***e)*** *Kila insha ina alama **20***

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 40 | |

**MASWALI**

**1. LAZIMA**

Andika insha ya wasifu wa kiongozi umpendaye

**2.** Mitandao ya kijamii ina faida nyingi kuliko hasara. Jadili

**3.** Andika kisa kitakachodhinirisha maana ya

Methali: Ukiona vyaelea jua vimeundwa

**4.** Andika insha itakayoishia kwa maneno yafuatayo**…….**nilipomtazama namna alivyojikunyata, ndipo nilipotanabahi kuwa mtoto wa kiume ametelekezwa.

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 8

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2 (LUGHA)**

**MUDA: SAA 2½**

**NAME**………………………………………………………………………………………

**SCHOOL**……………………………………………… **SIGN**…………………………

**INDEX NO**…………………………………………… **ADM NO**……………………

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**Maagizo**

***(a)Andika*** *jina na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

***(b)****Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani*

***(c)*** *Jibu maswali yote.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 4 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| | | |

**UFAHAMU** **(Alama 15)**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***

Basi huu ni mwanzo tu.*Mwanzo wa ngoma ni lele*. Huu ni mwanzo wa safari ndefu.Itatuchukua miaka na mikaka.Lakini msiwe na papara,Sharti mwanzo tutanabahi twaelekea wapi ndipo tuamue tutasafirije.Tahadhari na hatari ya hasira visasi na papara pamoja na maradhi yanayozidi yote,yaani maradhi ya matumaini yanayozidi uhalisi.Matumaini yaliyopindukia ndiyo huwalewesha watu wakadhani watapata afueni wakizifuata pepo za siasa za chama kimoja au siasa za vyama vingi.mfumo wa soko huria au mfumo wa ukiritimba,mfumo wa utandawazi au mfumo wa kibepari, utawala wa kidikteta au utawala wa kidemokrasia na udini, ujamaa na ukomunisti na kadhalika.Hatari kabisa hii ya kujenga nyumba kwa karata.Nasema tena, tahadhari na ulevi wa ushindi.Mimi nashauri hivi;hatua ya kwanza ni elimu si elimu ya shahada na stashahada zipatikanazo vyuoni. Elimu ya kujielewa sisi nani twatoka wapi, twaelekea wapi na utu tutaurejeshaje pahali pake mahsusi toka kule mwituni kwa wanyama

Ulikotokomelea''.Amani awe mtemi!'' umati ukadai Hapana.Hata kidogo.Badala yake acha amani iwe na mtemi mpya msinivishe joho ambalo si makamo yangu kulivaa'',aliwaambia.''Kaeni mfikirie vema juu ya mustakabali wenu.Nilichodhamiria mimi ni kushirikiana na ndugu yangu madhubuti kumnyonyoa kipungu mmoja,ila sikutaka niingie pahala pake niruke juu nikijihadaa kwamba nitafika mbinguni.

Ila msikubali dhuluma.Dhuluma msikubali, Ikija dhuluma tena, msimlaumu mtu mwingine, Jilaumuni wenyewe. Nakumbusha tu ya kwamba kuwepo mamlakini kwa mtemi Nasaba bora muda wote huo si kosa lake tu.Alisema Amani.Ni kosa letu sote.Tulimruhusu sisi wenyewe kwa kimya chetu,kwa kukubali dhuluma zake na udhalili wetu.hatuwezi kumlaumu peke yake.Kwa kila mtawala katili kuna umma uliomruhusu ama kampa uwezo wa kutekeleza ukatili wake.

Punde si punde mkutano ukesha watu wakafumukana wakiwa wamestaajabu

Amani alisadiki kwamba toba ya mwalimu majisifu ilitosha.Amani alijambia mwenyewe kwamba mkono uliondika kidagaa kimemwozea ungeanidia riwaya tena na tena tamthilia na nudhuma na hadithi fupi mpaka maktaba zijae zitapike.Mwenyewe Mwalimu Majisifu alilewa chopi zaidi kuliko mwanzo,hadi siku yake ya mauko ila katika kulewa na kuleuka,akawa hawaoni tena watoto wake walemavu kama masimbi na mashata au laana kwa kosa lolote la mkewe au lake mwenyewe ama la watoto wenyewe.

''Hakuna jambo muhimu sasa kama wanangu wapendwa",alipita akiimbaimba akishauchapa na kuwaza vivyo hivyo alipoleuka

"Hatuwezi kuwa binadamu endapo hatuoni walemavu kama wenzetu.tuktakuwa tumelemaa ulemavu mbaya zaidi kuliko ulemavu". Kauli hii ilikuwa tokeo la funzo alilojifunza mwalimu majisifu kutokana na amali na kalima za imani kuwaelekea watoto wake walemavu.

***(Imenulikuliwa kutoka kwa riwaya ya kidagaa kimemwozea- Ken Walibora)***

**MASWALI**

**(a)** Kulingana na taarifa ni nini kinachochea dhuluma katika jamii **( alama 2)**

**(b)** Eleza mabadiliko yaliyotokea katika maisha ya mwalimu majisifu **( alama 2)**

**(c)** Taja changamoto ambayo walemavu hupitia katika jamii **(alama 2)**

**(d)** Ni nini maana ya mwanzo wa ngoma ni lele' Ukirejelea kufungu hiki **( alama 2)**

**(e)** Fafanua mwelekeo uliostahili kuchukuliwa ili kutimiza ndoto zao kama ilivyo katika taarifa **( alama 4)**

**(f)** Eleza maana ya **( alama 3)**

**(i)** waombolezaji wa kuhesabu

**(ii)** ukiritimba

**(iii)** kumnyonyoa kipungu

**UFUPISHO** **(ALAMA 15)**

***Soma taalifa kisha ujibu maswali yanayofuata***

Tangu mwaka huu uanze,kumekuwa na ongezeko la visa vya watu kupatikana wakiwa na pesa zinazoshukiwa kuwa bandia. Mwezi jana,polisi katika eneo la Ruiru kaunti ya Kiambu walinasa kwenye nyumba moja pesa bandia za thamani ya 32 bilioni. Pesa hizo zilikuwa mchanganyiko wa dola, Pauni na za Kenya na zilikuwa.pesa hizo zilikuwa zimeingizwa katika masanduku 20 ya mabati.Tayari washukiwa walifikishwa mahakanani kuhusiana na tukio hilo.

Siku chache baadaye polisi wamepata pesa nyingine bandia zikiwa zimehifadhiwa kwenye kasha salama ndani ya benki ya Barclays.

Polisi wanasema mteja wa benki hiyo tawi la Queens way jijini Nairobi, aliingiza pesa hizo pia zikiwa za kigeni,zenye thanani ya Sh. 2 bilioni. Awali polisi wa kitengo cha Flying Squad na wenzao wa kupeleleza uhalifu (DCI) walikuwa wamekisia kiwango cha pesa kuwa Sh. 17 bilioni vyovyote iwavyo, pesa hizi ni nyingi mno kuwa zinaweza kuwa mikononi mwa watu.kusambaa kwa pesa bandia,kunaashiria kuwa humu nchini,kuna watu ambao wana viwanda vya kutengeza fedha hizo na kuna uwezekano mkubwa kwamba baadhi ya wananchi wanazitumia bila ya kuwa na habari.

Kusambaa kwa pesa nyingi kunatukumbusha mwaka 1992 wakati aliyekuwa kiongozi wa vijana wa chama cha kanu, alipokuwa akisambaza pesa kana kwamba alikuwa na kiwanda chake. Ni wakati huo ambapo noti ya Sh. 500 ilitolewa kwa mara ya kwanza.

Lakini matokeo yake ni kuwa uchumi wa nchi ulisambaratika wakati huo. Baada ya uchaguzi mkuu wa 1992 ambao Rais Daniel Arap Moi alishinda tena, nchi ilijikuta ikipitia kipindi kigumu cha kiuchumi.

Kusambaa kwa pesa bandia wakati huu ambapo Kenya inakubwa na madeni makubwa, ni hatari kwa uchumi wetu. Pesa zinaposambaa kwa wingi katika nchi, zinapoteza thamani yake na kufanya kila bidhaa na huduma kuwa ghali tukiendelea kuruhusu wahuni wachache wachapishe pesa za ziada na kizitumia kwenye soko letu tutakuwa tumeidhinisha kuporomoka kwa uchumi ambao tayari uko katika hali isiyoridhisha

Polisi wanaochunguza wana wajibu wa kutambua chanzo cha pesa hizo na kukikomesha kabisa.Nchi yetu inahitaji kuimarisha uchumi wake ili wananchi wanufaike kwa jasho lao na wala si kuruhusu watu wachache watuangamize kwa kutafuta utajiri kwa njia za mkato.

***(imenukuliwa kutoka kwa Taifa leo tarehe 20/3/2019).***

**(a)** Fupisha ujumbe wa aya **tatu** za mwanzo kwa maneno 70- 80 (alama 8,1 mtiririko) Matayarisho

**c)** Kwa kutumia maneno 60-70,bainisha mambo muhimu yanayotokea katika aya **tatu** za mwisho matayarisho

**3. MATUMIZI YA LUGHA** **(Alama 40)**

**(a)** Tunga sentensi iliyo na muundo ufuatao **(alama3)**

I + N+V+$T_S$ +T+E

**(b)(**i) Eleza maana ya silabi **(alama 1)**

**(iii)** Andika neno lenye muundo ufuatao wa silabi-konsonanti + irabu + konsonanti + irabu **(alama 1)**

**(c)** Eleza sifa mbili mbili za sauti zifuatazo **( alama 2)**

(i) /o/

(ii) /f/

**(d)** Andika visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari **( alama 1)**

Maghulama wale walishiliki katika Kinyang'anyiro hicho kwa ustadi

**(e)** Tunga sentensi tatu kuonyesha matumizi ya neno 'kimya' kama: **( alama 3)**

(i) Kielezi

(ii) Nomino

(iii)Kitenzi

**(f)** Huku ukitolea mifano onyesha matumizi matatu ya alama hisi katika lugha **(!)** **( alama 3)**

**(g)** Eleza matumizi mawili ya kiambishi 'ji' **( alama 2)**

(ii) Tunga sentensi moja kuonyesha moja ya matumizi hayo **( alama 1)**

**(h)** Changanua sentensi ifuatayo kwa jedwali **( alama 4)**

Mwanasiasa anahutubia wananchi huku wakimshangilia

**(i)** Andika wingi wa sentensi ifuatayo **( alama 2)**

Yeye ndiye mkulima bora atakayetuzwa na katibu mkuu wa kilimo

**(j)** Tumia kiwakilishi kisisitizi cha mbali sana na nomino katika ngeli ya U-ZI kutunga sentensi **( alama 2)**

(l) Bainisha mofimu katika neno "lililopikwa' **( alama 3)**

**(l)** Andika katika msemo wa taarifa **(alama 2**)

"Sara!Sara!" Mama aliita kwa hasira

**(m)** Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo: Japo wageni walikuwa wengi waliweza kuwatumbuiza **( alama 2)**

**(n)** Andika udogo wa sentensi **( alama 2)**

Paka alirukia mfupa uliorushiwa kwa dirisha

**(o)** Yakinisha sentensi ifuatayo **(alama 2)**

Usipofanya kazi hiyo kwa bisii hutafanikiwa

**(p)** Eleza matumizi ya 'ka' sentensi ifuatayo **( alama 1)**

(i)Tuliamka, tukaoga, tukasali,kisha tukaanza safari

**q**) Bainisha kiarifu katika sentensi **( alama 2)**

Mwalimu wao aliwafunza vizuri

4. **ISIMU JAMII** **(Alama 10)**

**(a)** Eleza namna kaida zifuazo zinavyoathiri matumizi ya lugha katika jamii **(alama 4** )

***(i)*** uhusiano

***(ii)*** malezi

**(b)** Eleza majukumu **mawili** ya lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa katika nchi ya Kenya **( alama2)**

**(c)** Taja sifa **nne** zinazotambulisha sajili ya hospitali

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 8

**102/3**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 3 (fasihi)**

**MUDA: SAA 2½**

NAME…………………………………………………………………………………

SCHOOL……………………………………………… SIGN…………………………

INDEX NO…………………………………………… ADM NO……………………

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

- *a) Andika jina lako, nambari ya usajili, mkondo, sahihi na tarehe katika nafasi ulizoachiwa.*
- *b) Jibu maswali **manne** pekee.*
- *c) Swali la kwanza ni la **lazima**.*
- *d) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Fasihi Simulizi.*
- *e) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
- f) ***Maswali yote ni sharti yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.***

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

**SEHEMU A : FASIHI SIMULIZI**

**1**. lazima

(a) Miviga ni nini? **alama2)**

b) Eleza sifa **tano** za Miviga **alama 5)**

c) Fafanua hasara **tatu** za miviga **alama 3)**

(d) Eleza changamoto **tano** ambazo mtafiti hukabiliana nazo anpokusanya data ya miviga **(alama 10)**

**SEHEMU B:**

**TAMTHLIA – BEMBEA YA MAISHA**

**2.** Ulevi. Ulevi mwanangu! Gongo liliyamega maadili yake kimyakimya na taratibu uwajibikaji ukawa umemponyoka na kuteleza kama sabuni ya povu jingi na kumwacha na kisomo chake tu.

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

b) Fafanua mbinu **nne** za kimtindo zilizotumiwa katika dondoo hili. **(alama4)**

c) Eleza sifa **nne** za anayerejelewa . **(alama 4)**

d) Jadili umuhimu wa mandhari ya mazungumzo haya. **(alama8)**

***au***

**3.** a)Mwandishi wa tamthilia ya Bembea amefaulu kuchora mpaka uliopo kati ya usasa na ukale.Jadili kwa kutoa hoja **kumi.** **(alama 10)**

b)Kuishi mijini kuna adha chungu nzima.Jadili kwa kurejelea tamthilia nzima. **(alama 10)**

**SEHEMU YA C: USHAIRI**

**4.B.** Moyo wanambia imba,dikteta simwimbie
Moyo wanambia lumba,muhitaji mlumbie
Moyo wanambia chimba,maovu uyachimbue
Moyo wanambia woga,ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia kuwa,ila kasuku usiwe
Moyo wanambia iwa,kunguni ila usiwe
Moyo wanambia pewa,cha mnyonge usipewe
Moyo wanambia woga,ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia nenda,penye dhuluma senende
Moyo aanambia penda,mnyonyaji simpende
Moyo wanambia ponda,ateswaye simponde
Moyo wanambia woga,ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia tenda,lenye jamala litende
Moyo wanambia unda,lenye faida liunde
Moyo wanambia tunda,lisilo sumu litunde
Moyo wanambia woga,ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia ota,kuwa mwizi usiote
Moyo wanambia kata,marija yote ikate
Moyo wanambia teta,penye dhuluma patete
Moyo wanambia woga,ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia nyosha,penye na kombo panyoshe
Moyo wanambia usha,mateso yote yaushe
Moyo wanambia isha,yenye majonzi yaishe
Moyo wanambia woga,ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia waza,yalopita yawazie
Moyo wanambia kaza,mwovu njia mkazie
Moyo wanambia vuaza,lenye heri tuvyazie
Moyo wanambia woga,ndio mwazo wa maafa

***(Shairi la mbegu la E. Kezilahabi, 1988)***

**MASWALI**

**(a)** Fafanua dhamira ya mtunzi wa shairi hili **( alama 2)**

**(b)** Ainisha bahari za ushauri huu kwa kutegemea

*(i)* Mpangilio wa maneno

*(ii)* Vipande vya mishororo

*(iii)* Idadi ya mishororo kwa kila ubeti **( alama3)**

**(c)** Tambua aina **moja** ya urudiaji na utolee mfano **( alama 2)**

**(d)** changua muundo wa shairi hili **( alama 4)**

**(e)** Andika ubeti wa **tano** kwa lugha ya nathari **( alama 4)**

**(f)** Onyesha aina **moja** ya uhuru wa kishairi aliotumia mwandishi katika shairi lake **(alama 2)**

**(g)** Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika ushairi **(alama 2)**

**(i)** Dikteka

**(ii)** Kasuku

**(iii)** Mnyonyaji

**5.USHAIRI**

Ni mimi nizamishaye chini Mizizi kwenye majabali Kufyonza chumvi!

Ni mimi ninyunyizae maji
Ili mimea ifumbue
Nafasi zao hewani
Ili miti ishike mimba kuzaa
Matunda,nafaka,mizizi na viazi Ela mimi sili hata punje moja Nabaki mtupu!

Ni mimi tumbo kubwa,
Niliyeshiba madini
Ni mimi ninayechimba
Kupakua raslimali

Dhahabu,chuma,makaa… ela yote yanaona Yatiririka kwao!
Nabaki mtupu!

Vyakula vyote nazalisha mimi Na mi' nabaki na njaa!

Nguo zote nawapa mimi Na mi'nabaki u tupu!

Madini yote nawapa mimi
Na mi'nabaki kununua vyao!

Kazi zote nafanya mimi Wao wabaki kunila nguvu!

Wao wanajita bora
Na mi' nabaki fukara!

***( Shairi la S.A Mohamed Jicho la ndani, Longhorn Publishers 2002)***

**MASWALI**

**(a)** Lipatie shairi hili anwani mwafaka **( alama 2)**

**(b)** Fafanua aina moja ya taswira katika shairi hili **( alama 2)**

**(c)** Eleza ujumbe mkuu wa mtunzi wa shairi hili **(alama 2)**

**(d)** Huu ni ushairi wa aina gani.Toa sababu ya jibu lako **(alama 2)**

**(e)** Eleza toni ya ushairi **(alama 2)**

**(f)** Mtunzi ametumia mbinu zipi kukuza ujumbe wake **( alama 4)**

**(g)** Huku ukitolea mifano onyesha matumizi ya mistari mishata katika shairi hili **( alama 2)**

**(h)** Onyesha umuhimu wa kinaya katika shairi hili **(alama 2)**

**(i)** Tambua nafsineni katika shairi hili **(alama 2)**

**SEHEMU D:**

***Hadithi fupi (MAPAMBAZUKO YA MACHWEO na Hadithi Nyingine)***

**D.Lutomia na Phibbian Muthama:** *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine.*

**6.(a)** 'Nipe Nafasi"

Baridi ilizidi kututafuna kadri tulivyokazana kupanda Milima ya Maloti. Vidole vyangu vya miguuni vilikufa ganzi. Mashavu yetu yaliadhibika kwa upepo baridi huku vipande vya theluji vikitupiga kwenye nyuso zetu.Miili yetu iliathirika;tulihisi njaa na uchovu. Nikatamani tufike kwa jamaa ya baba yetu ambako tungepata angalau mchuzi wa papa kabla ya kulala. Bidii ya mama ilitutia moyo wa kuendelea na safari.

(i) Tambua nafsi ya usimulizi iliyotumika katika hadithi hii na uthibitishe jibu **lako. (alama 2)**

ii) Eleza umuhimu wa mwandishi kutumia nafsi uliyotaja hapo(i) juu. **(alama 2**

iii) Bainisha mbinu mbili za kimtindo zilizotumika katika dondoo hili **(alam 2)**

iv) "Mamake Msimulizi (Richman) ni kielelezo cha wanawake jasiri""Thibitisha kwa kutolea mifano mwafaka **(alama 7)**

b) Hadithi "Toba ya Kalia" inahimiza uwajibikaji. Jadili. **(alama 7)**

**AU**

**D.Lutomia na Phibbian Muthama:** *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

8***.Fadhila za Punda***

Alipozidiwa akapoteza fahamu.Fahamu zilipomrudia,maumivu yakamvamia.Mumewe hakuonekana,amejiendea na kumwaacha afilie mbali.Alilia machozi yakamwisha.

a)Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

b)Taja mbinu **mbili** za lugha zilizotumika katika dondoo hili. **(alama 4)**

c)Fafanua mbinu **nne** za kutambua sifa za mhusika anayerejelewa. **(alama 4)**

d)Kwa kurejelea hadithi "Fadhila za punda" onyesha kwa hoja **nane** ufaafu wa mdokezo wa methali ufuatao: ***maskini akipata makalio hulia bwata*** kwa kutolea mifano mwafaka hadithini. **(alama 8)**

**<u>SEHEMU YA E:</u>**

**SEHEMU C: RIWAYA**

**Clara Momanyi: Nguu za Jadi**

**Jibu swali la 4 au 5**

**4. Hakujua** akimbilie wapi.Sasa afanye nini?Alilitupia lile jinyama lakini likahepa.Alihisi maisha yake yamo hatarini.

a) Yaweke maneno haya katika muktadha wake. **(alama 4)**

b) Kwa kutoa mfano,tambua mbinu mbili za lugha katika dondoo hili **(alama2)**

c) Fafanua umuhimu wa mandhari katika riwaya hii. **(alama 6)**

d) Jamii ya nchi ya Matuo imesheheni vikwazo ambavyo vinakaa kama nguu,na kutoka jadi nguu hizi zimeathiri kwa upana usawa katika jamii.Tathmini kauli hii kwa hoja **sita.** **(alama 6)**

**7.** Hivyo,alitaka kubadili hali hata kama ilimaanisha kukitia kichwa chake kinywani mwa simba. <u>Alitaka kuliokoa jahazi lililokuwa likielekea mwambani kwa kasi.</u> Lakini angeliweza vipi kupambana na utandu wa mahasidi hao?

**a)**Fafanua umuhimu wa anayerejelewa dondooni katika kukuza na kuendeleza vitushi riwayani. **(alama 4)**

b) Eleza sababu za mrejelewa kutaka kufaulisha kauli iloyopigiwa mstari. **(alama 10)**

**c)** Mwandishi wa riwaya ya Nguu za Jadi amefanikiwa kutumia **mbinu ya majazi** katika kukuza wahusika na mandhari mbalimbali riwayani.Fafanua kwa kutolea mifano **sita**. **(alama 6)**

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 9

**102/1**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 1 (INSHA)**

**MUDA: SAA 1¾**

**NAME**…………………………………………………………………………………

**SCHOOL**…………………………………………… **SIGN**…………………………

**INDEX NO**………………………………………… **ADM NO**……………………

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

***a)*** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

***b)*** *Andika insha **mbili**. Insha ya **kwanza** ni ya **lazima.***

***c)*** *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya tatu zilizobakia.*

***d)*** *Kila insha isipungue maneno **400***

***e)*** *Kila insha ina alama **20***

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 40 | |

**SWALI LA LAZIMA**

**1.** Wewe ni mtafiti wa maswala ya usalama nchini. Mwandikie barua Waziri wa Usalama wa Ndani barua ukimweleza sababu za wanafunzi wa shule za upili kujiunga na makundi ya wanamgambo, almaarufu Al Shabaab.

**CHAGUA MOJA:**

**2.** Utandawazi una athari mbaya katika maisha ya vijana. Jadili.

**3.** Andika insha inayodhihirisha maana ya 'Umdhaniye ndiye siye'

**4.** Kamilisha insha yako kwa maneno:

**...**Sitaisahau siku hiyo kwani sijawahi kufedheheka kama nilivyoaibika siku hiyo.

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 9

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2 (LUGHA)**

**MUDA: SAA 2½**

**NAME……………………………………………………………………………………**

**SCHOOL……………………………………………… SIGN…………………………**

**INDEX NO…………………………………………… ADM NO……………………**

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**Maagizo**

***(a)Andika*** *jina na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

***(b)****Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani*

***(c)*** *Jibu maswali yote.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 4 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| | | |

**1. UFAHAMU** **ALAMA15**

**Shule yangu ya upili**

Majio yangu katika shule hii ya upili hayakutokea kwa bahati nasibu bali kwa mipango kabambe niliyoianza tangu nikiwa shule ya vichekechea. Nikiwa sitetereki hata kwa wazazi wangu waliponisihi nijiunge na shule nyingine za karibu nikawa sisikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini. Nikawa na ragba ya mkanja nikingoja siku ya kujiunga na shule yenyewe. Kweli majuto ni mjukuu na huja kinyume.

Nilizaliwa katika aila yenye nafasi iliyotopea na kubobea katika ukwasi uliodhihirika kutokana na mitaa tulikoselelea kwa muda kabla ya baba kuaamua kununua nyumba yake mwenyewe huko upande wa Karen hivyo tukagura kutoka Runda. Wakati wa likizo tukawa tunaruka hadi pwani ambako mama yangu alikuwa amemiliki jumba lililokuwa katika ufuo wa bahari lililojengwa katika kipande kisichopungua ekari tatu alilotunukiwa wakati wa nikahi yao na wakwe wa baba yangu.

Wavyele wangu wakawa wanaendesha magari meusi ya kifahari ingawa sikuwahi kumwona mama akichangamka kuendesha magari yake ya maana, kila macheo ya siku za kazi gari lililoendeshwa na dereva ambaye alimstahi mama hadi akawa anamfungulia mlango wa gari na kuufunga baada ya mama kujitoma katika tumbo la gari lilimjia na kumrejesha kwa wakati. Nikajiunga na shule ya msingi ya kibinafsi ambako nilishughulikiwa kama kikembe. Wengi wa wale tuliosoma nao walikuwa wa tabaka langu na walikuwa wametoka katika kila sehemu nchini Kenya.

Hayawi hayawi huwa na siku ya kuripoti ikafika. Alfajiri, dereva mmoja akatumwa kwenda hadi Kisumu ili atulaki na kutusafirisha kutoka uwanja wa ndege hadi shule ya upili ambayo ilikuwa yangu ya rohoni. Nasi tukaelekea hadi uwanja wa ndege ili turuke hadi Kisumu. Safari yetu kutoka kitongoji cha kifahari hadi Airport ilikuwa njema, safari yetu tulipoabiri ndege ilikuwa bila bughudha, safari yetu kutoka Kisumu mjini haikuwa na kasoro na tulienda kulingana na mpango. Safari yetu ilikuwa mufti hadi tulipofika katika lango la shule ya kitaifa! Tulipotia ozi tu!!....jamani......jamani nikafa moyo. Labda mama aliweza kubaini mabadiliko ya hisia zangu, nilitamauka, nikawa mchege na kusema kweli niliyoyaona sikuamini. Mvua iliyokuwa imepasua hapo awali ilikuwa imeacha vitua vya maji kwenye vijia vya kutembea vilivyochakaa na kubomoka bila yeyote kujali kuvikarabati. Majengo yalikuwa makongwe yaliyojengwa miaka mia moja iliyopita na yalistahili kuitwa makafadhi badala ya pahali pa kumkaribishia mwanafunzi aliyepita kwa alama mia nne na thelathini na tano. Asiye na wake ana Mungu, nikapiga moyo konde lazima nisajiliwe katika shule ya ndoto langu. Ningewezaje kughairi wazo langu baada ya siku hizo zote za maandalizi tena mbele ya wanuna walioniona kama kielelezo chao tangu walipozaliwa. Nikasajiliwa!

Sikujua, hakika sikujua, sikujua shule ya upili ya kitaifa yaweza kuwa hivi. Kweli mwanafunzi aweza kukosa viatu na hata kushindwa kununua rangi ya kupaka viatu hivyo iwapo amenunuliwa na wahisani? Nilimlaumu nina maana hakunieleza kuwa mtu anaweza kula chakula ambacho mbwa wetu hawezi hata kukiangalia. Nilipoingia katika ukumbi wa chakula nilihisi kitefutefu nusura

nichafukwe na moyo, makapi ya mboga na uchafu usioelezeka ulinikumba, kisha nikapewa kisahani cha plastiki na kupakuliwa kipande cha ugali ambacho bado kilikuwa na unga na kuachiwa hiari ya kukila au kukitupa. Wenzangu wakawa wanakirambatia chakula kwa kasi huku mmoja wao alipoona jinsi nilivyokiangalia changu akanihisi nimpe chote na kukimaliza fyu. Wote walikuwa na furaha kemkem na kuajabia utukufu wa shule iliyotukuka ya kitaifa ila mimi.

Baada ya mlo 'rojo rojo', tukaelekea darasani nilikopigwa na mghuma mkubwa. Tulikuwa wanafunzi hamsini na watano katika darasa moja tu! Mwalimu mmoja akaja na kutukaribisha shuleni kisha akatuarifu kuwa atakuwa mwalimu wa darasa letu. Nilipomsikia akinena nusura niishiwe na stahamala, kimombo chake kilinishangaza, hasa matamshi yake yalipungukiwa na kudhirisha athari za lugha ya asili. Nilihisi kana kwamba ningemrekebisha lakini sikudhubutu.

Tukafululiza hadi bweni na nikajilaza kitandani chembamba huku mwingine nisiyemjua lakini asiyejua kuwa kuna nguo maalum za kulala akalala uchi katika ghorofa ya juu ya kitanda chetu. Mgeni njoo mwenyeji apone maana baada ya muda wadudu ambao sikuwahi kuwaona aushini mwangu wakanza kunishambulia. Nikaamka baada ya kumnasa mmoja wa wadudu hawa na kuuliza mmoja wa wenzangu ni wepi wadudu hawa na kwa kutojali hata kidogo, akanieleza kuwa hawana neno bali ni kunguni tu, sikujua na kwa kweli mama hakuniambia kuwa kuna wadudu wanaotafuna mtu na hunuka fye! Sikulala kwa hofu huku wenzangu wakiforota kwa njia ya kunighasi. Sikuwahi kudhani kuwa watu wengi wanaweza kulala chumba kimoja huku changu kikiwa na hamamu na vifaa vyote muhimu kikibaki bila mtu!

Tulisomeshwa na walimu wasiojali kana kwamba tunaelewa au la. Hawakushughulika iwapo tulifanya kazi za ziada au la, ndio, hakujali chochote. Kilichonishangaza ni kuwa wanafunzi waliojiunga nasi kutoka shule za umma wenye alama duni waliwapenda na kuelewa haraka walichosomeshwa na hawakujali matamshi yao, labda hawakuyatambua.

Hatimaye tukafanya mtihani wa mwisho wa muhula wa kwanza. Nilishangaa ghaya iliponibainikia kuwa aliyetuongoza alikuwa ghulamu mmoja mshamba niliyempuuza tu mvulana kutoka kijijini ambacho singetambua katika ramani ya nchi ambaye hata vitu vya kimsingi vilimpiga chenga. Nikafanya uchunguzi nikatambua mwenzangu alikuwa na alama mia mbili hamsini na tatu akitoka katika darasa la nane, nilifanikiwa kuwa nambari mia mbili hamsini na tatu kwa jumla ya wanafunzi mia tatu! Tulipofunga kwa likizo ya Pasaka nikaamua kuchukua hatua nyingine sitawahi kuhama kutoka shule hii ya upili wala kuwa zaidi ya nambari kumi!

**<u>Maswali</u>**

***a)*** Thibitisha kauli kuwa msimulizi ana msimamo thabiti **(alama 2)**

***b)*** Tofautisha jinsi mwandishi alivyofunzwa katika shule ya kibinafsi na shule ya upili. **(alama 3)**

***c)*** Taja mambo matatu yanayotuonyesha kuwa msimulizi alilelewa katika aila ya kikabaila kulingana na aya ya pili. **(alama 3)**

***d)*** Andika masuala matatu yaliyomshangaza katika shule ya upili **(alama 3)**

*e)* Andika tamathali mbili zilizotumika katika kifungu. **(alama 2)**

*f)* Eleza maana ya msamiati huu kama ulivyotumika katika kifungu. **(alama 3)**

*a)* alimstahi

*b)* kughairi

*c)* kunighasi

**2. UFUPISHO** **ALAMA 15**

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali***

Mwana wa Adamu ni kiumbe cha ajabu! Ni kiumbe kilichopewa uwezo wa kuhodhi na kumiliki kila kitu, kiumbe kilichopewa akili na maarifa fuvu tele ili kutaratibu shughuli na mambo: kiumbe kilichopewa uwezo wa kuwasiliana na kutumia sauti nasibu ili kuwa na urari na muwala; kiumbe kilichopewa uwezo wa kufaidi viumbe wengine kwa njia mbalimbali na jumla jamala; hiki ndicho kiumbe kilichopewa idhini maalum ya kuzaana na kujaza dunia. Huyu ndiye mwana wa mama Hawa ambaye sasa amegeuka ndovu kumla mwanawe.

Kwa sababu ya bongo alizonazo, binadamu ana uwezo wa kutumia teknolojia kwa manufaa yake na ithibati zipo tele. Binadamu ametumia nyambizi kuzuru chini ya bahari, amefika mwezini, amevumbua magala: amevumbua uyoka: amevumbua tarakilishi na sasa shughuli zake ni za kutandaridhi. Mwenyewe yuasema kuwa dunia yake imekuwa kitongoji katika muumano huu.

Chambilecho wavyele, akili nyingi huondoa maarifa. Binadamu amekuwa dubwana linalojenga kushoto na kubomoa kulia na tuna sababu ya kulisoza dubwana hili kidole. Rabana ndiye msanii asiye mfanowe kwani aliisawiri murua. Rabuka akaona yote yalikuwa mema na mazuri: akamwambia binadamu," Haya twende kazi!"

Viwanda vya binadamu vinatiririsha maji-taka ovyo hadi mitoni, maziwani na baharini na matokeo yamekuwa ni vifo vya viumbe vya majini kama samaki ambavyo ni urithi aliopewa na muumba. Hakuna kiumbe kinachoweza kustahimili maisha bila maji safi. Maji yote sasa yametiwa sumu na binadamu kwa sababu ya 'maendeleo' yake. Joshi kutoa katika viwanda vivyo hivyo nalo limehasiri ukanda wa ozone ambao sasa umeruhusu jua kutuhasiri kwa joto kali mno. Siku hizi inasemekana kuwa kuna mvua ya aside inayonyesha katika baadhi ya sehemu za dunia na kuleta madhara makubwa. Labda hata mabahari yamekasirika kwa sababu hivi majuzi katika kile kilichoitwa 'tsunami', bahari lilihamia nchi kavu na kusomba maelfu ya binadamu na kuwameza wazima wazima. Vimbunga navyo vimetokea kwa wingi.

Wataalamu wanasema kuwa viwango vya miyeyuko vitazidi kwa sababu ya joto na kiwango cha maji kitazidi pia. Binadamu atatorekea wapi?

Idadi ya binadamu imezidi hadi kiasi asichoweza kukishughulikia kwa sababu anaijaza kiholela kwa sababu anadai kuwa aliruhusiwa kuijaza. Hii ni imani potovu. Anasahau kuwa alipewa ubongo

wa kuwaza na kuwazua kabla ya kufanya chochote. Dhiki, maradhi na ufukara zimehamia kwa binadamu na kumtia kiwewe'

Binadamu amefyeka misitu kwa kutaka makao, mashamba, mbao, makaa, ujenzi wa nyumba na barabara na mahitaji mengine mengi. Wanyama wamefurushwa na wengi kuangamia kwa sababu ya ukosefu chakula na wengine kushindwa kuhimili mabadiliko katika mazingira. Chemichemi za maji zimekauka nalo jangwa limeanza kutuzuru kwa kasi inayotisha. Kazi ya binadamu imekuwa ya kusukia kamba motoni. Itambidi aanze kujenga kwa matofali ya barafu.

**a)** Bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mwandishi wa taarifa, fupisha aya ya kwanza. **(Maneno 40-50)** **(alama 5)**

**b)** Kwa kuzingatia aya 4 za mwisho, eleza mambo muhimu yanayoshughulikiwa na mwandishi **(maneno 95-105) (alama 8)**

**3. MATUMIZI YA LUGHA.** **ALAMA 40**

**a)** Taja sifa mbili bainifu za irabu /u/ **(alama 2)**

**b)** Tunga sentensi kwa kutumia kiwakilishi huru cha nafsi ya tatu umoja. **(alama 2)**

**c)** Andika umoja wa sentensi zifuatazo. **(alama 2)**

**i)** Wakitaka tuwasamehe waje watuombe radhi kwa waliyotufanyia.

**ii)** Yaliyosemekana kuwa ni yao yameharibiwa na binamuo

**d)** Yakinisha **(alama 2)**

Hasikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini.

**e)** Bainisha shamirisho **kipozi** na **kitondo** katika sentensi ifautayo. **(alama 2)**

Mama alimpikia mwanawe chakula alichokitamani sana.

**f)** Tunga sentnesi moja yenye chagizo ya mahali na ya wakati. **(alama 2)**

**g)** Onyesha mfumo wa sauti katika tungo: Mtumbwini**.** **(alama 2)**

**h)** Tambulisha vipashio **vitatu** vya sarufi ya Kiswahili. **(alama 3)**

**i)** Huku ukitoa mfano, eleza mantiki inayopatikana katika kauli ya kutendua. **(alama 2)**

**j)** Taja matumizi manne ya kiambishi "ki". **(alama 2)**

**k)** Eleza maana mbili ya sentensi ifuatayo. **(alama 2)**

Jambazi lilimwibia Okoth gari jipya.

**l)** Bainisha vishazi huru na vishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo. **(alama 2)**

Nitaenda maktabani ingawa ninaumwa na kichwa.

**m)** Andika katika kauli ya kutendesha **(alama 1)**

Ile pombe aliyokunywa Chacha ilimfanya alewe.

**n)** Changanua kwa kutumia mtindo wa kielelezo matawi. **(alama 4)**

Mtoto ambaye amefika ni ndugu yangu.

**o)** Andika kinyume cha sentensi ifautayo. **(alama 2)**

Huzuni alisifu nduguye aliyekusanya takataka zote. p) Tumia neno 'vibaya' kama:

i) kivumishi

ii) Kielezi

**q)** Tunga sentensi yenye kihuhishi cha 'A' - unganifu katika ngeli ya U - ZI. (alama 1)

**r)** Mbwa wetu amekatwa mkia. Geuza katika hali ya ukubwa. **(alama 2)**

**s)** Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya maneno haya. **(alama 1)**

Mkembe, mkebe

**t)** Tumia ngali kutunga sentensi ili kuleta maana ya: **(alama 2)**

i) Tendo katika hali ya kuendelea

ii) Tendo kutoweza kufanyika kwa sababu ya wakati kupita

**4. ISIMUJAMII** **(ALAMA 10)**

**a)** Kwa nini kulikuwa na haja ya kusanifisha lugha ya Kiswahili. Toa sababu tano. **(alama 5)**

**b)** **"**….sote tunajua kwamba ni kudura. Makiwa!"

**i.** Tambua sajili iliyotumika katika dondoo hili. **(alama 1)**

**ii.** Eleza sifa nne za sajili hiyo. **(alama 4)**

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 9

**102/3**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 3 (fasihi)**

**MUDA: SAA 2½**

**NAME**…………………………………………………………………………………

**SCHOOL**……………………………………………… **SIGN**…………………………

**INDEX NO**…………………………………………… **ADM NO**……………………

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

***a)*** *Andika jina lako, nambari ya usajili, mkondo, sahihi na tarehe katika nafasi ulizoachiwa.*
***b)*** *Jibu maswali* ***manne*** *pekee.*
***c)*** *Swali la kwanza ni la* ***lazima****.*
***d)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Fasihi Simulizi.*
***e)*** *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
**f)** ***Maswali yote ni sharti yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.***

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

**SEHEMU A : SWALI LA LAZIMA (ALAMA 20)**

**1. USHAIRI**

**UTU NI NINI ?**

Utu na ubinadamu, ni kama yai la kuku
Utu ni ile nidhamu,Mola aliyokhuluku
,ubinadamu ni Damu,ya utu wa kila siku
Utu wowote wa mtu,ni kujali mwenzake.

Ye yote mwanaadamu, ana asili ya utu,
Ya'ni kwenye yake damu, hakikosi hiki kitu
Utu sifa maalum, ya mtu kuitwa mtu,
Utu wowote wa mtu, ni kujali mwenzake

Utu ni kiumbe hai, tunacho chaonekana
Utu kamwe haudai, tabia ya kujivuna,
Utu ni ule uhai, ushikao uungwana,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Utu huweza pimika, kwa hisia ya akili,
Huwezi kuhifadhika, kulingana na Fadhili,
Utu huweza pendeka, palipo na maadili
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Utu unayoaibu, na tabia ya muhali,
Utu huenda na jibu, la Imani na ukweli,
Utu huiona tabu, tabia ya ujahili,
Utu wowote wa mtu ni kuwajali wenzake

Filosofia ya utu, inapinga ubinafsi,
Utu hautaki kitu, cha upeke wa nafsi,
Utu hauna kiatu, cheupe au cheusi
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Utu wa kweli kwa mja, ni mwenzake kuwajali,
Utu huinoa haja, ya kujua watu hali,
Utu ni kuwa pamoja, kwenye shida mbalimbali
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Utu ni ubinaadamu, udugu na wenzi wako,
Utu wote waheshimu, kwa nidhamu na kicheko,
Utu ona mwanadamu, sijitenge peke yako,
Utu wowote wa mtu,ni kuwajali wenzake

Ingawaje tu dhaifu, katika ubinafsi,
Utu kweli nausifu, ubinadamu halisi,
Utu ni safi tukufu, iletayo kila nemsi,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

a. Tambua aina ya shairi hii kwa kutolea ithibati. **(Alama 2)**
b. Taja sifa tano za mtu mwenye utu kulingana na shairi. **(Alama 5)**
c. Tambua mbinu mbili za kimtindo zilizotumiwa na mshairi**.** **(Alama 2)**
d. Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. **(Alama 3)**

**I.** Vipande
**II.** Vina
**III.** Mpangilio wa maneno

e. Tambua nafsineni katika shairi**.** **(Alama 1)**
f. Tambua mbinu tatu alizotumia mshairi ili kukidhi mahitaji ya kiarudhi. **(Alama 3)**
g. Andika ubeti wa saba kwa lugha ya nathari**.** **(Alama 4)**

**SEHEMU B : RIWAYA**

**Nguu za Jadi :** *Clara Momanyi*

Jibu swali la 2 au 3

**2.** ‘’ Aah, si unajua wale watu hatari. Lakini hawatakuwa na nguvu tena. Njia zao zote nitazifunga…’’

a. Eleza muktadha wa dondoo hili**.** **(Alama 4)**
b. Jadili hatari zilizosababishwa na watu wanaorejelewa na msemaji. **(Alama 10)**
c. Msemaji ananuia kuzifunga njia za warejelewa vipi**?** **(Alama 6)**

**3.** Fafanua sifa na umuhimu wa wahusika wafuatao. **(Alama 20)**

a. Sihaba
b. Mwamba
c. Mrima
d. Chifu Mshabaha

**SEHEMU C TAMTHILIA**

*T. Arege***: Bembea ya Maisha**

Jibu swali la 4 au la 5

‘’…wakati mwingine mwindaji huwa mwindwa. Hata kijijini wanaishi watu. Watu hao hawakumbwi na dhiki kiasi hiki. Ya nini kung’ang’ana kuyatafuta Maisha kama kwamba hayapatikani?Maisha mshumaa uso mkesha!Ukijiachia sana peupe hata upepo unaweza kuumiza kabla ya Kulika hadi nchani.’’

**<u>Maswali</u>**

**4.a.**Eleza muktadha wa dondoo hili**.** **(Alama 4)**
b.Bainisha toni katika kauli hili**.** **(Alama 2)**
c.Eleza vipengele vinne vya kimtindo alivyotumia msemaji kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe. **(Alama 4)**
d.Eleza umuhimu wa msemaji katika kuendeleza ploti ya tamthilia hii**.** **(Alama10)**

**5.a.**Fafanua umuhimu wa mazungumzo kati ya Luka, Beni na Yona katika kujenga tamthilia ya ‘’Bembea ya Maisha.**’’** **(Alama 10)**

b. ‘’Bembea inapolika na kukatika haiwi mwisho wa michezo.Huungwa na mchezo kwanza tena.’’Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kutolea mifano mwafaka tamthiliani. **(Alama 10)**

**SEHEMU YA C**

***Hadithi Fupi – Mapambazuko Ya Machweo Na Hadithi Nyingine – Dw Lutomia***

***Jibu swali la sita au la saba***

**6. Jadili** maudhui ya taasubi ya kiume katika hadithi ya fahila za punda. **(Alama 20)**

**7.**Racheal Wangare:Fadhili za Punda

"Rudi, nyumbani mwanamke wewe! Nitakuja jioni tuyamalize haya."

a)(i)Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama4)**

(ii) Fafanua hulka ya msemaji wa kauli hii **(alama4)**

iii) Huku ukizingatia hadithi hii, jadili maudhui ya mabadiliko yanavyojitokeza katika hadithi **(alama7)**

**b)** Changanua mtindo katika dondoo hili **(alama 5)**

Alasiri ile, baada ya ibada mbili, mhubiri akawa hoi kwa mavune. Akatamani kufika nyumbani apumzike, kazi ya kuwalisha kondoo wa Mungu si kazi rahisi. Wamefika nusu safari, bintiye katulia kama maji ya mtungi. Akimtazama kipembe anamkumbusha marehemu mkewe. Miaka mitatu sasa na dhiki ya kuondokewa haijamwisha. Alihisi ukiwa, akatamani mwenziye. Sasa kazi kukilea kitoto chao, kibinti hiiki kilicho mlanda mamake kama shilingi kwa ya pili. Nyuma ilijaa kicheko alipokua hai mamake. Kama si bintiye ambaye ulimi wake hautulii, kiroho kingemvamia labda hata kumvuta kuelekea kaburini .

**SEHEMU D: FASIHI SIMULIZI**

8. **Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali.**

Hapo zamani za kale, Nyani na mamba walikuwa marafiki wa kufa kuzikana. Watoto wao walipendana na kufaana kama ndugu wa toka nitoke. Familia ya mamba aliishi mtoni nayo ya Nyani aliishi katika msitu uliokuwa maili thelathini kutoka mtoni. Kila mara marafiki hawa walitembeleana na kusaidiana kwa hali na mali. Kwa vile mamba alikuwa mvivu msahuhuri, aliweza kumwauni Nyani na aila yake kwa Samaki wa aina mbalimbali. Nyani naye alimpelekea mamba matunda na nafaka kutoka shambani mwake.

Urafiki wao ulikita mizizi na kunawiri zaidi wakati mamba alipokuja kwa Nyani kumposea mwanawe binti. Ukwe uliutilia viungo uhusiano wa Nyani na mamba wakawa wanagandana kama kupe na mkia wa ng'ombe. Wakatenda mengi Pamoja. Wakazungumza ya kupwa na ya kujaa. Hakuna hata mmoja wao aliyeutilia shaka uaminifu wa mwenzake. Wake zao nao walifuata kaida ya maji kufuata mkondo. Walikuwa masahibu wa chanda na pete. Msimu mmoja wa mapukutiko ulishuhudia mabadiliko ya kudumu katika maisha ya Nyani na mamba. Wakati huo, bahari ilichafuka si haba. Kazi ya mamba ya uvivu ikaanza kukabiliwa na majabali ya kila aina. Kila mara mamba alipokwenda uvuvini, alirudi akichekelewa na nyavu zake. Hakuambulia chochote. Njaa ilianza kubisha hodi katika familia ya mamba. Hali hii ilitishia kuitia ufa urafiki kati ya mamba na Nyani. Mamba alivamiwa na pepo ambaye hata yeye alishindwa kumfahamu. Kila mara alipomwona. Nyani au Watoto wake alitamani kumdakia na kumla mzima mzima. Kadiri kujiasa dhidi ya fikira hii mbovu ndivyo moyo wake ulivyo endelea kumshauri, '' Una njaa bwana, familia yako itaangamia. Je huoni rafiki yako na familia yake wanaweza kuwa kitoweo ? Utaendelea kula wishwa hadi lini? Mbona huyo Nyani ambaye alijiita rafiki yako sasa amekata guu humu? Mbona haji tena kukutazama hata karafu alizokuwa akikuletea ameacha kuleta."

Mamba akaanza kumshuku rafiki yake na akasadiki kuwa nyali alikuwa mla naye tu. Usiku mmoja baada ya kula mate na kujilaza kitandani mwenzake akihesabu nyota, wazo lilimjia.

Alikata shauri kumlaghai rafiki yake wa miaka mingi iliapate kujiokoa yeye na familia yake kutoka katika kinamasi cha njaa. Asubuhi yake alikwenda kwa Nyani akiwa amejinamia kwa jitimai. Alisema, ‘’Rafiki yangu, jana tulipoagana nilipata tanzia. Mjumbe kutoka kijijini aliniarifu kuwa baba yangu ni mgonjwa mahututi. Alisema kwamba baba ananitaka nyumbani upesi,’’ Habari hizi zilimtia Nyani majonzi makuu. Alimwahidi mamba kwamba wangeandamana Pamoja. Kwa vile Nyani hangeweza kutembea majini ilibidi abebwe na mamba. Alipatwa na kichefuchefu na manyezi kila alipotazama Bahari iliyojitandaza mbele yao kwa mbwembwe. Hata hivyo, mamba alimhakikishia kuwa wangefika salama. Naye kwa Imani iliyotokana na urafiki na mazoea ya miaka mingi, alitulia.

Safari ilikuwa ndefu na yenye machovu yaliyomfanya Nyani kulala mgongoni mwa mamba. Walipofika kwenye vina vya maji, mamba aliamua kumpasulia mbarika Nyani. ‘’rafiki yangu,nimekuwa nikidhani wewe ni rafiki wa dhati,kumbe uzuri wako wa mkakasi?mimi na wanangu tumetafuna na njaa kwa miezi kadha sasa huku maghala yako yakishiba na kutapika chakula. Hujadhiriki hata siku moja kuja kujua kama nimepata hata senti moja ya kusagia mkunguni. Jana usiku nilipokuwa nikiwazia hali yangu, nilioteshwa katika ndoto kwamba kama ningepata moyo wako na kuula, basi hali ya uhitaji ingeniishia. Moyo wangu unaniuma sana kukufanyia tendo hili, hata hivyo nilisobudi hutendwa’’

Nyani alipigwa na butwaa nusura moyo wake mwenyewe ujikabidhi kwa mamba. Hata hivyo, akili yake nyepesi ilifanya kazi. Alimwambia mamba, ‘’ ndugu yangu, pole sana ikiwa umekuwa unadhani sikujali. Kwa kweli, hata ungeniomba moyo wangu siku hizo ningekupa tu. Umejua tena sisi Nyani, tumbili na kima tuna mioyo mingi. Hata hivyo nasikitika kuwa Mungu alituambia kuwa daima mioyo yetu itakaa mitini. Basi ndugu mpenzi, badala ya kuendelea na safari hii, turudi pale mtini nikupe moyo wangu pamoja na mitatu ya mwanangu kusudi uwalishe wanao na mkeo.’’ Mamba akaingia mtegoni. Wakarudi hadi ufuoni. Kwa vile mamba hakuweza kutoka majini, alibaki ufuoni akimngojea rafiki yake amlete mioyo.

Mamba alitunga macho yake kwenye ujia alioufuata Nyani akiomba pasitokee lolote la kumchelewesha Nyani. Matumbo yalimguruma kwa njaa. Roho ikampapa kwa tumaini. Alingoja, akongoja,akangoja…wiki,miezi,mwaka… Nyani hakurudi. Mamba akajua amepwaguliwa na Nyani. Akaapa kumtafuta kwa udi na ambari.huo ukawa mwisho wa urafiki kati ya Nyani na mamba. **Hadithi yangu inaishia hapa.**

**<u>Maswali</u>**

a.Tambua kipera cha utungo huu. Thibitisha. **(Alama 2)**

b.Tambua mbinu sita kimtindo alizotumia mtambaji wa utungo huu. **(Alama 6)**

c.Umepewa jukumu la kutamba ngano hii. Fafanua mambo Matano muhimu utakayozingatia ili kufanikisha uwasilishaji wako. **(Alama 5)**

d. fafanua umuhimu wa ngano hii katika jamii. **(Alama 3)**

e. Kwa kutoa hoja nne jadili umuhimu wa maneno yaliyokolezwa rangi katika utambaji wa ngano kama hizi. **(Alama 4)**

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 10

**102/1**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 1 (INSHA)**

**MUDA: SAA 1¾**

**NAME**……………………………………………………………………………………

**SCHOOL**…………………………………………… **SIGN**…………………………

**INDEX NO**………………………………………… **ADM NO**………………………

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

- **a)** *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
- **b)** *Andika insha **mbili**. Insha ya **kwanza** ni ya **lazima.***
- **c)** *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya tatu zilizobakia.*
- **d)** *Kila insha isipungue maneno **400***
- **e)** *Kila insha ina alama **20***

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 40 | |

**Swali la kwanza ( lazima)**

1. Wewe ni Gavana wa gatuzi mojawapo katika nchi ya Kongomano. Wakaazi wa mji wa Songambele wamekiuka sheria zilizowekwa na baraza la gatuzi hilo. Waandikie ilani

2. Jitihada za kumwinua mtoto wa kike zimepeleka kudhalilishwa kwa mtoto wa kiume.Jadili.

3. Andika kisa kitachodhihirisha maana ya methali.

Ulimi huuma kuliko meno

4. Tunga kisa kitakapomalizika kwa kauli ifuatayo**….** Nilijitazama na kujidharau. Kwani nini nilijiingiza katika hali hii?  Nilijuta.

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 10

**102/2**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 2 (LUGHA)**

**MUDA: SAA 2½**

**NAME**……………………………………………………………………………………

**SCHOOL**……………………………………………… **SIGN**…………………………

**INDEX NO**…………………………………………… **ADM NO**……………………

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**Maagizo**

***(a)Andika*** *jina na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

***(b)****Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani*

***(c)*** *Jibu maswali yote.*

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 4 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| | | |

**A. UFAHAMU** **(ALAMA 15)**

**Soma makala yafuatayo kasha ujibu maswali**

Ajali haina kinga. Watu wengi wanapotajiwa neno ajali, fikira zao hukimbilia moja kwa moja hadi barabarani. Mara chachemawazo yao huenda viwandani, mashambani au kwenye viwanja vya michezo. Ni nadra sana watu kufikiraia kuwa nyumbani ndiko ajali nyingi zinztokea.

Idadi kubwa ya ajali nyumbani hutokea kimchezo tu. Watu wengi wameteleza msalani na wanapata majeraha mabaya. Wengine wameteleza walipokanyaga vitu vyenye unyevu sakafuni, kama vile mafuta, mabaki ya chakula au hata maganda ya ndizi. Ulemavu walio nao watoto na hata watu wazima hutokana na ajali kama hizi wasizofikiria wtu wengi.

Ajali vilevile hutokea watu wanapozama katika shughuli au kupata jazba kuu ya kutenda. Katika hali hii, huweza kujiumiza au kuwaumiza wengine bila kujua.

Hapa tunazungumzia watu ambao hujaribu kubebe mizigo yenye uzani wasiokadiria. Madhara huwa kuteguka viungo na kuchanika misuli. Aghalabu hulemewa na kubanwa. Mwandishi wa makala haya siku moja alipanda kibao kuangika picha ukutani. Ingawa alikuwa mfupi, ari ilimsukuma kuchuchumia. Matokeo ni kibao kilijisukuma nyuma. Mhusika alianguka akajigonga kidevu. Kitendo hiki kilisababisha yeye kujiuma ulimi vibaya. Kuvunjika jino na hata kuzirai. Bahati ni kuwa alikuwepo mtu aliyempa huduma ya kwanza na kumkimbiza hospitalini.

Hat hivyo ajali nyingi hutokana na vifaa vya nyumbani. Zana hizi ni pamoja na visu, meko ya gesi, mashine zinazotumia umeme na kadhalika na huwa hatari sana, hasa kwa watoto. Kitu kidogo hata kama wembe huweza kusababisha madhara makubwa. Kwa hakika hakuna yeyote kati yetu, hata waliokulia katika makasri ya fahari asiye na kovu. Makovu haya ambayo tunayaficha katika mavazi yetu ni ishara ya majeraha kutokana na ajali nyumbani. Je una kovu lolote? Unakumbuka ulivyolipata?

Ingawa ajali hizi haziepukiki, yawezekana kuzipunguza. Ni muhimu kukuza tabia na mazoea ya kuwa waangalifu nyumbani. Kwa mfano, ni hatari kuepua chungu chenye maji yanayotokota mekoni kwa mikono mitupu. Aidha ni kutowajibika kuchanganya kitu chochote chenye unyevu na mafuta moto mekoni. Watu wengi wamebambuka ngozi na nyumba kuteketea kwa namna hii. Kwa hivyo ni vizuri kupata ujuzi wa jinsi ya kutumia vifaa na kuhakikisha tunavirudisha ipasavyo.

Jambo la tatu na muhimu zaidi ni kuwepo kwa vifaa pamoja na uwezo wa kutoa huduma ya kwanza. Inawezekana kuokoa maisha au kuounguza majeraha kwa kuchukua hatua za dharura.

**Maswali**

1. Eleza maana ya methali 'Ajali haina kinga' **alama 2)**
2. Kwa nini mwandishi anasema ajali nyumbani hutokea kimchezo? **alama 3)**
3. Ni mambo gani mengine yanayosababisha ajali nyumbani? **alama 3)**
4. Onyesha vile invyowezekana kupunguza ajali nyumbani. **alama 3)**

**5.** Eleza maana ya: **(alama 4)**

**(i)** jazba

**(ii)** makasri

**(iii)**makovu

**(iv)**kuepua

**B. UFUPISHO** **(Alama 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali**

Ardhi ni mali ya taifa. Hivyo inampasa kila raia kuinafidhi. Hii ina maana kwamba hatuna budi kuwarithisa wana na wajukuu, vitukuu na vilembwe, vining'ina na wapwa zetu ardhi yenye rutuba. Ardhi ndiyo chanzo cha riziki zote. Fauka ya hayo, ardhi ni dafina kubwa.

Tangu asili ardhi hii imefunikwa na joho la miti na majani. Rutuba ilienea kila mahali. Lakini wakati ulifika ambapo wanadamu hawakuvumilia kukaa bila kuitumia johari hii. Walishika maparange na mashoka. Wakafyeka majani na miti yote. Wakalima wakapanda na kuvuna.

Kisha walihama hapo. Waliendelea kufanya hivyo mwaka hadi mwaka. Hali ya kufyeka sehemu mbalimbali za nchi, kuchoma mioto ovyo, kuwa na mifugo mingi na kutojua kuhifadhi ardhi vizuri kulileta mavuno hafifu kila mwaka.

Mvua iliponyesha matone ya mvua yaligonga ardhi. Maji yakajiri kwa nguvu na kutawanya chembe za udongo. Wakati wa kiangazi udongo ulipokauka, upepo mkali ulichukua tabaka la juu. Hivyo ikawa mazao hayawezi kustawi. Hatimaye nchi ikawa kama mkuranga. Mambo haya yakasababisha mmomonyoko wa juu juu halafu mwanzo wa michirizi na mwisho makorongo na maporomoko ya ardhi.

Walakini basi ya kale hayapo. Sasa wakuu wa serikali yetu ya Insafu wamekuhimizeni, ikiwa mu wakulima, mpande zaidi. Wamewashauri namna ya kuongeza mavuno katika mashamba yenu kwa maarifa bora ya zaraa, kama vile kuunafidhi udongo, kutumia mbolea, njia za kunyunyizia dawa makondeni ili kuua wadudu wanaoharibu mimea, na kutumia maarifa malihi katika kupanda mbegu. Kwa wale ambao si wakulima, serikali yetu ya Insafu imeweka shule za mafundisho maalum na kumhimiza kila mmoja wao aongeze maarifa yake na afanye kazi kwa tabasuri na bidii ili aongeze mapato yake na mapato ya serikali pia. Katika sehemu nyingine maelezo ya wakuu wa serikali yamefuatwa barabara, na kumetokea maongezeko malihi ya mazao.

Walakini pia katika sehemu hizo maongezeko yake hayakutosha sana. Katika sehemu nyingine kwa bahati mbaya watu wamepotezwa na watu wakaidi ambao kwa kutaka ushaufu, wamewaambia watu kuwa njia rahisi na nyepesi ya kujipatia serikali ya kujitawala yenyewe, na wamewashawishi na kuwatisha baadhi ya watu waasi amri za serikali zihusuzo zaraa. Wahaini hao wametibua mambo. Ni watu wa kuaili na ni afkani.

**Maswali**

**a.** Fupisha ujumbe wa aya tatu za kwanza kwa maneno 80. (alama 9, 1 ya mtiririko)

**b.** Eleza masuala ambayo mwandishi anaibua katika aya mbili za mwisho kwa maneno 60. (alama 6, 1 ya mtiririko)

**C. MATUMIZI YA LUGHA**

**(a)** Taja sauti **mbili** ambazo huitwa likwidi **(alama 1)**

**(b)** Andika neno lililo na muundo wa silabi ufuatao **(alama 1)**

IKKI ……………………………………………………………

**(c)** Ainisha viambishi katika neno lifuatalo **(al. 2)**

yafutikayo………………………………………………………………………

**(d)** Tambua aina mbili za sentensi ukizingatia uamilifu na utoe mfano mmoja kwa kila moja **(ala. 2)**

**(e)** Ainisha vielezi vya namna katika sentensi hii **(ala. 2)**

Mzee huyu mkongwe alicheka kijinga huku akila haraka haraka

**(f)** Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo **(ala. 2**

Kijana aliyezungumza na nyanyake ameingia katika darasa lililochafuliwa na wanafunzi

**(g)** Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha <u>mstari</u> **(ala. 3)**

Mwanafunzi mwerevu sana aliyekuwa mgonjwa jana amepelekwa nyumbani

**(h)** Bainisha shamirisho na chagizo katika sentensi ifuatayo **(ala. 3)**

Somo aliukata mti kwa kisu jana asubuhi

**(i)** Andika kwa usemi wa taarifa **(ala. 3)**

Karani: Njoo nikutume kwa babu yangu.

Karanja: Sitaki kupita njia ya kwa babu

**(j)** Eleza matumizi ya 'ni' katika sentensi hii **(ala. 2)**

Ingieni darasani mara moja ili niwape zoezi ambalo ni rahisi

**(k)** Eleza maana ya sentensi zifuatazo **(ala. 2)**

**(i)** Ningalisoma kwa bidii ningalipita mtihani

**(ii)** Ningesoma kwa bidii ningepita mtihani

**(l)** Andika katika udogo wingi **(ala. 2)**

Mti wa msonobari unatengeneza meza nzuri sana

**(m)** Tambua miundo yoyote mitatu ya ngeli ya LI-YA **(ala. 3)**

**(n)** Eleza maana **tatu** za sentensi ifuatayo **(ala. 3)**

Alisema angeenda kwao

**(o)** Andika upya sentensi ifuatayo katika hali ya 'a' **(ala. 1)**

Mwanafunzi anasoma darasani

**(p)** Tumia neno 'hadi' kuonyesha mahali na wakati katika sentensi **(ala. 2)**

**(q)** Yakinisha katika hali ya mazoea. **(ala. 2)**

Asiyeugua hahitaji daktari

**(r)** Tunga sentensi ukitumia neno 'komaa' kama **(ala. 2)**

**(i)** kivumishi

**(ii)** nomino

**(s)** Taja matumizi yoyote mawili ya <u>kistari kirefu</u> **(ala. 2)**

**D. ISIMU JAMII**

**(a)** Kwa nini kulikuwa na haja ya kusanifisha Kiswahili? Toa sababu tano **(ala. 5)**

**(b)** Fafanua sifa za lugha ya kazi **(ala. 5)**

# KCSE 2025 CROSS-COUNTRY MOCKS

## JARIBIO LA KITAIFA 10

**102/3**

# KISWAHILI

**KARATASI YA 3 (fasihi)**

**MUDA: SAA 2½**

**NAME**……………………………………………………………………………

**SCHOOL**………………………………………………… **SIGN**…………………………

**INDEX NO**……………………………………………… **ADM NO**……………………

*Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)*

**MAAGIZO**

a) *Andika jina lako, nambari ya usajili, mkondo, sahihi na tarehe katika nafasi ulizoachiwa.*
b) *Jibu maswali **manne** pekee.*
c) *Swali la kwanza ni la **lazima**.*
d) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Fasihi Simulizi.*
e) *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
f) ***Maswali yote ni sharti yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.***

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

**SEHEMU A:FASIHI SIMULIZI** **(ALAMA 20)**

**1. LAZIMA**

Hamkuona jinsi tulivyowapiga mabao
Hamkuona vile tuliwachezea kama watoto,tuliwachenga kila mara
Hamkuona waliponea tundu la sindano tungewapiga mabao kumi na mbili
Ingekuwaje timu mbovu kama hii kucheza na miamba kama sisi?
Niliwafunga baada ya sekunde wakati ule nitashindwaje leo?

**Maswali**

a) i)Tambua kipera kinachodokezwa na maelezo haya na ukifafanue. **(alama 2)**

ii) Fafanua sifa zozote sita za kipera ulichotambua katika (a) **(alama 6)**

b)i)Wewe ni miongoni mwa wale wanaotambiwa ngano katika kikao cha utambaji wa ngano.Fafanua mambo sita ambayo unaweza kuchangia ili kufanikisha uwasilishaji wa utambaji. **(alama 6)**

ii) Umeanza mikakati ya kukusanya data kupitia mbinu ya mahojiano. Eleza changamoto sita ambazo unaweza kukumbana nazo nyanjani. **(alama 6)**

**SEHEMU B:TAMTHILIA**

**Timothy M.Arege :Bembea ya Maisha**

*Jibu swali swali la 2 au la*

**2.** Mama!Mamangu mzazi ni mboni ya jicho kwetu.Ananihitaji kipindi hiki cha lala salama.

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

b) Tambua mbinu tatu za lugha zinazojitokeza katika dondoo hili. **(alama 3)**

c) Fafanua sifa za mhusika '***mamangu mzazi'*** ukirejerea tamthlia nzima. **(alama6)**

d)Fafanua majukumu ya elimu katika jamii kwa mujibu wa tamthlia ya Bembea ya Maisha. **(alama 7)**

***au***

**3.** "Sara: Si neno mama!(kimya).Hakuna kizuri kijacho kwa urahisi.Mazuri hutoka mbali na wakati mwingine yana hadithi za kutisha.Maisha yetu ni mfano wa mbegu iliyopandwa .Mbegu hiyo haina budi kuoza kwanza ndipo ioteshe mche upendezao."

a) Changanua mtindo katika dondoo hili. **(alama 8)**

b) "Sasa hali ni tofauti. T<u>amaduni,mila na desturi</u> zetu zimezidi kuyakubali mabadiliko."

i) Eleza nafasi ya msemaji wa kauli katika (b),katika kuendeleza tamthilia husika. **(alama 6)**

ii) Wahusika mbalimbali katika tamthilia ya *Bembea ya Maisha* wamebuni mikakati mwafaka ili kujikomboa kutokana na kauli zilizopigiwa mstari.Fafanua mikakati **sita** kutoka tamthliani. **(alama 6)**

**SEHEMU C: RIWAYA;Clara Momanyi: Nguu za Jadi**

**Jibu swali la 4 au 5**

**4.** Hakujua akimbilie wapi.Sasa afanye nini?Alilitupia lile jinyama lakini likahepa.Alihisi maisha yake yamo hatarini.

a) Yaweke maneno haya katika muktadha wake. **(alama 4)**

b) Kwa kutoa mfano,tambua mbinu mbili za lugha katika dondoo hili **(alama2)**

c) Fafanua umuhimu wa mandhari katika riwaya hii. **(alama 6)**

d) Jamii ya nchi ya Matuo imesheheni vikwazo ambavyo vinakaa kama nguu,na kutoka jadi nguu hizi zimeathiri kwa upana usawa katika jamii.Tathmini kauli hii kwa hoja **sita.** **(alama6)**

***au***

**5**. Hivyo,alitaka kubadili hali hata kama ilimaanisha kukitia kichwa chake kinywani mwa simba. Alitaka kuliokoa jahazi lililokuwa likielekea mwambani kwa kasi. Lakini angeliweza vipi kupambana na utandu wa mahasidi hao?

**a) ) Fafanua** umuhimu wa anayerejelewa dondooni katika kukuza na kuendeleza vitushi riwayani. **(alama 4)**

**b) Eleza** sababu za mrejelewa kutaka kufaulisha kauli iloyopigiwa mstari. **(alama 10)**

**c)** Mwandishi wa riwaya ya Nguu za Jadi amefanikiwa kutumia **mbinu ya majazi** katika kukuza wahusika na mandhari mbalimbali riwayani.Fafanua kwa kutolea mifano **sita**. **(alama 6)**

## SEHEMU D: USHAIRI

**Jibu Swali la 6 au 7**

6. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

**Barabara.**

Barabara bado ni ndefu
Nami tayari nimechoka tiki
Natamani kuketi
Ninyooshe misuli
Nitulize akili

Lakini

Azma yanisukuma
Mbele ikinihimiza kuendelea
Baada ya miinuko na kuruba
Sasa naona unyoofu wake
Unyoofu ambao unatisha zaidi.

Punde natumbukia katika shimo
Nahitaji siha zaidi ili kupanda tena,
Ghafla nakumbuka ilivyosema
Ile sauti zamani kidogo
“Kuwa tayari kupanda na kushuka”.

Ingawa nimechoka
Jambo moja li dhahiri
Lazima niifuate barabara
Ingawa machweo yaingia
Nizame na kuibuka

Nipande na kushuka
Jambo moja nakumbuka: Mungu
Je, nimwombe tena?  Hadi lini?
Labda amechoshwa na ombaomba zangu
Nashangaa tena!

Kitu kimoja nakiamini
Lazima niendeleee kujitahidi kwa kila hatua mpya
Nijikokote kuiandama hii barabara yenye ukungu
Nikinaswa na kujinasua,
Yumkini nitafika mwisho wake
Ikiwa wangu mwisho haitauwahi kabla.

***(Timothy Arege)***

**Maswali:**

(a) Taja aina ya shairi hili. **(alama 2)**
(b) Eleza toni ya shairi hili. **(alama 2)**
(c) Fafanua dhamira ya shairi hili. **(alama 2)**
(d) Bainisha vipengele vifuatavyo vya kimtindo katika shairi hili. **(alama 3)**
(i) Tanakuzi
(ii) mbinu rejeshi
(iii) Taswira
(e) Eleza umuhimu wa maswali balagha katika shairi. **(alama 2)**
(f) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari. **(alama 4)**
(g) Eleza matumizi ya mistari mishata katika shairi hili. **(alama 2)**
(h) Eleza muundo wa shairi hili. **(alama 3)**

**AU**

***7. Soma shairi  hili kisha uyajibu maswali;***

Jicho, tavumiliaje, kwa hayo unayo?
Kicho, utasubirije, maonevu yapitayo?
Kwacho, lijalo nalije, nimechoka vumiliyo
Naandika!

Moyo, unao timbuko, maudhi tusikiayo
Nayo, visa na mauko, wanyonge yawakutayo,
Kwayo, sina zuiliko, natoa niyahisiyo
Naandika!

Hawa, wanatumuliya, dhiki wavumiliayo
Hawa, mamiya, na mali wazalishayo
Hawa, ndo wanaumiya, na mafia wakutayo
Naandika!

Hawa, sioni wengine, kwao liko angamiyo
Hawa, huwapa unene, watukufu wenye nayo
Hawa, bado ni wavune, kwa shida waitikayo
Naandika!

Bado, wawapo mabwana, wenye pupa na kamiyo
Bado, tofauti sana, kwa pato na mengineyo
Bado, tuling'owe shina, ulaji pia na choyo.
Naandika!

**Maswali**

a) Malenga wa shairi hili alidhamiria kufafanua masuala kadhaa yanayokumba Jamii.Taja **manne** ya masuala haya kwa kurejerea shairi. **(alama 4)**

b) Tambua bahari za shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo; **(alama 4)**

i) vina
ii) kibwagizo
iii) idadi ya vipande
iv) mishororo

c) Kwa kutoa mifano,tambua mbinu **mbili** ambazo mshairi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. **(alama2)**

d) Tambua kwa mifano mbinu **mbili** za kimtindo alizotumia mshairi. **(alama4)**

e) Andika ubeti wa **nne** katika lugha nathari. **(alama 4)**

f)Tambua na ueleze toni katika shairi hili. **(alama 2)**

## SEHEMU E: HADITHI FUPI

**D.Lutomia na Phibbian Muthama:** *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

8***.Fadhila za Punda***

Alipozidiwa akapoteza fahamu.Fahamu zilipomrudia,maumivu yakamvamia.Mumewe hakuonekana,amejiendea na kumwaacha afilie mbali.Alilia machozi yakamwisha.

a)Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

b)Taja mbinu **mbili** za lugha zilizotumika katika dondoo hili. **(alama 4)**

c)Fafanua mbinu **nne** za kutambua sifa za mhusika anayerejelewa. **(alama 4)**

d)Kwa kurejelea hadithi "Fadhila za punda" onyesha kwa hoja **nane** ufaafu wa mdokezo wa methali ufuatao: ***maskini akipata makalio hulia bwata*** kwa kutolea mifano mwafaka hadithini. **(alama 8)**

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA**

# MWISHO

# FOR THE FOLLOWING;

- ONLINE TUITION
- REVISION NOTES
- SCHEMES OF WORK
- SETBOOKS VIDEOS
- TERMLY EXAMS
- QUICK REVISION KITS
- KCSE TOPICALS
- KCSE PREMOCKS
- TOP SCHOOLS PREMOCKS
- JOINT PREMOCKS
- KCSE MOCKS
- TOP SCHOOLS MOCKS
- JOINT MOCKS
- KCSE POSTMOCKS
- TOP SCHOOLS PREDICTIONS
- KCSE PREDICTIONS
- KCSE REVEALED SETS

# *To Obtain Copies of Respective Marking Schemes / Answers*

# CALL/TEXT/WHATSAPP

## *0746-222-000*

## *0742-999-000*

*mwalimuconsultancy@gmail.com*

*kcsepredictions@gmail.com*

*This is a Copyright Property of Mwalimu Consultancy Ltd.*

**Powered By Mr Isaboke**

**SUCCESS**